

## **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Sita – Tarehe 13 Aprili, 2011**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatuh Asubuhi)*

**DUA**

Spika (*Mhe. Anne S. Makinda*) Alisoma Dua

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:**

Taarifa ya Mwaka ya Upimaji wa Utekelezaji wa Mamlaka ya Manunuzi ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 (*The Annual Performance Evaluation Report on Public Procurement Regulatory Authority for the Financial Year 2009/2010*).

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 75

**Hitaji la Mji Mdogo wa Kondoa**

**MHE. MOZA ABEDI SAIDY** aliuliza:-

Moja ya sababu za kimsingi za kuanzisha maeneo mbalimbali ya kiutawala ni kurahisisha maendeleo ya Wananchi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha Mji Mdogo wa Kondoa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Moza Abedi Saidy, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mji Mdogo wa Kondoa, ilianzishwa rasmi kwa Tangazo la Kiserikali Na. 137 la tarehe 8 Juni, 1990. Mamlaka ya Mji Mdogo wa Kondoa ilipewa cheti cha kuanzishwa kwake (*Certificate of Establishment of Kondoa Township Authority*) na Halmashauri Mama Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa tarehe 1 Julai, 2000.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mji Mdogo wa Kondoa ilizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 20 Januari, 2005, kwa kipindi hicho akiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Hivyo, hivi sasa ni Mamlaka ya Mji Mdogo wa Kondoa iliyokamilika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kumbukumbu zilizopo, Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa inaendelea na mchakato wa kuipandisha hadhi Mamlaka ya Mji Mdogo wa Kondoa kuwa Halmashauri ya Mji wa Kondoa. Maombi haya yaliwasilishwa na baada ya kupita katika vikao halali, yatafanyiwa kazi na Serikali kwa mujibu wa sheria zilizopo.

**MHE. MOZA ABEDI SAIDY:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri swali lifuatalo:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri anasema kwamba Mamlaka ya Mji Mdogo wa Kondoa imepewa cheti cha kuanzishwa kwake; na kwa kuwa nimefuatilia na nimegundua kuwa cheti hicho hakijafika; je, Naibu Waziri yuko tayari kuongozana nami ili tukahakiki?

**SPIKA:** Mnakwenda kuhakiki cheti jamani, mnaweza kuleta hapa hapa! (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, labda niiweke vizuri hapa, kabla hata sijamwambia kwamba mimi nipo tayari kufuatana naye kwenda Kondoa, lakini kwa mfano Kitongoji, Kitongoji huwa hakisajiliwi kinaanzishwa, Kata huwa haisajiliwi inaanzishwa na hii Miji Midogo huwa inaanzishwa; kinachosajiliwa ni Kijiji kwa sababu kuna masuala ya ardhi na vitu vingine. Kilichopo hapa ni kwamba, zipo kumbukumbu ambazo nimezitaja hapa katika majibu ambazo zinaonesha kwamba, Serikali ilikwishakuridhia. Nimemtaja mtu mkubwa hapa; Waziri Mkuu, alikwenda kule, ndiye aliyezindua wakati huo akiwa Naibu Waziri. Sasa mimi ninashindwa kuelewa tatizo lipo wapi; ninamwomba Mbunge kama kuna tatizo lolote la mawasiliano aje pale ofisini tuzungumze naye na mimi nipo tayari kuondoka naye kwenda Kondoa tukalimalize hilo jambo liishe. (*Makofi*)

**SPIKA:** Alikosea, alifikiri kwamba mnaweza kukaa ofisini akakueleza vizuri na si kwamba mwende Kondoa; ni matumizi mabaya ya fedha za umma. (*Kicheko*)

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. Ninalo swali dogo la nyongeza:-

Kwa kuwa utaratibu na mchakato wa kuanzisha Mji Mdogo wa Madaba katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea ulienda sambamba na mchakato wa kuanzisha Mji Mdogo wa Kibaigwa katika Halmashauri ya Kongwa; na kwa kuwa mpaka sasa maendelezo ya uanzishwaji wa Mji Mdogo wa Madaba bado hayajakamilika ipasavyo kwa Serikali kumalizia shughuli zinazotakiwa:-

Je, Naibu Waziri yupo tayari sasa kufanya mazungumzo rasmi na mimi Mbunge wa Jimbo la Peramiho ambako Mji Mdogo huu utaanzishwa ili mchakato huo ukamilike na Wananchi waweze kufaidi kile ambacho kimeshaazimiwa na kuitishwa rasmi katika vikao vyote husika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, labda kwa kifupi tu niseme kwamba, Halmashauri zinazohusika na Miji hii Midogo ndizo ambazo zinatakiwa zioneshe umuhimu wa kuanzisha hizo Halmashauri. Tunachokitaka pale, eneo hilo liwe na idadi ya watu wasiopungua elfu kumi, kuwepo na huduma za jamii kama vile kituo cha afya, shule za sekondari, soko na maduka ishirini ya rejareja yenye leseni na Mahakama za Mwanzo. Eneo liwe katika Makao Makuu ya Kata au Tarafa. Wakishapitisha katika Halmashauri, wakakubaliana kwamba wao wanafikiri wafanye hivyo, sisi tunapeleka wataalam pale wanakwenda kuangalia. Wakiona kwamba, eneo lile linakidhi, maana yake wanakubalika.

Mheshimiwa Spika, kinachopimwa na kinachoangaliwa hapa ni suala zima la Mipango Miji kwamba; kama Madaba pale pasije pakafika mahali pakajengeka halafu ikafika mahali unataka kuweka nguzo za umeme, unataka kuweka barabara za kuitisha watu au unataka kuweka mitaro ya kutoa maji taka halafu hujui kwamba utaifanya pale. Hata Kibaigwa anapopasema, ni kwa sababu tu ya aina ya biashara inayoendelea pale; kwa hiyo, Halmashauri ikaona kwamba, kuna umuhimu wa kuifanya Mamlaka ya Mji Mdogo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kinachosemwa hapa ni kwamba, Halmashauri yenye we ikishaona kuna umuhimu wa kufanya hivyo, yenye we ndiyo inaleta yale mapendekezo na sisi tunapeleka wataalam tunakwenda kuangalia hivi vigezo tulivyovizungumza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Jenista Mhagama wala asiwe na wasiwasi; sisi tupo tayari kukaa naye na kushirikiana naye katika jambo hili.

**SPIKA:** Ahsante. Utakaa naye; si Halmashauri yake ndiyo inabidi iandike?

Na. 76

**Ongezeko Kubwa la Wamachinga - Shinyanga**

**MHE. STEPHEN J. MASELE** aliuliza:-

Kumekuwa na ongezeko kubwa la Wamachinga Mjini Shinyanga na ni muda mrefu sasa tangu aliyezeka Waziri Mkuu Mheshimiwa Edward Lowassa alipoahidi kuipatia Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga fedha za kujenga soko jipya la kisasa:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kutekeleza ahadi hiyo iliyotolewa na Kiongozi wa juu kabisa?

(b) Serikali haioni kuwa huu ni wakati muafaka wa kutenga fedha katika bajeti ya mwaka huu ili ujenzi huo uanze mara moja na kutatua kero ya soko kwa Wamachinga hao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Julius Masele, Mbunge wa Shinyanga Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza ahadi iliyotolewa na Serikali, Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, iliandika andiko la ujenzi wa soko na kuliwasilisha kwa Wadau mbalimbali. Aidha, Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*) na Shirika la Hifadhi ya Jamii (*NSSF*), wameonesha nia ya kuwekeza katika Mradi huo kwa kuingia ubia na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Mwekezaji Binafsi wa Bariadi, amewasilisha rasimu ya ujenzi wa soko hilo kwa gharama ya shilingi milioni 300 akitaka kuweka hisa ya asilimia 70 *SUSSCO Company Limited*, Halmashauri asilimia 20 na asilimia 10 kwa Wafanyabiashara. Halmashauri ile imetenga eneo litakalojengwa soko hilo ambapo litakuwa karibu na Soko la Nguzo Nane. Aidha, imeundwa Kamati Ndogo ya kufutilia kuratibu ujenzi wa soko hilo.

(b) Mheshimiwa Spika, kutohana na ukomo wa bajeti unaotolewa, imekuwa siyo rahisi kwa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga kuingiza katika bajeti suala la ujenzi wa soko jipya la kisasa katika Manispaa ya Shinyanga. Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, inaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ili kusaidia ujenzi wa soko la kisasa. Aidha, Halmashauri imeandaa maombi maalum na kuyawasilisha Serikalini ili kutekeleza azma ya kujenga soko hilo.

**MHE. STEPHEN J. MASELE:** Mheshimiwa Spika ahsante kwa majibu mazuri ya Waziri.

(i) Manispaa ya Shinyanga kwa sasa imekuwa na ongezeko kubwa la wafanyabiashara wadogowadogo wakiwemo Akina Mama na wamachinga na Sheria za

Mipango Miji zimekuwa zikitekelezwa vizuri kiasi kwamba akina mama na Wamachinga wananyang'anywa na kuporwa vitu vyao ambavyo mitaji yake wamekopa kwenye *Financial Institutions* mbalimbali. Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kuingilia na ku-speed up process ambayo Manispaa imeshaanzisha ya kujenga soko hilo kuitia Wadau mbalimbali?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa ajili ya *records*, ninazungumzia Akina Mama pamoja na Wafanyabiashara wadogowadogo.

Mheshimiwa Spika, *it is our judgement* kama Serikali kwamba, Mbunge huyu anayezungumza hapa hivi sasa amefanya kazi kubwa sana katika kufuatilia suala hili linalozungumzwa. Ninataka niwaambie Wabunge wenzangu na Mheshimiwa Spika kwamba, amejitahidi kulisukuma jambo hili kwa nguvu zake zote. Ninataka nieleze hapa maana mimi ninaweka mambo katika *perspective* inayotakiwa. Kila wakati amekuwa anakuja ofisini kwa ajili ya kufuatilia jambo hili.

Mheshimiwa Spika, jambo hili likuwa ni ahadi ya Serikali na tuseme ukweli uliotokea ni kwamba, *by the time* maombi yale yanaletwa hapa, bajeti ilikuwa imekwishapita. Kwa hiyo, wakaambiwa waandike, wangeambiwa waweke katika bajeti, isingwezekana kwa sababu Bunge lilishapitisha bajeti ile. Kwa hiyo, wameleta sasa kama maombi maalum kwa sababu wakiingiza katika bajeti hii ina-bust, kuna kitu kinachoitwa *sealing* hapa; sisi tunafahamu kwa hiyo inashindikana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Masele tumepokea yale maandishi na ninataka nithibishe kwamba, tutashirikiana na Mbunge huyu, kuona tufanye nini ili Halmashauri hiyo iweze kupata soko hilo kama anavyozungumza ili Akina Mama pamoja na Wafanyabiashara wadogowadogo waweze kunufaika na mpango huo.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Kwa kuwa Wamachinga wanaonekana kama ni kero kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wanabughudhiwa kila mahali katika Miji ya Arusha, Dar es Salaam ...

**SPIKA:** Mheshimiwa Lema, rudi kule kwa sababu hiyo siyo nafasi, unapita kati ya anayezungumza na Spika

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wamachinga wanaonekana kuwa kero kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na kwa kuwa kumekuwepo na migogoro mingi inayowagusa Wamachinga katika Miji mbalimbali kama vile Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na hata Mpanda; je, Serikali itakuwa tayari kutoa tamko la kuzuia kuwabugudhi Wamachinga mpaka hapo Serikali itakapokuwa imejipanga na kuwatengenezea mipango madhubuti ili wafanye kazi zao vizuri?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninataka

nihilafiane na mwuliza swal; Serikali ya CCM haina ugomvi na Wamachinga wala haiwahesabu kuwa ni kero kama alivyosema yeye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua tatizo la vijana wetu au wafanyabiashara wadogowadogo, Serikali ya Tanzania pale ilipowezekana, imetenga maeneo ya kufanya biashara kwa wafanyabiashara wadogowadogo. Dar es Salaam; Halmashauri ya Manispaa ya Ilala, tumejenga *Machinga Complex*, ambayo lengo lake ni kupata mahali pa kufanya biashara kwa wafanyabiashara wadogowadogo. Ukienda Mwanza na sehemu mbalimbali ni hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema, nchi hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria; ni lazima ufanye biashara mahali ambapo panaruhusiwa kufanya biashara. Pamoja na kuwapenda Wamachinga, huwezi kuwaruhusu wakaenda kufanya biashara hospitalini au barabarani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninataka kusema kwamba, ninakubali kabisa kwamba, Serikali yetu inatambua kwamba, tunalo tatizo kubwa la ajira kwa vijana wetu na tunaahidi tumeanza kushughulika na tatizo la wale wanaojajiri wenyewe kwa kufanya biashara na tutaendelea kufanya hivyo kadiri ya mipango ya fedha inavyoruhusu katika Halmashauri zetu.

Na. 77

### **Vituo vya Kisasa kwa Magonjwa ya Sukari, Saratani na Shinikizo la Damu**

**MHE. HAMAD ALI HAMAD** aliuliza:-

Kumekuwepo na ongezeko kubwa la Maradhi ya Sukari, Saratani na Shinikizo la Damu hapa Nchini:-

Je, kutokana na hali hiyo, Serikali iko tayari kujenga Vituo vya Afya vya Kisasa vyenye hadhi na sifa za kukidhi mahitaji ya tiba ya magonjwa yaliyotajwa angalau kimoja kwa kila Tarafa?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swal la Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mbunge wa Magogoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tiba ya Magonjwa ya Sukari, Saratani na Shinikizo la Damu, inatakiwa kutolewa na mtaalam aliyehitimu mafunzo yanayohusiana na magonjwa hayo katika ngazi ya ubingwa kwa kutumia miongozo iliyowekwa na Nchi au Taasisi za Kitaalamu za Kimataifa. Hii ni kwa sababu kama utambuzi na tiba kwa magonjwa hayo

haitafanyika inavyotakiwa, ni rahisin kwa mfanon Ugonjwa wa Saratani kusambaa mwilini na kumfanya mgonjwa kupoteza maisha au kupata madhara mengine. Hata hivyo, Magonjwa ya Sukari na Shinikizo la Damu yanaweza kutibiwa na Madaktari wasio mabingwa waliopo katika Hospitali au Vituo vya Afya, kulingana na uwezo wao na vifaa vilivyopo. Kwa mujibu wa Mwongozo wa Utoaji wa Huduma za Tiba, Vituo vya Afya na Zahanati zinatakiwa kuwa na uwezo wa kutambua dalili za magonjwa hayo na kutoa rufaa kwenye ngazi za huduma zinazohusika.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MAAM), Serikali itajenga Kituo cha Afya katika kila Kata na Zahanati katika kila Kijiji. Vituo hivyo vitapatiwa Watumishi ambao watakuwa wamepitia mafunzo ya kutambua magonjwa hayo na kutoa rufaa kwa wagonjwa ambao hawawezi kutibiwa katika Zahanati au Kituo cha Afya. Aidha, Vituo vya Afya vinaweza kuendelea kuwashudumia wagonjwa wa sukari, shinikizo la damu na saratani, kwa kuzingatia maelekezo ya tiba kama ambavyo yatakuwa yametolewa na Madaktari au Madaktari Bingwa. Aidha, mpango wa Serikali wa kuzipandisha hadhi hospitali zote za Mikoa na kuwa Hospitali za Rufaa za Mikoa, utaharakisha upatikanaji wa huduma za kibingwa katika Mikoa, ikiwa ni pamoja na kurahisisha huduma za mkoba za mabingwa (*Outreach Services*), kwa kila Wilaya.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ninaomba kumwuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Je, Wizara imefanya utafiti kwa kiasi gani ili kujua chanzo na sababu ya kuongezeka kwa magonjwa niliyoyataja?

(b) Kwa kuwa Watanzania walio wengi ni maskini sana na kwa kuwa Mtanzania mpaka anathibitisha kwamba ameathirika na magonjwa hayo anakuwa yuko hoi bin taaban yeye na familia yake kifedha; je, kwa mapenzi kabisa kwa Wananchi; Serikali iko tayari kutoa matibabu bure kwa Watanzania ambao watathibitishwa kwamba wameathirika na magonjwa haya? (*Makofii*)

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, kama ifuatavyo:-

Kuhusu swali (a); tafiti mbalimbali zimefanyika hapa nchini na zimedhihirisha wazi kwamba, haya magonjwa yanaongezeka na sababu kubwa ambazo zimeonesha kuongezeka kwa matatizo haya ni *style* ya maisha ya Watanzania; namna gani tunaishi na tunakula nini. Mojawapo ya visababisho vya magonjwa haya ni chakula tunachokula na uwiano wake, ambao unasababisha wengi kuwa na uzito. Vilevile *style* tunazoishi; watu wengi hatufanyi mazoezi kiasi kwamba, chakula tunachokitumia hakitumiki chote na hiyo ziada ndiyo inakuja kusababisha madhara hayo.

Mheshimiwa Spika, vilevile tumekuwa na tabia ya kutumia vilevi, tumekuwa na tabia ya uvutaji sigara; hivyo navyo vinachangia kwa kasi kikubwa kuongezeka kwa

maradhi hayo. Hivi sasa kuongezeka kwa tatizo la UKIMWI nako kunachangiwa kwa kiasi kikubwa sana na tatizo la maradhi haya ambayo Mheshimiwa Hamad ameyaeleza.

Vilevile ninaomba nitoe taarifa kuwa, Wizara tayari imeshajipanga kwamba, wale wanaopatikana na matatizo ya magonjwa ya saratani, matababu yake ni bure, hawapaswi kulipa malipo yoyote. Ninaomba taarifa hii Waheshimiwa Wabunge waipate waisambaze kwa Wananchi; matibabu ya saratani ni bure na matibabu ya kisukari na moyo, tunaangalia namna gani tunaweza kusaidia; lakini sasa hivi bado hatujaanza kuyatibu matibabu haya bure japokuwa kuna taasisi mbalimbali zinazotoa msaada kwa matibabu haya.

**SPIKA:** Lakini dawa za saratani siyo bure Mheshimiwa Waziri?

**MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo la kansa limekuwa ni kubwa na linazidi kuua mwaka hadi mwaka; na kwa vile hospitali tuliyokuwa nayo imeshindwa kukidhi haja kwa kuwa wagonjwa wengi wanapelekwa Ocean Road; na kwa kuwa Serikali ilikuwa na mpango wa kupeleka huduma hii hadi Bugando na KCMC; je, Serikali imefikia wapi katika hatua zake za kupeleka huduma hiyo ili kukidhi haja katika maeneo hayo na kuwapunguzia usumbufu wa kuja Dar es Salaam? (*Makofî*)

**SPIKA:** Waziri, majibu pamoja na kununua dawa za saratani.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, tumeshaanza kutoa huduma za matibabu za magonjwa ya saratani nje ya Hospitali ya Ocean Road. Tayari Hospitali ya Bugando na Hospitali ya KCMC, wameanza kutibu magonjwa hayo kama alivyolekeza Mheshimiwa Mbunge.

**SPIKA:** Habari ya kununua za saratani? (*Kicheko*)

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunikumbusha suala la kununua dawa za saratani. Ninaomba nitoe taarifa kwamba, wagonjwa hawapaswi kununua dawa hizo, lakini kwa sababu ya upungufu wa bajeti ambao unatukabili, wakati mwingine tunashindwa kukidhi mahitaji ya wagonjwa hao; hivyo basi, tunaomba wakati mwingine wagonjwa watusaidie kutoa huduma hiyo. Licha ya hivyo, Serikali imejipanga katika kipindi cha Bajeti inayofuata, angalau kuongeza bajeti kwa ajili ya kununua dawa hizo za saratani.

Na. 78

#### **Elimu Juu ya Matumizi ya ARVs kwa Waathirika wa UKIMWI**

**MHE. MARYAM S. MSABAHA** aliuliza:-

Waathirika wengi wa VVU wa vijijini hawana elimu ya kutosha kuhusu matumizi ya ARVs na wengi wao hawapati lishe bora:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha misaada ya wafadhili inawafikia walengwa?

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba elimu inayoendelea kutolewa kupidia vyombo vyahabari na taasisi mbalimbali inawafikia watu walioko vijijini kuwanusuru waathirika?

#### **WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali hupokea misaada kwa ajili ya mapambano dhidi ya UKIMWI kutoka kwa wahisani mbalimbali. Baadhi yao ni Mfuko wa Dunia wa Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria (*Global Fund*), Mpango wa Mfuko wa Dharura wa Rais wa Marekani wa Kupambana na UKIMWI (*PEPFAR*), ambao hutoa misaada mbalimbali ikiwemo ya kifedha katika ngazi ya Taifa inayolenga kupanua huduma za Kinga, Tiba na Matunzo kwa wanaoishi na VVU. Matumizi ya fedha za wahisani yanajonesha kwa kupanuka kwa huduma hizo nchini. Hadi kufikia Juni 2010, jumla ya watu 8,590,209 walikuwa wamepatiwa huduma ya ushauri nasaha na upimaji wa VVU. Aidha, hadi kufikia Septemba, 2010 watu 701,242 walikuwa wameandikishwa katika mpango wa huduma za tiba. Kati ya hao, watu 361,262 walikuwa wakipatiwa dawa za kupunguza makali ya VVU.

(b) Mheshimiwa Spika, ninaomba nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba, elimu ya matumizi ya ARVs bado haijawafikia waathirika wengi wa VVU hususan katika maeneo ya vijijini. Hata hivyo, ninaomba kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, hutoa mafunzo kwa watoa huduma za tiba na matunzo katika vituo vyote vilivyopo mijini na vijijini, vinavyotoa huduma hizo. Watalaam hao hutoa ushauri wa kitaalam kwa watu wanaotumia dawa za kupunguza makali ya VVU kuhusu masuala mbalimbali ya kiafya, ikiwa ni pamoja matumizi sahihi ya ARVs. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa na Wahisani mbalimbali katika mapambano dhidi ya UKIMWI nchini, inaendelea kutoa elimu ya upatikanaji na matumizi sahihi ya ARVs kwa njia ya Redio, TV, Machapitisho na Mikutano.

**MHE. MARYAM S. MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Watanzania wengi wamekuwa na mila potofu wengine wamekuwa wakitumia dawa za kuongeza umri wamekuwa wengi hasa wa vijijini wamekuwa wanakimbilia kwenye Kikombe cha Babu. Je, Waziri ananihakikishiaje kuwa Dawa ya Babu inatibu Ugonjwa wa UKIMWI moja kwa moja?

**SPIKA:** Wewe unaulizwa maswali ya Babu?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, Kikombe cha Babu kama kinavyojulikana Babu wa Loliondo, hadi sasa bado tunakifanyia utafiti ili kutoa jibu kwamba kile Kikombe kimoja cha Babu kinatibu magonjwa yale matano ambayo Babu amedai anatibu. Taarifa tulizozitoa mwanzo kwa Watanzania, tulijibu swal la kwamba, dawa ile ni salama kwa matumizi ya afya ya binadamu na haina sumu. Tumewaambia Wananchi kwamba, kwa kile Kikombe cha Babu, anachokitoa ambacho anachemsha kilo tatu za ule mzizi ndani ya maji yali lita 60, bado imedhihirisha ni salama haina madhara. (*Makofi*)

Hivyo basi, tunaomba Wabunge mpeleke taarifa kwa Wananchi kwamba, wavute subira, tunaendelea na utafiti ambao tunahusisha na wagonjwa pia ambao tayari wamepata Kikombe cha Babu ili tutoe jibu kama kile Kikombe kinatibu yale magonjwa matano. Ninashukuru.

**SPIKA:** Ukishauliza Babu hakuna kuuliza maswali mengine. (*Kicheko*)

Na. 79

### **Ajira kwa Vijana**

**MHE. NAOMI M. KAIHULA** aliuliza:-

Liko ongezeko la kutisha la vijana wanaomaliza shule katika viwango mbalimbali na kujiunga na jamii ya watu wazima, wakiwa hawana ajira:-

(a) Je, Serikali ina mipango gani madhubuti ya kuwawezesha vijana hao kujitegemea?

(b) Je, nini uwiano wa ajira na wanaomaliza shule na vyuo katika kipindi cha miaka mitano iliyopita?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swal la Mheshimiwa Naomi Kaihula, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Ili kuwawezesha vijana kujitegemea, Serikali imeweka mazingira wezeshi na sera mbalimbali zikiwemo Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007), Sera ya Taifa ya Ajira (2008) na Sera ya Elimu na Mafunzo (1995). Aidha, juhudhi mbalimbali zimekuwa zikifanyika ikiwa ni pamoja na:-

- Kuhamasisha vijana kujiunga katika vikundi vya kiuchumi na Vyama vya Kuweka Akiba na Kukopa (SACCOSS) na kuwawezesha kujipatia mitaji ya kuanzisha na kuendeleza miradi ya kujajiri.

- Uwekezaji mkubwa katika Sekta ya Elimu na Ufundu Stadi ukienda sambamba na uboreshaji wa mitaala ili vijana wanaohitimu waweze kuwa na ujuzi wa kuwawezesha kujajiri na kujitegemea.
- Kupanua huduma za ajira kwa kuanzisha wakala wa huduma za ajira (*TAESA*), unaohusika na kuwaunganisha vijana watafuta kazi na waajiri na kutoa mafunzo na ushauri kwa watafuta kazi.
- Kutoa fursa kwa sekta binafsi kutoa huduma za ajira kupitia wakala binafsi wa huduma za ajira ili kuwafikia vijana wengi zaidi.
- Kuimarisha taasisi za mafunzo ya stadi kama *VETA*, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na Vituo vya Vijana ili viweze kutoa mafunzo kwa vijana hasa wa vijijini.
- Kuhimiza uwekezaji katika sekta za uzalishaji na biashara zenyenye kutoa ajira nyingi kama kilimo, ufugaji, uvuvi, viwanda, ujenzi, usafirishaji, mawasiliano na biashara.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa sasa ni vigumu kupata taarifa za uwiano wa vijana wanaomaliza shule na vyuo na wanaopata ajira kutokana na kukosekana mfumo wa utuutiliaji (*Trace Study*) kamili fu, ambao ungetuwezesha kufahamu ni vijana wangapi kati ya waliomaliza shule au vyuo wameweza kuajiriwa. Kutokana na upungufu huo, Wizara yangu inaandaa mfumo wa upatikanaji wa taarifa za soko la ajira, ambapo utakapoanza kufanya kazi mwishoni mwa mwaka huu tutakuwa tunapata taarifa hizo.

Hata hivyo, kwa mujibu wa matokeo ya utafiti wa Nguvu Kazi wa Mwaka 2006, kwa ujumla kila mwaka vijana kati ya 800,000 na 1,000,000 huingia kwenye soko la ajira kama nguvu kazi. Utafiti huo wa mwaka 2006 ulionesha kwamba, asilimia 88.3 ya nguvu kazi inayoingia kwenye soko la ajira, hupata ajira na asilimia 11.7 hawapati ajira kabisa. Aidha, utafiti huo ulionesha kuwa, kati ya nguvu kazi iliyoajiriwa Sekta ya Kilimo iliongoza kwa kuajiri asilimia 74.6. Hata hivyo, takwimu hizi ni kwa mujibu wa utafiti wa miaka mitano iliyopita. Kwa sasa hali inaweza kuwa tofauti.

**MHE. NAOMI M. KAIHULA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini amenijibu robo kwa sababu swali langu lilitaka kuonesha jinsi Serikali inavyowawezesha vijana kujitegemea. Hata hivyo, ningependa kuuliza swali kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Waziri amekiri kwamba hawana mfumo mahususi wa kuweza kufuutilia vijana kama ni wangapi wanaajiri na wangapi wanamaliza vyuo, nilikuwa na swali hili: Kwa kuwa wakati Mheshimiwa Rais alipokuwa katika Wizara mbalimbali kuna jambo lilijitokeza linalohusu mabilioni ya JK kwamba hayakutolewa ipasavyo kutokana na kwamba hakukuwa na takwimu nzuri za urejeshaji na utoaji; je, Mheshimiwa Waziri, anaweza kutuambia kwamba inawezekana wakafanya tathmini ili

kuweza kutupa njia gani watatumia kulitatu suala hili kwa sababu ni aibu sana kukiri kwamba hakuna mfumo wa ufuatiliaji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naoni Kaihula, umeuliza maswali mawili, la kwanza umesema unashangaa kwa nini takwimu hazipo, la pili ni ajira.

**MHE. NAOMI M. KAIHULA:** Mheshimiwa Spika, la kwanza ni ufuatiliaji la pili ni ajira, aliposema kwamba mpaka sasa ajira 88.3 zimekwishatolewa. Katika hali halisi, unafahamu hata wewe na Wabunge wetu wanafahamu kwamba, suala ala ajira ni tatizo kubwa mno, ukiniambia 88 ndiyo wamekwishapata basi hakuna kusema kweli kuna tatizo la ajira.

Swali langu ni hili; ninaomba Mheshiwa Waziri atufafanulie je, anaweza kutupa ufanuzi wa aina za ajira hizo walizotoa kwa watu 88 na hao 11.7 waliobaki wako maeneo gani na kwamba anafikiri ni kitu gani kinawasababisha wasiweze kuajiri. Ahsante.

**SPIKA:** Jamani watu wanaanza kujifunza kuuliza maswali; kwa nini mnazomea!

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, alisema kwamba, sikujibu swalii la vijana wanajitegemea vipi. Hatua sita nilizozitaja mwanzoni zilikuwa ni zile ambazo zinawawezesha vijana kujitegemea. Kuhusu masuala ya ufuatiliaji wa mabilioni ya JK ni kweli alitoa agizo hilo na ni Agizo la Rais; sisi Wizara ya Kazi na Ajira, tukishirikiana na Wizara ya Uwezeshaji, tumeanza zoezi hilo la kufanya ufuatiliaji namna fedha hizi zilivyotumika na alisema katika ahadi yake atatoa tena bilioni 100 kwa ajili ya vijana kujiajiri lakini kama tutaweka mfumo mzuri na mipango mizuri na mikakati ya kuandaa vijana kujitegemea. Mimi ninasema kwa sababu ni agizo lenye motisha kwamba, tutapata bilioni 100 kwa ajili ya vijana kujiajiri tutalitekeleza kwa kuandaa mazingira hayo. (*Makofii*)

Kuhusu vijana 88, mimi nilichosema ni kwamba, katika vijana wanaoingia kwenye soko la ajira, asilimia 88.3 kwa mujibu wa utafiti wa mwaka 2006, walikuwa wanapata ajira, asilimia 11.7 hawana ajira. Sasa hivi inawezekana hali imekuwa tofauti kwa sababu hatujafanya utafiti kwa miaka mitano. Tutakapomaliza utafiti, tutawenza kujua kwa uhakika sasa asilimia ngapi inaa jiriwa na ngapi hai a jiriwi. (*Makofii*)

**SPIKA:** Tumechukua muda mrefu kwa suala hili, kwa hiyo, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Na. 80

#### **Fursa ya Kuwa na Uraia wa Nchi Mbili**

**MHE. LETICIA M. NYERERE** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa leo ni siku ya kuzaliwa Baba wa Taifa, baba yetu mpendwa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, ninaomba niungane na Watanzania wote walioko nchini na wale walioko nchi za nje, kumshukuru Mwenyezi Mungu. Sasa ninaomba swalii langu namba 80 lijibiwe. (*Makofii*)

Kumekuwa na mjadala wa muda mrefu kuhusu Watanzania kuwa na fursa ya uraia wa nchi mbili (*Dual Citizenships*) na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa aliwahi kunukuliwa akisema maandalizi yanaendelea:-

- (a) Je, maandalizi hayo yamefikia wapi?
- (b) Je, ni lini Serikali itawasilisha Bungeni marekebisho ya Sheria husika ili Taifa letu lianze kunufaika na *Dual Citizenship*?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, ninapenda kujibu swalii la Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, maandalizi ya Serikali yetu kuwaruhusu kisheria Watanzania wanaoishi nje kupata uraia wa nchi mbili (*Dual Citizenship*), yamefikia pazuri. Tumefanikiwa kuwafikia kwa wingi Watanzania walioko nje kuitia mikutano na majukwaa mbalimbali na kupata maoni yao. Tumekwishafanikiwa kuunda Idara ya *Diaspora* katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa ajili ya kuratibu masuala haya. Kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, ameunda Kitengo cha *Diaspora* kinachoongozwa na Naibu Katibu Mkuu, ambacho kipo chini ya ofisi yake na tunashirikiana nacho kwa karibu sana. Aidha, tumefikia maelewano na wadau mbalimbali ikiwemo Wizara ya Mambo ya Ndani, Taasisi za Umma kama Benki Kuu, Kituo cha Uwekezaji (*TIC*), Mamlaka ya Mapato (*TRA*), Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*), Mfuko wa Uwekezaji (*UTT*), NSSF na Wadau nje ya Serikali kama Benki za *CRDB*, *Commercial Bank of Africa (CBA)*, na Mawakala Binafsi wa Ajira (*Recruitment Agencies*).

Maelewano haya yanasadidua katika mkakati wetu wa kujenga mazingira ya kisheria na kisera ya kuwezesha *diaspora* kushiriki kikamilifu katika uchumi wa nchi yetu.

(b) Mheshimiwa Spika, hatua hiyo mbele yetu ni kwa Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Mwanasheria Mkuu kuwasilisha Waraka kwenye Baraza la Mawaziri ili ujadiliwe na kisha kwa wakati muafaka, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kutakiwa kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Uraia ili jambo hili liletwe rasmi Bungeni kwa majadiliano. Kwa kuwa mwaka huu ni mwaka wa kuitia upya Katiba na kwa kuwa suala la uraia ni suala linalogusa Katiba; ni azma yetu kuona suala hili linakwenda sambamba

na mchakato wa Katiba unaotarajiwa kuanza karibuni. Wizara imedhamiria kuona suala la uraia wa nchi mbili linazinduliwa sambamba na Katiba mpya.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri.

(i) Ninamwomba Mheshimiwa Waziri anieleze faida ambazo zinajitokeza kwa kuwa na *Dual Citizenship*?

(ii) Je, Serikali inatambua kwamba kuna faida za kuwa na uraia wa nchi mbili; na je, suala hili litachukua muda gani kukamilika? Ninaomba nitajiwe mwaka, mwezi na ikiwezekana tarehe ili niweze kufuatilia. (Makofî)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ninaomba ujibu swalî la kwanza, la pili umesema mchakato wa Katiba unaendelea.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje, ninaomba kumjibu Mheshimiwa Leticia Nyerere, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, faida za *Dual Citizenship* ziko katika makundi mawili; faida ambazo wanapata wale Wananchi ambao watakuwa na uraia; na faida ambazo zinapatikana na nchi husika. Kwa upande wa Wananchi ni kwamba, wanaweza kuendelea na kupata faida zote ambazo Wananchi walioko nchini wanaendela kuzipata. Kwa hiyo, mtu mwenye uraia wa nchi mbili anaweza kuendelea kupata fursa na haki ya kupiga kura, fursa ya kuwekeza kama Mwananchi mwingine ye yole yule ambaye hana *Dual Citizenship* na pia kuweza kuleta mitaji na fedha nchini kama Mwananchi wa kawaida.

Kwa upande wa nchi husika ni kwamba, inakuwa ni rahisi kwa wale Wananchi ambao wana uraia wa nchi mbili na wanaishi labda nje ya nchi, kuleta fedha na kuwekeza katika nchi hii na pia kuweza kupata fursa. Kwa mfano, kama mtu ana uraia wa Uingereza na ni Mtanzania, anaweza kuishi na kufanya kazi katika nchi zote za Ulaya na kwa hiyo wanaweza kupata taaluma na ufundi ambao pia wanaweza kuuleta nchini na nchi ikafaidika katika *technology transfer*. Ahsante.

Na. 81

### **Tatizo la Maji - Ubungo**

**MHE. JOHN J. MNYIKA** aliuliza:-

Wananchi wa Kata za Kwembe, Kikamba, Msigani, Mbozi, Saranga na Kimara wanaotegemea maji toka Ruvu Juu na wana matatizo makubwa ya maji:-

(a) Je, ni lini Serikali itawezesha mitambo ya Ruvu Juu kupata umeme wa uhakika ikiwemo kuweka jenereta za dharura na pampu zenye uwezo wa kusukuma maji ili Wananchi hao wapate maji ya uhakika?

(b) Serikali ina mpango gani wa kudhibiti upotevu mkubwa wa maji (*Non Revenue Water*) unaotokea kati ya Kibaha na Kimara ili kuongeza upatikanaji wa maji kwa Wananchi wengi?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha tanki lililojengwa Luguruni linatumika kuhifadhi maji ili Wananchi wa Kata hizo wapate maji kama ilivyo kwa wenzao baada ya tanki la Kimara?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa John John Mnyika, Mbunge wa Ubungo, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika kukabaliana na tatizo la umeme kwenye Mtambo wa Ruvu Juu, Serikali kuititia DAWASA, tayari imechukua hatua ya ujenzi wa njia maalumu ya umeme kutoka msongo mkubwa (*Dedicated Overhead Line*) ulioanzia Kituo cha TANESCO Mlandizi hadi kwenye chanzo cha Mtambo wa Ruvu Juu kilichopo Ruvu Darajani. Msongo huo ni wa KV 33 na una urefu wa kilomita sita. Mradi huo ulikamilika tarehe 9 Aprili 2011; hivyo, usukumaji wa maji kutoka kwenye Mitambo ya Ruvu Juu umeimarika.

(b) Mheshimiwa Spika, sababu kuu ya upotevu wa maji maeneo ya kati ya Kibaha na Kimara ni uchakavu wa mabomba makubwa yanayosafirisha maji. Tatizo hilo litamalizika baada ya kujenga bomba jipya litakaloanzia Kibaha hadi Kimara. Maombi ya kumpata Mhandisi Mshauri atakayefanya mapitio ya usanifu, kuchunguza athari za kijamii na mazingira, pamoja na kusimamia ujenzi, yamepokelewa na uchambuzi wa zabuni umeanza tarehe 28 Februari, 2011 na unaendelea. Zabuni ya kumtafuta mkandarasi itatangazwa kuanzia mwezi Agosti, 2011 baada ya Mhandisi Mshauri kutayarisha nyaraka za zabuni. Kazi ya ujenzi wa bomba jipya inatarajiwa kuanza Januari, 2012.

(c) Mheshimiwa Spika, tanki la Luguruni lilijengwa ili kurahisisha usafirishaji wa maji kati ya Mlandizi na Kimara. Tanki hilo kwa sasa halitumiki kutokana na uchakavu wa mabomba yanayotoka Kibaha kwenda Kimara. Maji yakijaa kwenye tanki hilo, husukuma maji mengi kwenye mabomba yanayoelekeea Kimara na kusababisha upotevu wa maji zaidi. Mpango uliopo ni kujenga bomba jipya kutoka Kibaha hadi Kimara ili kuimarisha usafirishaji na usambazaji wa maji katika maeneo hayo kama ilivyoolezwa katika jibu la swali (b) hapo juu.

Huduma ya maji kwa Wananchi waishio kati ya Kibaha na Mbezi Luisi, itaboreshwa kwa kujenga mfumo mpya wa usambazaji maji katika maeneo hayo kama ilivyoofanyika katika maeneo ya Kibaha hadi Mlandizi. Kazi hii imepangwa kutekelezwa kuanzia Julai 2012 ili kwenda sambamba na ongezeko la uzalishaji maji katika Mtambo

wa Ruvu Juu na ujenzi wa bomba kubwa kati ya Kibaha na Kimara; kazi zitakazoanza Juanuari, 2012.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa kwenye jibu lake la msingi Naibu Waziri amesema sababu ya upotetu wa maji ni masuala ya miundombini; na kwa kuwa *DAWASCO* walishapewa maelekezo na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali toka mwaka 2007 walishughulikie lakini mpaka sasa halijashughulikiwa na kiwango cha maji kuwa nusu ya maji yanayozalishwa; na kwa kuwa pamoja na uwekaji wa mabomba maarufu kama Mabomba ya Wachina kwenye maeneo ya Stop Over, King'on'go na mengineyo bado maji hayatoki; na kwa kuwa Shirika hili sasa lina hasara ya shilingi bilioni 12.6; je, Serikali iko tayari kufanya ukaguzi wa kifedha na kiufanisi kwa Shirika la *DAWASCO* kutokana na hali tete ya Shirika ilivyo hivi sasa kiutendaji na hivyo kuathiri Wananchi kuhusiana na upatikanaji wa maji?

(b) Kwa kuwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri yote yameonesha hatua ambazo zitachukuliwa na zitakamilika mwishoni mwa mwaka 2012 au mwanzoni mwa mwaka 2013; na kwa kuwa zipo hatua nyingine za dharura ambazo zinaweza kusaidia kupunguza ukubwa wa tatizo mathalani utekelezaji wa ahadi ya Rais ya tarehe 24 Oktoba, 2010 ya ujenzi wa visima Bonyokwa na ujenzi wa visima kumi chini ya Mradi ya Benki ya Dunia Msaguzi, Mpege magoye na kwingine: na kwa kuwa Makao Makuu ya Wizara yako ndani ya Jimbo la Ubungo; je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kusimamia kwa dharura utekelezaji wa ahadi hizi ili kupunguza kero kwa Wananchi?

## **TAARIFA YA SPIKA**

**MHE. ESTER A.BULAYA:** Mheshimiwa Spika, ninataka kutoa ufanuzi; Mheshimiwa Mbunge aliyetoka kuuliza swali lake sidhani kama *figure* yake ni sahihi; *DAWASA* wamepata hasara bilioni 26 katika tatizo zima la upotetu wa maji; bilioni 12 ni hasara kwa ajili ya ukusanyaji mapato na si tatizo la upotetu wa maji.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, naikata taarifa kwa sababu kwa takwimu nilizonazo, kuna hasara za aina mbili; *DAWASCO* bilioni 12.6 pamoja na bilioni 26.8, ambayo ni kwa sababu ya tofauti kati ya mtaji wa *DAWASCO* pamoja na maji.

**SPIKA:** Hiki ni kipindi cha maswali tunaendelea. Ninyi nyote hamjasema kitu, Naibu Waziri hebu sema sasa. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa John Mnyika, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Tatizo la upotetu wa maji ambalo limeainishwa kwenye ukaguzi, sehemu kubwa ni kwamba, mtambo wa kutoa maji Ruvu kuja Dar es Salaam; kwanza, ulijengwa mwaka 1959. Miradi mingi ya maji muda wake ni miaka 20, kwa hiyo, imepitwa na muda. Sasa

kwa vyovyote vile, upotevu wa maji unatokana na uchakavu wa mabomba, lakini sehemu nyingine ni watu wanaofanya *connection* kinyume na sheria. Kwa hiyo, ina maana yale maji hayalipiwi. Kwa hiyo, hasara ile inatokana na kwamba, watu hawalipi yale maji na pia uchakavu wa yale mabomba.

Mheshimiwa Spika, mpango uliopo hivi sasa ni kufufua mpango mzima; Serikali imesharidhia mpango mkubwa wa maji Dar es Salaam, ifikapo Desemba 2012. Mpango huu utakuwa na maji ya kutosha maeneo yote kwa asilimia 75. Maeneo yote ya Dar es Salaam mpaka Mlandizi na Watu wa Ubungo, watapata maji kwa asilimia 75. Kwa hiyo, matatizo yote haya yatakwisha.

Suala la upotevu na suala la kuhakikisha Wananchi wanapata maji litaisha Desemba 2012; hiyo ndiyo ahadi ya Serikali.

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ya swali haijajibiwa.

**SPIKA:** Anasema hatua za dharura.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, mpango ambao nimeusema wa Desemba 2012 ni wa dharara. Tuna visima 20 Kimbiji na Mpera, ambavyo tunatarajia kuanza kuchimbwa kuanzia mwezi Mei, 2010 pamoja na visima ambavyo viro. Kwa hiyo, hii ni mipango yote ambayo inakwenda sambamba kuhakikisha Wananchi wa Dar es Salaam wanapata maji.

Na. 82

### **Huduma ya Maji Toka Bwawa la Manchira**

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE** aliuliza:-

Serikali imekamilisha uchimbaji wa Bwawa la Manchira kwa ajili ya maji Mugumu Mjini na tayari vioski vya maji vimeshaanzishwa:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwapa maji ya kutosha Wananchi wa Tarafa ya Rogoro pamoja na Vijiji jirani vya Kibeyo, Kisangura, Ngarawani, Kogonga, Sedeco na Vijiji vya Kata ya Choramichanga ambako bwawa limejengwa lakini vijiji vya Miseke, Manchira na Bwitangi havina maji kabiza?

(b) Je, mfumo wa kusafirisha maji ya Bwawa hilo kwenda sehemu zilizokusudiwa utajengwa lini?

(c) Je, mtandao wa mabomba na kuongeza vioski vya maji Mjini Mugumu utajengwa lini ili kuboresha huduma ya maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Kebwe Stephen Kebwe, Mbunge wa Serengeti, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imetekeleza Mradi wa Maji Mjini Mugumu kutoka katika chanzo cha Bwawa la Manchira na kuzinduliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mwezi Julai, 2010. Mradi huo umeongeza upatikanaji wa maji katika Mji wa Mugumu kutoka mita za ujazo 90 mpaka mita za ujazo 760 kwa siku, sawa na asilimia 70 ya mahitaji kwa sasa. Mradi huu uligarimu shilingi bilioni 11.02. Serikali pia inatambua umuhimu wa Wananchi wa vijiji vya jirani kupata maji ya kutosha. Katika kutekeleza suala hili, Serikali imeajiri Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kufanya usanifu na uandaaji wa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya Mradi wa Majisafi na Majitaka Mjini Musoma na Mradi wa Majisafi katika Miji ya Mugumu, Tarime, Bunda na Mradi wa Kitaifa Mugango Kiabakari. Usanifu huu pia unahu su Tarafa ya Rogoro na Vijiji vya Mikese, Manchira na Bwitangi, ambavyo ni sehemu ya Mji wa Mugumu na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Aprili, 2011.

(b) Mheshimiwa Spika, baada ya usanifu kukamilika, gharama za ujenzi wa Mradi zitafahamika na ujenzi utatekelezwa katika Awamu ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (*WSDP*), itakayoanza mwezi Julai, 2012. Taarifa ya awali ya usanifu inaonesha kuwa, chanzo cha Bwawa la Manchira kinatosheleza mahitaji ya maji kwa Mji wote wa Mugumu.

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika kipengele (b), baada ya usanifu kukamilika, kazi ya kuongeza mtandao wa mabomba na ujenzi wa vioski vya maji Mjini Mugumu itafanyika.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Tunajua kwamba mitambo inavyotumika huwa kuna kuchakaa na suala zima la ukarafati wa mitambo. Je, kuna utaratibu gani wa kupata *standby pump* katika Bwawa hili ili pale ambapo kutakuwa na ukarafati au uharibifu Wananchi wasikose maji katika Mji wa Mugumu?

(b) Je, Wizara ya Maji pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii wana mpango gani kudhibiti wanyama ambao wanatoka hifadhini kuingia katika bwawa hili hususan viboko ambao tunajua asili yao sehemu kubwa wanaishi majini ambao wameanza kuvamia katika bwawa hili?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Kwanza, kuhusu suala la kuwa na *standby pump* hii inatokana na fedha zilizopo kwa sababu kama unazo fedha za kutosha, lazima uwe na *standby pump* ili ikiaribika nyingine iweze kufanya kazi. Kwa sasa tutaangalia hali ilivyo, kama uwezo wa fedha utaruhusu, tutaweka *standby pump*, lakini kwa sasa ninaona hakuna tatizo la *pump* iliyopo.

Mheshimiwa Spika, katika suala la kudhibiti wanyama, ninaomba niseme kwamba, hili si suala la Serikali peke yake, ni suala ambalo itabidi tusaidiane Wananchi na Halmashauri kwamba, maji yale wanyama watumie kiasi gani na pia binadamu watumie kiasi gani.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ninaomba niongeze majibu. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, ninaomba nijibu swali la pili la nyongeza la Mheshimiwa Kebwe Stephen Kebwe, Mbunge wa Serengeti, kwamba; ni kweli Wizara yangu imebaini tatizo la wanyama kutoka hifadhini kwa sababu mbalimbali, hasa kwa sababu ya kutafuta maji na kuna maeneo mengi ambayo wanyama wamekuwa wakifikia hata hatua ya kufa kutokana na ukosefu wa maji hifadhini. Nimekwishakuagiza wanaosimamia Sekta ya Wanyamapor, Idara ya Wanyamapor, pamoja na Shirika la Hifadhi la Taifa (*TANAPA*), kuanza mpango wa utafiti wa mpango wa maji ya ndani ya hifadhi na ikiwezekana, sehemu ambazo zinaweza zikawa na maji ya kutosha, waweze kuchimba mabwawa. Ninaamini utaratibu huu unaweza kupunguza tatizo hili. Ninashukuru.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa tatizo la maji lililopo Wilaya ya Serengeti linafanana kabisa na tatizo la maji ambalo wanakabiriwa nalo Wananchi wa Wilaya ya Bunda na Mkoa wa Mara kwa ujumla; je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kujenga Mradi mkubwa wa Maji kama ule wa Shinyanga ili Wananchi wanaoshi Mikoa ya Kanda ya Ziwa na Wananchi wa Mkoa wa Mara na Wilaya ya Bunda wawe na uhakika wa kupata maji safi na salama?

**SPIKA:** Mzee wa Bunda amenyamaza anakusikiliza tu. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, ninaomba nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kuhusu upatikanaji wa maji ya uhakika katika Wilaya ya Bunda, kama ifuatavyo:-

Kwa hivi sasa, tuna Mradi mkubwa wa kufufua miundombinu ya upatikanaji wa maji katika eneo la Musoma na Bunda. Kwa hiyo, tunaye Mhandisi Mshauri ambaye anafanya utafiti wa kuweza kukarabati miundombinu iliyoko sasa pamoja na kushauri namna ya kuboresha. Kwa hiyo, utafiti huo utakapokamilika, tutaona ni namna gani tutaongeza upatikanaji wa maji katika Mji wa Bunda.

Na. 83

### **Bei ya Tumbaku**

**MHE. SHAFFIN A. SUMAR** aliuliza:-

Asilimia kubwa ya Wakazi wa Mkoa wa Tabora ni wakulima wa tumbaku na ingawa wanakopeshwa mbolea na Serikali ili wazidishe kilimo lakini hawana uhakika na bei ya kuuzia tumbaku hiyo:-

Je, Serikali inaweza kutafuta bei ya zao la tumbaku kwa sasa na kutoa mwongozo wa bei hizo kwa wakulima ili wajipange vizuri wasije kupata hasara na kushindwa kulipa deni la pembejeo na kuwa sababu ya kuviua Vyama vya Ushirika?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swalii la Mheshimiwa Shaffin Sumar, Mbunge wa Tabora Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, bei za tumbaku kwa mkulima hujadiliwa na kuamuliwa na Halmashauri ya Tumbaku Tanzania (*Tanzania Tobacco Council*), ambayo ni chombo cha kisheria kwa mujibu wa Sheria ya Tumbaku Na. 24 ya Mwaka 2001. Halmashauri ya Tumbaku Tanzania, huwakutanisha wawakilishi wa wakulima kupitia ushirika wao na wawakilishi wa makampuni yanayonunua tumbaku nchini, ambayo ni *Tanzania Leaf Tobacco Company (TLTC)*, *Alliance One Tobacco Tanzania Ltd (AOTTL)* na *Premium Active Tanzania Ltd (PATL)*. Majadiliano hayo hupanga bei kwa mkulima katika msimu unaohusika. Aidha, majadiliano hayo huzingatia gharama za uzalishaji, mwenendo wa Soko la Dunia wa zao la tumbaku, mahitaji ya tumbaku katika soko pamoja na masilio ya kimataifa ya zao hilo kutoka msimu uliopita. Bei ya Soko la Kimataifa ikiwa nzuri, utaratibu huo humhakikishia mkulima bei nzuri, lakini bei ya dunia ikishuka na bei ya mkulima pia inaathirika. Kwa mfano, katika msimu wa 2009/2010, bei ya tumbaku ilikuwa nzuri kiasi cha kuwahamasisha wakulima kuongeza uzalishaji msimu huu. Ili kulinda maslahi ya wakulima wa tumbaku, Serikali inaendelea kufanya mazungumzo na wadau wote, yakiwemo makampuni yanayonunua tumbaku pamoja na kutafuta masoko mapya kwa lengo la kupata bei mwafaka kwa tumbaku yetu.

**MHE. SHAFFIN A. SUMAR:** Ninashukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya ziada. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ninaomba niulize kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa Wananchi wa Tabora wana bidii sana na wanalima sana tumbaku kiasi kwamba wanazalisha tumbaku kupita malengo ya mnunuzi. Je, tunaweza kufahamishwa ni lini bei ya tumbaku itajulikana kwa msingi huu ili wakulima wajue hatima ya kilimo chao?

(ii) Je, Serikali ina mpango gani wa kutupatia kiwanda cha tumbaku sisi Mkoani Tabora?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kama alivyosema, zao la tumbaku kwa kweli linaendelea kutupa shida kidogo kutokana na tumbaku nyingi ambayo ipo na haijanunuliwa. Hivi sasa tunafanya mazungumzo na wanunuzi na kama mnavyojua, wanunuzi ni wachache, wapo watatu tu. Kwa hiyo ni rahisi kwao kutuyumbisha katika kuamua bei ipi. Kwa hiyo, Serikali sasa inafanya mazungumzo na wadau wote ikiwa ni pamoja na Wawakilishi wa Wakulima, Bodi ya Tumbaku na *APEX* ya Tumbaku na tuna hakika kabisa kwamba, mpaka kufika mwisho wa mwezi huu, tutakuwa tumepata muafaka wa bei ipi itumike.

Nilipojibu swalii la Mheshimiwa Sakaya, nilisema pamoja na hayo, tunajitahidi kutafuta masoko mapya na kwa hiyo, Wizara ya Biashara na Masoko sasa hivi imetuma wawakilishi au ujumbe katika nchi ya Irani ili tuweze kupata wanunuzi wengine kupunguza haya matatizo ya bei ya tumbaku. Kuhusu kiwanda, suala la viwanda ninadhani ni suala zuri, lakini ni vizuri likafuata utaratibu maana uwekezaji wa viwanda, Sekta Binafsi inaweka viwanda na Serikali inaweka viwanda. Kwa hiyo, ninalipokea ni wazo zuri. Ninadhani tulifanyie utaratibu ili mchakato uweze kuendelea wa kuwahamasisha wawekezaji katika sekta hii ya tumbaku.

Na. 84

#### **Kusaidia Wakulima wa Vitunguu Swaumu Katika Kijiji cha Bashay Wilayani Mbulu**

**MHE. MARTHA J. UMBULLA** aliuliza:-

Pamoja na umuhimu wa zao la vitunguu swaumu ndani na nje ya nchi ya Tanzania kama chakula na dawa, zao hili huzalishwa kwa zana duni hasa katika Kijiji cha Bashay Wilayani Mbulu:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha kilimo cha zao hilo kiendane na umuhimu wake?

(b) Je, Serikali itawasaidiaje wakulima wa zao hilo walioko Bashay wanaolima kwa miaka mingi bila tija?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mikakati ya Serikali katika kuboresha kilimo cha zao hilo ni kama ifuatavyo:-

- (i) Kutenga fedha kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya, yaani *District Agricultural Development Plans (DADPs)* na *District Irrigation Development Fund (DIDF)*, kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya umwagiliaji kwa mazao yenye thamani kubwa likiwemo zao la vitunguu swaumu;
- (ii) Kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya matrekta madogo (*power tillers*) ili kuongeza uzalishaji wa vitunguu swaumu kwa kuongeza eneo la uzalishaji; na
- (iii) Kuhamasisha wakulima kutumia mpango wa stakabadhi ghalani ambao umeonesha mafanikio mazuri kwa msimu wa 2009/2010 katika Wilaya ya Mbulu kwa zao la vitunguu swaumu.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kuongeza tija katika uzalishaji wa zao la vitunguu swaumu, Wizara itatuma wataalam wa mazao ya bustani (*Horticulture*), kukagua kilimo cha vitunguu swaumu huko Bashay ili kutambua fursa na changamoto zinazowakabili wakulima wa zao hilo. Pamoja na hatua hiyo, wakulima wanashauriwa kutumia Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA) na *Tanzania Horticultural Association (TAHA)*, kupata habari za masoko ili kuchochaea uzalishaji wa zao hilo.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Martha Umbulla, kwa kuibua suala hili hasa la mazao haya ya bustani.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hiyo. Ninampongeza Naibu Waziri, kwa majibu yake yenye matumaini kwa wakulima wadogo wa vitunguu swaumu kule Bashay, Wilayani Mbulu. Pamoja na majibu hayo mazuri, nina swalii moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na zao hili kuwa na faida kubwa kwa maana ya kuuzwa debe moja shilingi 70 hadi laki moja au karibia shilingi laki nne na zaidi kwa gunia moja na pengine laki saba hadi milioni moja katika Jiji la Dar es Salaam; bado zao hili halijapewa hamasa kubwa kwa wakulima wadogo kulilima kwa wingi kutokana na kukosa soko la uhakika na la karibu. Je, Serikali sasa ili kuhamasisha zao hili lenye faida kubwa namna hii katika Kata ya Wilaya ya Mbulu na kwingineko hapa nchini; itasaidia vipi wakulima wadogo wakiwepo makundi ya wanawake na vijana ili waweze kulima zao hilo kwa wingi waweze kupata faida kubwa? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyo sema katika majibu ya msingi, ninampongeza sana Mheshimiwa

Martha Umbulla, kwa sababu ametukumbusha zao ambalo lilikuwa bado halijawekewa mkazo mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ninapenda niseme kwamba, kati ya mazao ambayo hayajapata msukumo mkubwa ni haya mazao ya bustani, ambayo ni pamoja na mboga, matunda, viungo na maua; na hivi sasa Serikali yetu tunapata fedha kidogo sana, takriban shilingi bilioni tatu tu kwa mwaka ukilinganisha na wenzetu wa Nchi ya Kenya, ambao wanauza zaidi ya bilioni tatu. Sisi tunapata milioni 380, wenzetu zaidi ya bilioni tatu kwa mwaka. Kwa hiyo, Mheshimiwa Martha Umbulla, ameibua jambo ambalo ni la msingi sana. Kama nilivyosema, wakulima wanaolima vitunguu swaumu washirikiane na *Tanzania Horticulture Association*, ambayo Makao Makuu yake yako pale Arusha na nimewasiliana na *Executive Director*, ambaye anaitwa Jackline Mkund; ameomba sana Mheshimiwa Mbunge na Wakulima wawasiliane naye kwa sababu ye ye pia anasaidia kutafuta masoko na namna ya kuwawezesha Wakulima kuweza kulima zao hili. Vilevile kwa Sheria Na. 19 ya 2009, tumeanzisha Bodi ya Mazao Mchanganyiko. Mimi nitamwomba Mwenyekiti wa Bodi hii, ambaye alikuwa pia Naibu Waziri na Mbunge katika Bunge lililopita, aangalie namna ya kulisimamia zao hili la vitunguu swaumu ambalo linaonekana lina bei nzuri kwa wakulima.

Na. 85

### **Utekelezaji wa Bajeti ya Nchi**

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR** aliuliza:-

Bajeti ya nchi yetu inategemea fedha za ndani na za nje (Wafadhili) lakini utekelezaji wa matumizi ya bajeti hiyo mara nyingi unakwamishwa kwa kutopatikana kwa fedha za baadhi ya Wafadhili wa nje ambao wamekuwa wakiahidi kusaidia bajeti yetu: Je, Serikali inachukua hatua gani hali kama hiyo inapotokea?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, ninapenda kujibu swalii la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Serikali inapata misaada kutoka nje kwa njia kuu tatu; nazo ni hizi zifuatazo: Misaada na mikopo kupitia Bajeti ya Serikali (*General Budget Support*); vile vile mifuko ya pamoja ya kisekta (*Basket Funds*); na misaada ya Miradi Maalum ya Maendeleo (*Project Funds*). Misaada ya kibajeti inachangia moja kwa moja Bajeti ya Serikali (mfuko wa jumla wa Serikali) ili kuchochaea utoaji wa huduma muhimu unaolenga kupunguza umaskini kwa jamii kama ilivyoainishwa katika MKUKUTA. Mifuko ya pamoja ya kisekta inatumika kuchangia kwa kiasi kikubwa, kugharamia programu muhimu ya kuboresha maendeleo ya Serikalini na shughuli za maendeleo katika ngazi za sekta husika. Misaada ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo huwa inalenga miradi mahususi.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa ujumla, umekumbwa na changamoto nyingi ikiwemo ya Washirika wa Maendeleo kutoa fedha chini ya kiwango wanachoahidi. Hali hiyo hutokana na mabadiliko ya uongozi katika nchi zao, mabadiliko ya hali ya uchumi duniani au taratibu za utekelezaji wa miradi husika kutokamilika kwa wakati uliotegemewa. Kwa kuwa tumekuwa tunatumia kile tunachopata, yaani *Cash Budget*, Serikali imeendelea kutenga fedha za matumizi kulingana na upatikanaji wa mapato, ikiwa ni pamoja na kulinda na kutoa kipaumbele zaidi katika kutenga fedha za kugharamia Miradi ya Maendeleo.

Pindi kunapotokea upungufu wa misaada na mikopo ya kibajeti, kwa kupitia kama nilivyosema *Cash Budget Support*, Serikali hupunguza matumizi yake ya kawaida bila kuathiri viashiria vya ukuaji wa uchumi kwa kuwa Serikali hulinda vichocheo vya ukuaji uchumi kwa kutopunguza matumizi yake. Vichocheo hivyo ni pamoja na ruzuku kwa ajili ya pembejeo za kilimo, upatikanaji wa umeme, barabara, kugharamia elimu na usalama wa raia na mali zao.

Mheshimiwa Spika, pindi kunapotokea upungufu katika Miradi ya Maendeleo pamoja na Mifuko ya Kisekta inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo, miradi hiyo inayotekeliza huahirishwa mpaka fedha itakapopatikana.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, ninaomba kumwuliza maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa sambamba na baadhi ya wafadhili kuahidi na kutokuchangia Bajeti ya Serikali; na kwa kuwa kuna baadhi ya wafadhili huwa wanaahidi na huchangia lakini katika *quarter* ya mwisho; je, Serikali inakabiliana vipi na tatizo kama hilo?

(ii) Kwa nini Serikali inapendelea utaratibu wa *General Budget Support (GBS)* badala ya ule wa fedha kwenda moja kwa moja katika Miradi inayohusika? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA):** Mheshimiwa Spika, la kwanza kama alivyosema yeye, endapo hawa wafadhili wanaoleta pesa kwa Serikali dakika ya mwisho kabisa halafu sisi tunashindwa kutekeleza yale ambayo tumeyadhamiria; kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba; huwa hatuna namna, namna pekee ni kupunguza Bajeti ya Maendeleo ya Kawaida, yaani *Recurrent Budget*. Itabidi tuangalie na kupunguza sehemu mbalimbali ili tuweze kuendelea mwaka wa fedha unaohusika na kama ni Miradi kama nilivyosema, sehemu ya fedha hizo zinapohusu Miradi, basi Miradi ile inaahirishwa mpaka pesa itakapopatikana hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, swali la pili nalo vilevile kama ambavyo nimesema kwenye jibu la swali la msingi kwamba, Serikali inapata misaada kutoka nje kwa njia kuu tatu; nazo kama nilivyosema ni ile ya misaada na mikopo kwa njia ya kupitia *General Budget Support* na Mifuko ya Pamoja ya Kisekta (*Basket Funds*) na Mifuko ya Miradi Maalum ambayo kama nilivyosema ni *Project Funds*. Sasa analouliza Mheshimiwa Mbunge ni

kwamba, kwa nini Serikali inapendelea *General Budget Support*; misaada ya kibajeti kupitia *General Budget Support* ndiyo mfumo unaopendelewa na Serikali katika kuchangia moja kwa moja Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, hii inachochea utoaji huduma muhimu na unaolenga kukuza uchumi na kupunguza umaskini kupitia MKUKUTA ambao tunaendelea nao kwa kipindi cha awamu ya pili.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa itikadi ya chama kinachoongoza Serikali leo ni pamoja na ujamaa na kujitegemea; na kwa kuwa misaada inalemaza na inafifiisha juhudzi za ndani za kujiimarisha na kujitegemea; na kwa kuwa Mataifa mengine ikiwemo jirani zetu Kenya waliweza kwenda kwa miaka kumi wakitegemea misaada kutoka nje wakati wa dharura isiyozidi asilimia tano; je, ni lini Serikali yetu itatusaidia kwa kutuwekea ukomo wa mipango ya namna ya kukopa na vilevile Serikali itaweza kuweka mikakati ya ndani kuhakikisha kwamba heshima ya Taifa inalindwa kwa kupunguza mikopo ambayo tunapata kutoka kwa Wafadhili?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa fursa. Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea na hasa kujitegemea, hakuna maana ya kwamba, hatuwezi kushirikiana na watu wengine duniani. Tunaendelea kujitegemea na bado tutaendelea kufanya biashara na tutaendelea kupata misaada ya wale ambao wako tayari kutusaidia. Tutaendelea kukopa na hata Mheshimiwa Mbewe anafanya biashara anakopa; kwa sababu kukopa siyo kuacha kujitegemea. (*Makofi/Kicheko*)

Na. 86

### **Tatizo la Msongamano wa Magari Dar es Salaam**

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR** aliuliza:-

Msongamano wa magari katika miji yetu umekuwa wa kutisha kutokana na kasi kubwa ya kuingizwa magari nchini hasa yaliyochakaa licha ya kuwekewa *extra duty* na kama hatua zipasazo hazitachukuliwa kudhibiti hali hiyo tatizo hilo litaleta usumbu mkubwa sana siku za usoni: -

Je, Serikali haioni haja ya kufuta ushuru huo wa ziada na kuweka utaratibu wa kuingizwa magari nchini kwa kuruhusu magari ya mwaka 2000 na kuendelea na yale yaliyo chini ya umri huo yasiruhusiwe kuingizwa nchini kama jitihada za kupunguza tatizo la msongamano na ajali za mara kwa mara?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, idadi ya magari katika nchi yetu, imeongezeka sana ikilinganishwa na miaka michache iliyopita. Hadi kufikia Februari mwaka 2011, jumla ya magari 816,131 yalikuwa yameandikishwa bila kuhusisha Magari ya Serikali na Taasisi zake na yale ya Miradi inayofadhiliwa na Wahisani (*Donor Funded Projects*).

Mheshimiwa Spika, asilimia 70 ya magari yote yanayoingizwa nchini hubakia katika Jiji la Dar es Salaam. Hii inaendana pia na mahitaji halisi ya usafiri na usafirishaji katika jiji la Dar es Salaam ambalo lina watu zaidi ya milioni nne. Idadi ya magari sambamba na mifumo duni ya miundombinu, yaani *infrastructure* iliyopo ni mojawapo ya sababu za msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam. Kwa upande mwingine takwimu zinaonesha kuwa ipo Miji mingi katika nchi yetu ambayo ina idadi ndogo ya magari ikilinganishwa na mahitaji halisi ya usafiri na usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, tatizo la msongamano wa magari lipo Dar es Salaam na baadhi ya Miji kama vile Arusha na Mwanza. Kwa hiyo, kuweka ushuru au sheria inayolenga kudhibiti uingizaji wa magari katika Jiji la Dar es Salaam pekee, kutaathiri nchi nzima ikiwemo Mikoa na sehemu ambazo zina upungufu wa magari kulingana na mahitaji halisi.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja la nyongeza. Je, ni kwa nini Serikali haioni ipo haja ya kupunguza ushuru wa magari mapya ili wananchi wasiendelee kununua magari chakavu?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI – MHE. PEREIRA AME SILIMA:** Mheshimiwa Spika, kupunguza ushuru kwa magari ya zamani yanayoingia kwa kweli kwa Serikali itakuwa ni jambo ambalo siyo jema kwa sababu sasa hivi tunaweka kodi kubwa kwa hayo magari ili kuweza kuwa-*discourage* watu wasiweze kuingiza magari hayo ambayo ni ya zamani.

## T A A R I F A

**MHE. MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa.

**MHE. MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, swali la nyongeza alilouliza Mheshimiwa Mbunge, sio swali alilolijibu Mheshimiwa Waziri.

**SPIKA:** Kwa nini?

**MHE. MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, swali lililoulizwa la magari mapya ni kwa nini yasipunguziwe ushuru, yeye akajibu magari kuukuu.

**SPIKA:** Amejibu *the other way round*. Anasema, wameweka kodi kubwa sana kwa magari kuukuu kusudi waya-*discourage*. Maana yake ni mapya yaingie. Amejibu *the other way round*.

Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na utalii. Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine. (*Makofi*)

Na. 87

### **Migogoro Kati ya Wafugaji na Mamlaka ya Hifadhi ya Serengeti**

**MHE. NYAMBARI M. NYANGWINE** aliuliza:-

Kumekuwepo na mgogoro kati ya wananchi wafugaji wanaoishi katika vijiji kando ya Hifadhi ya Serengeti vya Mrito, Gibaso, Masanga, Gong'ora, na kadhalika dhidi ya Mamlaka ya Hifadhi ya Serengeti kugombea maeneo ya malisho ambao umedumu kwa muda mrefu sasa:-

- (a) Je, kwa nini Serikali isisimamishe Mamlaka ya Hifadhi ya Serengeti kuacha mara moja kuyaingilia maeneo ya Vijiji hivyo vilivyotajwa ili wanavijiji waendelee kutumia maeneo hayo kwa ajili ya malisho ya mifugo yao?
- (b) Je, kwa nini Mamlaka hiyo isichukuliwe hatua za kisheria kwa kujinyakulia maeneo ya Vijiji vya Tarime bila ridhaa ya wanavijiji wenyewe?
- (c) Je, ni lini Mamlaka ya Hifadhi ya Serengeti itaacha manyanyaso ya kuwakamata na kuwashitaki wananchi isivyostahili na kuwanyima haki ya kuendelea kulisha mifugo katika maeneo yao?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, kwanza naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, Mbunge wa Jimbo la Tarime, kwa ushindi mnono alioupata kwa kupitia Chama cha Mapinduzi. Kwa heshima hiyo hiyo naomba nijibu swali lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwepo na mgogoro kati ya Hifadhi ya Serengeti na wananchi kuhusu maeneo ya malisho ambapo wananchi wamekuwa wakivamia maeneo ya hifadhi ili waweze kulisha mifugo yao. Hali hii imechangiwa kwa kiasi kikubwa na wananchi kutokuwa na maeneo ya malisho katika vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge na maeneo pekee yanayobaki kuwa malisho ni yale yaliyopo ama pembezoni sana na hifadhi au ndani ya hifadhi yenye.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Tarime kulikuwa na eneo la wazi la uhifadhi, yaani *Game Controlled Area*, linaloitwa Gong'ora lililokuwa likitumika kwa malisho. Hata hivyo, eneo hilo lilivamiwa na wananchi na kujengwa makazi ya kudumu na kilimo, jambo ambalo kwa kiasi kikubwa limechangia kuondoa au kukosekana kwa malisho katika eneo hilo. Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ilianzishwa kisheria kwa tangazo la Serikali Na. 235 la mwaka 1968 na maeneo yake yote yameainishwa. Tangu kuanzishwa kwake, mipaka ya hifadhi haijabadilika, badala yake wananchi wameongezeka na kutumia ardhi yote iliyopo nje ya Hifadhi, hivyo kusababisha migogoro kati ya Hifadhi na wananchi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuongezeka kwa migogoro hiyo, Shirika la Hifadhi za Taifa – *TANAPA*, kuanzia mwaka 2008 limeanza zoezi maalum la kupitia upya mipaka yake ili kuondokana na mipaka ambayo ni *descriptive*, yaani inatumia alama za ardhini kama milima, miti na kadhalika na kutumia mipaka ya kisasa inayotumia *GPS* inayotambulika wazi. Katika zoezi hilo, maeneo ambayo yamekuwa yakibainika kuwa nje ya hifadhi yamekuwa yakirejeshwa kwa wananchi. Mfano, halisi ni kama eneo la Bonde la Nyanungu pamoja na maeneo ya pembezoni mwa hifadhi, kwa mfano, Hifadhi ya Mikumi eneo la Kijiji cha Boma ambayo yanatokea kwamba yapo nje ya hifadhi yanarejeshwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, ningependa nimwombe Mheshimiwa Mbunge kwamba zoezi hili linaendelea na hivyo nimshauri ashirikiane na Halmashauri ya Wilaya ya Tarime kuweka mipango ya matumizi bora ya ardhi kwenye maeneo ambayo yapo nje ya hifadhi. Lakini pia watoe ushirikiano katika zoezi ambalo linaendelea kubainisha mipaka ya hifadhi na kuiwekea alama.

**MHE. NYAMBARI M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kwa kuwa Mheshimiwa Rais, mwaka jana alipokuwa katika Wilaya ya Tarime alijadiliana na wazee wa jadi na mila na akashauri kwamba suala hilo la mgogoro litashughulikiwa mara moja na akamwagiza Mkuu wa Mko wa Mara kulisimamia. Naomba nifahamishwe: Je, ni hatua zippi zimechukuliwa mpaka sasa hivi?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, kwa kuwa kumekuwepo na wanyama waharibifu wanaoingia katika Vijiji hivyo vilivyonajwa na hususan Vijiji vya Gibaso, Mrito pamoja na Kijiji cha Gong'ora ambao huharibu mazao ya wakulima na mpaka sasa hivi hakuna hatua zozote ambazo zimechukuliwa, hususan malipo ya fidia: Je, Mheshimiwa Waziri, anatoa kauli gani kuhusiana na uharibifu huo unaofanywa na wanyama hususan ndovu?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama nilivyosema kwenye zoezi hili la kubainisha mipaka ya hifadhi vizuri, kuna maeneo ya Bonde la Nyanungu ambayo mengi yapo nje ya Hifadhi na wananchi walikuwa wakibughudhiwa wanapokwenda kulisha mifugo yao kwenye eneo hilo.

Mwaka jana Mheshimiwa Rais alipotembelea eneo hilo, aliagiza kwamba maeneo haya yabainishwe wazi na wananchi wasibughudhiwe kwa sababu yapo nje ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, maeneo haya ya Mheshimiwa Rais tunayatekeleza na kwa sasa hivi ambacho *TANAPA* wanafanya ni kuweka alama za kudumu kwenye maeneo ambayo yapo nje ya hilo bonde na wananchi wanaendelea kutumia eneo ambalo lipo nje ya Hifadhi. Maelekezo haya ya Mheshimiwa Rais, yanahusu pia maeneo mengine yote nchini ambayo kwa namna moja ama nyingine mipaka yake imekuwa haipo bayana.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni kwamba kumekuwepo na migongano ya wananchi na wanyama kutoka hifadhini na kuharibu mazao ya wananchi. Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009, ilianisha utaratibu mpya ambao utakuwa unatumika kwa ajili ya kusaidia kulipa kifuta machozi pale ambapo wananchi wanakuwa wameuawa na wanyama na kulipwa kifuta jasho pale mazao yatakapokuwa yameharibiwa. Baada ya Sheria kuwa imepita, Kanuni zinazosimamia ulipaji wa kifuta machozi zimeshakamilika na nimezisaini mwezi uliopita, mwezi Machi na hivi sasa zinatumika.

Ninamwomba Mheshimiwa Mbunge awasiliane na mimi baadaye niweze kumpatia kopi ya hizo Kanuni, pamoja na Wabunge wote wengine ambao wapo-*interested* ili waweze kujua utaratibu ambao unatumika kwa ajili ya kulipa kifuta jasho.

Na. 88

### **Deni La *ZECO***

**MHE. HABIB JUMA MNYAA** aliuliza:-

Shirika la *TANESCO* linalalamikiwa kuhusu deni la shilingi milioni 718.5 linalodai *ZECO*; fedha hizo ambazo *ZECO* inazidai Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Wizara ya Mambo ya Ndani, hutengwa katika bajeti ya kila Wizara ingawa hawazilipi:-

- (a) Je, Serikali iko tayari kuliondoa deni la *ZECO* kwa *TANESCO* kwa kuwa Mawaziri wa Wizara zote hizi ni rahisi kulipana kwa kuwa wanakutana Bungeni au katika Baraza la Mawaziri?

- (b) Je, Bajeti zinazopitishwa Bungeni hutumiwa ipasavyo?
- (c) Kama hazitumiki ipasavyo, kwa nini kusiwe na uwajibikaji kwa wale wanaofanya makosa ya matumizi yasiyopangwa ya fedha za umma?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Habib Juma Mnyaa, Mbunge wa Mkanyageni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mkataba wa makubaliano ya *TANESCO* kuiuzia umeme *ZECO PPA* kwa mara ya mwisho ulisainiwa tarehe 22 Aprili, 2010. Lengo la Mkataba huo ni kuweka maelewano ya msingi ya kufanya biashara ya kuuza na kununua umeme kati ya *TANESCO* na *ZECO*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa uhusiano wa *ZECO* na *TANESCO* ni wa kibiashara kupitia mkataba maalum, deni la *ZECO* kwa *TANESCO* linapaswa kulipwa kulingana na taratibu zilizoafikiwa ndani ya mkataba na sio kwa utaratibu unaopendekezwa na Mheshimiwa Mbunge, kupitia maelewano Bungeni kati ya Mawaziri wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Serikali kwa kushirikiana na *EWURA*, *TANESCO* na *ZECO*, zinatafakari njia bora na ufumbuzi wa kudumu wa kero ya madeni inayodaiwa *ZECO*.

Mheshimiwa Spika, tarehe 31 Machi, 2011 *TANESCO* na *ZECO* walikutana kujadili hoja za msingi zinazolalamikiwa, ambapo kwa pamoja walikubaliana aajiriwe mtaalamu mshauri wa kutathmini gharama halisi za uzalishaji na usafirishaji umeme kwa upande wa *TANESCO* kwa umeme unaouzwa *ZECO*. Matokeo ya tathmini hiyo yatatumiwa na *EWURA* kupanga upya bei ya umeme unaouzwa *ZECO* na hatimaye kuweka msingi mzuri wa kushughulikia suala zima la madeni ya umeme kwa *ZECO*.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Ofisi ya Taifa ya Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali, hujiridhisha na matumizi ya fedha za Serikali yanayofanywa katika Wizara, Mashirika, Taasisi na Idara mbalimbali za Serikali baada ya kupitia ripoti zinazowasilishwa kila mwaka.

(c) Mheshimiwa Spika, Sheria inayosimamia taratibu na Kanuni za kufuatwa wakati wa kuidhinisha matumizi ya fedha za umma ziko wazi na wajibu wa kuzingatia sheria hizi wakati wa utekelezaji wa majukumu umeelezwa bayana. Serikali imekuwa ikisimamia kwa karibu utekelezaji wa sheria, taratibu na Kanuni za fedha na hatua za kinidhamu stahili kwa mujibu wa sheria hizi huwa zinachukuliwa kwa wale wanaokwenda kinyume cha taratibu hizo.

**MHE. HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri anasema uhusiano wa *TANESCO* na *ZECO* ni Mkataba wa kibiashara, na kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekataa kulipa hilo deni la

shilingi bilioni 44 kwa sababu za msingi, na kwa kuwa umeme ulipopandishwa bei mwaka jana katika upande wa Tanzania Bara ulizidi zile *tariffs* kwa asilimia 21, lakini kwa upande wa Zanzibar ulizidi kwa asilimia 168: Je, hivi Jamhuri ya Muungano ina sababu za msingi kupandisha bei kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kwa asilimia 168 au ndio inatoa *message* sasa kwamba Zanzibar izalishe umeme wao kwa kujitegemea? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, miundombinu yote kutoka *Ras Kilomoni*, Ubungo mpaka Zanzibar, iligharimiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, na kwa maana hiyo kuna sababu gani ya kumtafuta mtaalamu mshauri na wakati huo tayari kulishakuwa na maelekezo ya viongozi wakuu wa nchi? Au ndio njia ile ile ya kumtafutia mtu ulaji? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa maana nyingine suala hili ni mtambuka ambalo linahusu pia deni linalodai *ZECO* kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Wizara ya Mambo ya Ndani. Je, Serikali itahakikishaje sasa na Wizara hizi za Muungano zitailipa *ZECO*?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mnyaa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tatizo la *EWURA* kupandisha bei ya umeme kwa asilimia 21 kwa upande huu wa Bara na asilimia 168 kwa upande wa Zanzibar, ni jambo ambalo *EWURA* wamelifanya kazi na wameona kwamba kwa zile gharama zinazozalishwa umeme, umeme unaouzwa kwa *tariff* inayouzwa Zanzibar ni ndogo sana ukilinganisha na gharama ya umeme unaopelekwa. Katika majibu yangu nimesema kwamba *ZECO* na *TANESCO* ni vyombo vya kibiashara.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mnyaa ameniuliza swali ambapo katika swali lake amesema badala ya wao kukaa kama vyombo vya kibiashara, sisi Wizarani Mawaziri tukae hapa Bungeni tuliamulie jambo hili ambalo wao wana mkataba wa kibiashara. Kwa hiyo, kwenye jibu langu nikasema wao wakutane kwa sababu wana makubaliano, wana mkataba, wakae na Mshauri Mwelekezi, *Mediator* kati yao, eeh, bwana hii sawa na hii sawa, hii hapana, hii sawa; wataafikiana. Wakishaafikiana bado Serikali hizi mbili, yaani sisi na wenzetu kule *MUNA*, tutakaa na kusema haya, hilo jambo limeafikiwa litekelezwe.

Mheshimiwa Spika, hakuna mgogoro katika hili kwa sababu Serikali ya kule na Serikali ya huku, sisi wote ni wamoja. Kwa hiyo, sioni taabu yoyote itakayopatikana katika jambo hili. Kama ingekuwepo taabu, mimi naamini *TANESCO* wangekuwa wamesema kama wanavyofanya, wanasesma aah, basi kwa kuwa hawataki kulipa deni tufunge umeme. Hawawezi. Kwa sababu Serikali haiwezi kuruhusu hilo likatokea. Ndio maana nimesema tumewaachia wazungumze, wana mkataba wa kibiashara na mimi ninaamini wakitumia utaalamu wa Mshauri Mwelekezi, atawafafanulia ni njia gani wapite ili wapate ufumbuzi wa suala hili.

Mheshimiwa Spika, hili la pili la gharama za miundombinu, sina uhakika na hili kwamba miundombinu yote kutoka Ubungo mpaka Zanzibar, imegharimiwa na Serikali ya Mapinduzi. Inawezekana ni kweli, lakini umeme hauzalishwi Ubungo, umeme unazalishwa Mtera na kwingine. Kwa hiyo, umeme unapokwenda Zanzibar, Mwanza, Mbeya, gharama yake inaanzia pale kwenye kituo cha uzalishaji. Sio pale kwenye kituo cha Ubungo kwenda mbele, hapana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ndio maana nikasema kwenye kutathmini hili jambo *EWURA* na wataalamu wengine wote watakaa, wataafikiana. Tarehe 31 *TANESCO* na *ZECO* wamekutana, wameshindwa kuafikiana, lakini sio mwisho wa majadiliano. Wataendelea kuzungumza mpaka suala hili lipate ufumbuzi na sisi tutasimamia wapate ufumbuzi kwa sababu Serikali ya chama hiki, kama ilivyokuwa Serikali yenyewe na Chama ni ya Muungano, kwa hiyo tutapata ufumbuzi. (*Makofifi*)

Na. 89

### **Mpango wa Umeme Vijijini**

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE** aliuliza:-

Serikali kupitia mpango wa umeme Vijijini, ilipeleka umeme katika mashamba makubwa ya Kahawa Oldean na Kijiji cha Mang'ola ni kilometra chache tu kutoka mashamba ya kahawa ya Oldean:-

Je, ni sababu zipi zinazoifanya Serikali kutokupeleka umeme kwa wakulima wa kilimo cha umwagiliaji wa vitunguu, mpunga na mahindi wa Mang'ola?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mch. Israel Natse, Mbunge wa Karatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kupeleka umeme kijiji cha Mangola, maarufu kwa kilimo cha umwagiliaji wa vitunguu, mpunga na mahidni, inahitajika jumla ya shilingi bilioni 1.11. Gharama hizi zinahusu ujenzi wa kilometra 42 za njia ya umeme katika msingo wa KV 33, ujenzi wa vituo vitano vya kupoza umeme na ujenzi wa kilometra 10 za njia ya umeme msongo wa KV 0.4. Kutokana na ufinyu wa bajeti katika Shirika la Umeme la *TANESCO* fedha za utekelezaji wa mradi huu, zinatafutwa ikiwa ni pamoja na kuhusisha wakala wa nishati vijijini, *REA*.

Mheshimiwa Spika, napenda kumwomba Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi ambao wengi wao ni wakulima wa umwagiliaji wa vitunguu, mpunga na mahindi Mangole, kuwa na subira wakati Serikali inatafuta fedha za kugharamia utekelezaji wa mradi huu.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri; kwa kuwa Serikali imekiri ni kutokana na ukosefu na ufinyu wa bajeti ya *TANESCO*. Na kwa kuwa, Naibu Waziri pia amekiri kwamba fedha za mradi zinatafutwa.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa njia mbadala? Ni lini wananchi wangu wavute subira?

(b) Je, Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba Serikali imewatelekeza wananchi wake kwa kuwawezesha wawekezaji wa nje kuliko wananchi wazawa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa ridhaa yako, naomba nimjibu Mheshimiwa Mchungaji Natse maswali yake ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tatizo hili la kupeleka umeme Mangola ni tatizo linalofanana na maeneo mengine ya Tanzania ambayo maombi yamekuja ya kupeleka umeme na kwa sababu ni sera ya Chama chetu kupeleka umeme kwa maeneo mengi. Kuna vigezo vya kupeleka umeme. Tunaangalia vile vigezo, uzalishaji uwangi wa watu, shughuli za kiuchumi na kadhalika na tunapeleka kwenye maeneo hayo. Kwa hiyo, ombi hili la kupeleka umeme Mangola ndiyo maana nimesema litagharimu shilingi ngapi, kwa sababu limeshafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, napata taabu kidogo kwenye lile swalii la pili linalosema Serikali imewatelekeza wananchi wake; wa wapi, wa Karatu; maana yake Karatu ina Vijiji 43, Vijiji 11 vina umeme na umeme huo umekwenda kwa mradi *electricity form* mwaka 2000 na miradi mingine kuna Vijiji kama Endabashi na wapi na wapi vimepata umeme 2006/2007 na hivi sasa kuna Vijiji, jina kidogo zito. Kuna Kijiji kinaitwa Endamarieki na Bashai viko katika utaratibu wa kupata umeme hivi sasa. Kwa hiyo, Serikali hii ya CCM ambayo wengine hawataki kuitambua wanaipiga madongo ndiyo Serikali hii ambayo inayopeleka huduma hizi kwa wananchi wake wote bila kuwabagua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningependa Mheshimiwa Mbunge aridhie avute subira kama nilivyosema, tunaifanya mikakati kama ilivyokuwa kwenye maeneo mengine, ye ye aendelee kushukuru kwamba Serikali ya CCM itamfikishia miradi hii na ukipenda unawenza kushukuru hadharani na mimi namhakikishia kwamba, kama ilivyokuwa kwa miradi mingine na hii tutatekeleza. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Muda umekwisha na maswali yamekwisha, tena tumekula muda usiokuwa wa kwetu.

Waheshimiwa Wabunge, hapa nina wageni wenu. Nina wageni wa Bunge *Sport Club* amba ni wasani wa filamu nchini wakiongozwa na Jacob Stephen maarufu JB, basi yuko JB hapo wameongozana na Stephen Kanumba, Stephen Nyerere, Vicent Kigosi maarufu kama Ray, Singo Mtambalike maarufu Richie, Jacquline Wollupa, Jenifer Kiyaka na Zuena Mohamed. Sasa wasanii hao wamekuja kucheza mpira wa miguu na *Netball* na Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Halafu ujumbe walionao pia wanatumia hii michezo kutangaza amani ndani ya nchi ya Tanzania. Kwa hiyo, tunawashukuru sana. Hii imeletwa na Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* - Mheshimiwa Amos Makalla, tunawashukuru kwa hili tangazo la amani. Mimi kabla ya kuanza Bunge hili nilikaribishwa na Bunge la Liberia na Sierra Leon, kwa sababu nchi hizi zimepigana sana katika miaka michache iliyopita, Liberia wamepigana miaka 14 wao kwa wao halafu Sierra Leon wamepigana miaka 11 wao kwa wao. Ukiona wananchi kule Sierra Leon utakuta wengine wamekata viwiko mikono hivi, wale walikuwa wanawaambia, wanakushika mkono wanakuuliza: unataka *short sleeve*? ukisema *short sleeve* wanakukatia juu ya kiwiko mikono yote. Uki sema unataka *long sleeve* wanakukatia kwenye viganja. Kwa hiyo, unawakuta kabisa watu hawana mikono kwa sababu ya upuuzi amba o hata wao leo ukiwaliza kulikuwa na nini hawawezi kueleza. Lakini bado kule kuna Watanzania wengi. Wapo Watanzania wamekaribishwa kuwasaidia *ku-form government*, kwa mfano, wanasaidia kuunda Jeshi la Magereza kwa hiyo, walitukaribisha. Watanzania waliokuwa kule ni wengi sana. Wengine wako kwenye *UN* wengine wako kwenye mambo mengine ya kufundisha kurudisha Serikali zile katika hali nzuri.

*Sierra Leon* hivyo wako Watanzania kule wameunda Serikali, lakini nayo pia ina matatizo lakini wako pale wanawasaidia sisi, walitukaribisha kama Liberia na Mheshimiwa Mboge huyu Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, lakini kama Mwenyekiti wa CHADEMA pia alikuwa amekaribishwa pia kwa shughuli nyingine, walikwenda huko na waliwakaribisha. Wote kwa pamoja walituambia nyie Watanzania tunawaomba fanyeni mnayotaka, lakini amani yetu mtulindie. (*Makofi*)

Kwa hiyo, nawashukuru wasanii wetu hawa kwa kutangaza amani. Jamani amani bei yake sio kubwa, wala haipo, lakini gharama zake ni kubwa. Kwa hiyo, naombeni hili mlifahamu. Kwa hiyo, nawashukuru na mnakaribishwa mtaendelea na wenzetu wa *Sports Club* kufanya shughuli zenu kama kawaida. (*Makofi*)

Sasa nina matangazo ya kazi. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, Mheshimiwa Boniface Simbachawene anaomba niwatangazie Wajumbe wa Sheria ndogo kwamba kutakuwa na kikao cha kuendelea kujadili Muswada wa Sheria ya Uendeshaji wa Mahakama, 2011 (*The Judicial Administration Bill, 2011*) leo hii tarehe 13 saa 7.00 mchana katika chumba Na. 219. Ni saa 7.00 mchana kwa sababu asabuhi hii tuna shughuli nyingine.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama - Mheshimiwa Mussa Zungu, naye anaomba niwatangazie Wajumbe wa

Kamati yake hiyo kuwa kutakuwa na kikao kwa Kamati hiyo leo saa 5.00. Hapana, saa 5.00 haiwezekani, naomba niwafanyie saa 7.00 katika Ukumbi Na. 231. Ni saa 7.00 kwa sababu asubuhi wote hapa tuna shughuli.

Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala - Mheshimiwa Pindi Chana naye anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Katiba Sheria na Utawala kwamba kutakuwa na kikao cha Kamati leo tarehe 13 saa 7.00 katika Ukumbi wa Pius Msekwa C.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali - Mheshimiwa John Momose Cheyo, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuwa kutakuwa na kikao cha Kamati leo saa 7.00 mchana katika Ukumbi Na. 227. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Fedha na Uchumi Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Fedha na Uchumi kuwa kutakuwa na kikao cha Kamati leo, sio saa 5.00 kwa sababu wote tuna kazi hapa.

Mheshimiwa Vita Rashid Mfaume Kawawa - Katibu Mkuu wa APNAC ni Chama kinachojenga uwezo wa Wabunge katika mapambano dhidi ya rushwa kwa kutumia njia mbalimbali kama vile makongamano mafunzo, semina na mambo mengine hayo. Yeye anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote wanaotaka kuijunga na mtandano wa Wabunge wanaopambana na rushwa wajiorodheshe hapo kwenye jengo la kuingilia ukumbini mapokezi hapo, kunatolewa fomu. Kwa hiyo, mkitaka kuingia katika hiki Chama, basi unakwenda kuchukua fomu pale na ujiorodheshe pale.

Mheshimiwa David Kafulila anaomba niwatangazie Wabunge wote wa NCCR MAGEUZI kuwa watakuwa na kikao saa 7.00 mchana chumba 214. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Wako wanne.

**SPIKA:** Kwani wanne ni wachache! Wanatosha kabisa! (*Kicheko*)

Tunao watoto. Hawa wapo wiki nzima wanakuja, lakini wanaohusika hawakuwaandika, mimi naona kwa *uniform* zao, ni watoto wa shule ya kimataifa ya Martin Luther. Wanafunzi wa Martin Luther na Walimu wao kama wapo, basi wasimame. Wamekuja wiki nzima! (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, Martin Luther ni shule iko hapa hapa Dodoma, Waheshimiwa wengi hapa watoto wenu wako kule wasomasu na kwa kweli lazima tuwashukuru sana Walimu na Menejimenti ya shule ile, ina malezi mazuri sana, mimi mwenyewe nathibitisha. Kwanza kabisa ni-*declare interest*. Nasema hivyo kwa sababu nina mtoto wa mdogo wangu ambaye ni mlemavu, wangeweza kumrudisha, lakini wanaye, wanamtunza, wana maadili mazuri sana. Kwa hiyo, tunawashukuru sana Menejimenti, mwendelee vizuri kufanya hiyo kazi. Nimewatambua kwa *uniform*, hawakuniletea maelezo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tukiwa Bungeni huwa tunajitahidi kutoa huduma mbalimbali. Sasa hivi utawala unawatangazieni kwamba Waheshimiwa Wabunge Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kutambua umuhimu wa afya kwa Wabunge imeleta wataalam kwa ajili ya kupima afya kwa ujumla kwa Waheshimiwa Wabunge wote. Huduma hiyo itapatikana kwenye Ukumbi wa Msekwa kuanzia saa 7.00 mchana leo tarehe 13 Aprili, hadi tarehe 19. Kwa hiyo, wanaomba pia niwakumbushe Wabunge kwamba bado huduma zifuatazo zinatolewa hapa Bungeni. Hii ni ya afya, kwa hiyo, pimeni afya zenu, ni muhimu sana. Waziri asubuhi kaeleza, lakini pimeni afya zenu kusudi mjue hatua za kuchukua. Lakini huduma nyingine tulivyosema ya leseni iko hapo, vyeti vya kuzaliwa na *passport* mnaweza kuzipata hapo. Hii yote ni kusaidia msitumie muda mwingi huko mfanye kazi ambayo inastahili. Kwa hiyo, huduma hizo zipo.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine. Kuna mmoja sijui lini alikwenda kumwona Katibu wa Bunge ofisini kwake akasahau miwani yake pale.

Tangazo lingine *very serious*, Waheshimiwa Wabunge baadhi yenu hamjajaza zile fomu za kutangaza mali zenu, sasa ni mwezi Machi, kwa hiyo, hatua inayostahili hapo ni kufukuzwa Ubunge. Mnafahamu hivyo! Unafukuzwa Ubunge, sio kwamba unashitakiwa, unafukuzwa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nina orodha kubwa hapa, wote wamo humu. Kwa hiyo, ndugu zangu naombeni sana kama Wabunge wapya hamfahamu umuhimu wake, unafukuzwa Ubunge. Kwa hiyo, mkajaze, tena itabidi mjieleze *beyond reasonable doubt* kwanini hamkupeleka tarehe 31 Desemba? Kwa hiyo, sisi ofisini tunafanya kazi kuwaandikieni kama hamjitambui, tutawaandikia, lakini najua wengi mnajua kwamba hamja-*declare* mali zenu, ni suala zito kama hujipendi mwenyewe, basi endelea.

Nimeombwa tutangaze pia kwamba katika sisi Wabunge wote Bunge la Tanzania ni mwanachama wa Jumuiya ya Umoja wa Wabunge wa Jumuiya ya Madola, sisi ni wanachama. Sasa kama ni wanachama, pia tuna tawi letu hapa. Sasa kwa utaratibu kama ulivyokuwepo, Bunge lililopita viongozi wetu walikuwepo, wengine hawajarudi hapa, lakini pia wakati wa kufanya uchaguzi mwingine umefika. Kwa hiyo, mnatangaziwa hapa kwamba Waheshimiwa Wabunge mnaomba Wabunge wote mnaombwa kuwa tarehe 15 Aprili saa 7.00 mchana baada ya kusitisha shughuli za Bunge kutafanyika uchaguzi wa viongozi wa Kamati ya Utendaji wa Chama cha Jumuiya ya Madola (*The Commonwealth Parliamentary Association – CPA*) Tawi la Tanzania. Mimi ndiyo mlezi wa Tawi hilo.

Kwa hiyo, tutachagua Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Wajumbe wa Kamati hiyo, jumla yao ni 10, halafu kutakuwa na Wajumbe kutoka Chama Tawala wawili, Wajumbe kutoka Vyama vya Upinzani wawili, Wajumbe kutoka kundi la wanawake nafasi mbili, Wajumbe kundi la jumla nafasi nne. Fomu za kugombea nafasi hiyo zinapatikana katika Ofisi ya Katibu wa Bunge na aidha, uchaguzi huo utafanyika katika Ukumbi wa Pius Msekwa na muda wa mwisho wa kurudisha fomu hizo ni tarehe 14 Aprili, saa 10.00 jioni maana yake ni kesho tu.

Kwa hiyo, wanaopenda kuchukua zile fomu waende wakachukue pale kwa utaratibu ulioko huko, halafu uchaguzi utafanyika hiyo tarehe 15. Kwa hii hatufanyi uchaguzi humu kwa sababu ni kama Chama kilicho nje ya humu ndani. Kwa hiyo, mtafanya uchaguzi nje ya hapo. Baada ya hapo, Katibu.

**KATIBU:** Uchaguzi wa Wajumbe kwenye Taasisi mbalimbali za kibunge.

**SPIKA:** Msimamizi wa uchaguzi, maelezo.

**ND. JOHN N. JOEL – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Spika, leo ni siku rasmi iliyopangwa kwa ajili ya kufanya chaguzi za aina nne. Tutakuwa na uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika, kutakuwa na uchaguzi kujaza nafasi zilizoachwa wazi lile Bunge la *SADC*, halafu tutakuwa na uchaguzi wa kujaza nafasi moja ambayo haikufanyika kujaza nafasi ya *African Peer Review Mechanism (APRM)*. Kwa hiyo, hizo ni chaguzi tatu na pia tutakuwa na uchaguzi wa Wenyeviti watatu wa Bunge ambao wewe utautolea maelezo baadaye.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchaguzi wa Bunge la Afrika, kama nilivyowatangazia Waheshimiwa Wabunge tarehe 6 Aprili, 2011 na kama *Order Paper* ya leo inavyoonyesha, kutakuwa na uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika, uchaguzi huu unaendeshwa kufuatana na masharti ya nyongeza ya tano ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la mwaka 2007 Kanuni ya 5(a) ya nyongeza inaainisha makundi matano ya uwakilishi yanayotakiwa kama ifuatavyo:-

- Kundi A ni Wabunge wanawake nafasi moja;
- Kundi B ni Wabunge wa Zanzibar nafasi moja;
- Kundi C ni Wabunge wa Tanzania Bara nafasi mbili; na
- Kundi D ni Wabunge wa Kambi ya Upinzani nafasi moja.

Mheshimiwa Spika, wakati Bunge la Tisa linafikia ukomo wake, waliokuwa Wabunge wa Bunge la Afrika kufuatana na makundi yaliyotajwa hapo juu walikuwa kama ifuatavyo:-

Kundi A: alikuwa ni Mheshimiwa Balozi Getrude I. Mongella; Kundi B: Wabunge wa Zanzibar alikuwa ni Mheshimiwa Omar Sheha Musa; Kundi C: Wabunge wa Tanzania Bara, alikuwepo Mheshimiwa Athuman Janguo pamoja na Mheshimiwa Feetham Banyikwa na Kundi D: Kwa upande wa Kambi ya Upinzani alikuwepo Mheshimiwa John M. Cheyo.

Mheshimiwa Spika, muda wa mwisho wa kurudisha fomu za maombi ya uteuzi ilikuwa ni saa 10.00 jioni, Jumanne tarehe 12 Aprili, 2011. Muda huo ulipofika jumla ya Wabunge 13 walikuwa wamechukua fomu na kuzirejesha kama ifuatavyo:-

Kundi A, ni Wabunge wanawake na katika kundi hili kama Kanuni inavyoainisha anatakiwa Mbunge mmoja tu, waliorudisha fomu ni Mheshimiwa Dr. Mary Machuche Mwanjelwa pamoja na Mheshimiwa Bernadetha K. Mushashu.

Kundi B, ni Wabunge wa Zanzibar. Kundi hili pia anatakiwa Mbunge mmoja tu, lakini waliochukua na kurejesha fomu ni Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe na Mheshimiwa Hamad Yussuf Masauni.

Katika Wabunge wa Tanzania Bara kundi hili wanatakiwa Wabunge wawili tu, Waheshimiwa Wabunge waliojitokeza kuchukua fomu na kuzirejesha ni Mheshimiwa Stephen Julius Masele, Mheshimiwa Deogratias Aloys Ntukamazina, Mheshimiwa Dr. Hamis Andrea Kigwangalla, Mheshimiwa Faustine Ndungulile, lakini naomba nitoe taarifa ndani ya Bunge hili kwamba Mheshimiwa Faustine Ndungulile amejitoa na Mheshimiwa Joelson Luhaga Mpina.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, *ballot paper* nitakayoileta humu Bungeni itakuwa na majina manne na wala siyo matano kama ambavyo nilikuwa nimetoa tangazo langu jana baada ya kuwa nimefikia ukomo wa kupokea fomu za maombi.

Kundi D, ni Wabunge wa Upinzani na kundi hili linatakiwa kutoa Mbunge mmoja na Waheshimiwa Wabunge waliochukua na kurejesha fomu ni Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Moses J. Machali na Mheshimiwa Magalle J. Shubuda.

**SPIKA:** Mheshimiwa John M. Cheyo naye amejitoa!

**ND. JOHN N. JOEL – KATIBU MEZANI:** Sawa! Lakini pia kwa taarifa ambazo nimezipokea sasa hivi ni kwamba Mheshimiwa John M. Cheyo amejitoa kwa hiyo kwenye *ballot paper* tutakazozitoa, lile jina itabidi tuliondoe.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa nyongeza ya tano ya Kanuni za Bunge toleo la 2007 masharti na sifa za jumla zinazotakiwa kutimizwa na mgombea hadi kustahili kugombea na kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Afrika ni hizi zifuatazo:-

Moja, awe ni Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pili, awe amejaza kikamilifu fomu ya uteuzi akielezea pamoja na mambo mengine uzoefu wake wa kazi na uelewa wake kuhusu Bunge la Afrika. Tatu, awe na uwezo wa kuongea, kuandika na kusoma kwa ufasaha moja ya lugha rasmi za Bunge la Afrika ambazo kwa mujibu wa *Constitutive Act of the African Union* ya 2000 na *The Protocol to the Treat Establishing African Community Relating to the Pan African Parliament* ya mwaka 2000 pamoja na marekebisho yake, lugha hizo ni Kingereza, Kiswahili, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kispaniola. Nne, awe amedhaminiwa na Waheshimiwa Wabunge wasiopungua 10.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wangu nimeridhika kuwa Wagombea wote wametimiza vigezo hivi. Hata hivyo Bunge lako Tukufu nalo lina uwezo wa kuthibitisha sifa za Wagombea hawa hususan katika suala la C linalohusu lugha.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya tisa ya nyongeza ya tano ya Kanuni za Bunge, kila mgombea atapata fursa ya kujieleza mbele ya Waheshimiwa Wabunge na kujibu maswali kama yatakuwepo kwa idadi ambayo utaona inafaa. Baada ya Wagombea wa kundi moja kujieleza karatasi za kupigia kura kwa kundi husika zitatolewa ili Waheshimiwa Wabunge waweze kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha kwa kundi hili la Wagombea wa Uchaguzi wa Bunge la Afrika.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, tuliwatangazia Waheshimiwa Wabunge tarehe 6 Aprili, 2011 na kama *Order Paper* ya leo inaonyesha kuwa kutakuwa na uchaguzi mdogo wa kuziba nafasi za uwakilishi wetu katika *SADC Parliamentary Forum*.

Mheshimiwa Spika, nafasi zilizo wazi ni za kundi la Wanawake kuziba nafasi iliyoachwa wazi na Mheshimiwa Sophia Simba ambaye ameteuliwa kuwa Waziri, kundi la wanaume kuziba nafasi iliyoachwa wazi na Mheshimiwa Goodluck J. Ole-Medeye ambaye naye pia ameteuliwa kuwa Naibu Waziri. Hadi kufikia mwisho wa kurudisha fomu za uteuzi, Jumanne tarehe 12 Aprili saa 10.00 jioni ni Waheshimiwa Wabunge wawili tu waliokuwa wamejitokeza kuchukua fomu na kuzirejesha, nao ni Mheshimiwa Eng. Stellah M. Manyanya na Mheshimiwa Magalle John Shibuda.

Hata hivyo, nafasi katika kundi la wanaume imebaki wazi kufuatia uteuzi wa Mheshimiwa Goodluck J. Ole-Medeye ambaye kama nilivyoeleza hapo juu ameteuliwa kuwa Naibu Waziri, hivyo ni wazi kuwa nafasi hiyo inatakiwa kujazwa na Mbunge mwanaume kutoka Chama Tawala. Hata hivyo, kwa kuwa hakuna Mbunge wa aina hiyo aliyejitokeza kugombea nafasi hiyo na kwa kuwa kwa muda uliokuwa umebakari hadi kumalizika kwa Mkutano huu wa Tatu wa Bunge hautoshi kwa taarifa nyingine ya uchaguzi kutolewa, tunashauri kuwa Bunge hili Tukufu katika kikao cha leo lifanye uchaguzi katika kundi la wanawake tu na uchaguzi ule mwingine utatangazwa baadaye.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 8(2)(b) ya nyongeza ya pili, mgombea atapewa fursa ya kufika mbele ya wapiga kura, yaani Waheshimiwa Wabunge na kujieleza kwa lugha ya Kiingereza ambayo ndiyo inatumika na *SADC Parliamentary Forum*. Aidha, kama kutakuwa na maswali, Mgombea atajibu kwa idadi ambayo utakuwa umeelekeza. Kwa uzoefu, pia kwa mujibu wa utamaduni amba Bunge hili imejiwekea, inapokuwa amejitokeza Mgombea mmoja tu, Bunge bado linaweza kufanya maamuzi mengine ya kumpitisha bila kupingwa.

Mheshimiwa Spika, maeleo kuhusu uchaguzi wa *APRM*, kama nilivyatangazia, pia Waheshimiwa Wabunge tarehe 6 Aprili, 2011 na kama *Order Paper* inavyoonyesha pamoja na mambo mengine, leo kutakuwa na uchaguzi wa Mjumbe mmoja wa Baraza la Uongozi la Afrika, yaani *African Peer Review Mechanism* kutoka Chama Tawala. Hadi ulipofika muda wa mwisho wa kurejesha fomu, yaani tarehe 12 Aprili, saa 10.00 jioni siku ya Jumanne, ni mgombea mmoja tu aliyekuwa amejitokeza, naye ni Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla.

Uchaguzi huu unaendeshwa na masharti ya nyongeza ya pili ya nyongeza ya Bunge toleo la 2007 ambapo Kanuni ya 5(2)(c) ya nyongeza, hiyo inaelekeza kuwa endapo atajitokeza Mgombea mmoja wa nafasi inayohusika Wabunge watampigia kura ya ndiyo au hapana. Hata hivyo, Bunge hili Tukufu limejiwekea utaratibu kuwa inapotokea Mgombea akawa ni mmoja kwa nafasi moja, basi Mgombea huyo atapita bila kupingwa. Hivyo ni wajibu wa Bunge lenyewe kuamua utaratibu wa kufuata kama Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla apite bila kupingwa au apigiwe kura za ndiyo au hapana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofî*)

Kwa upande wa uchaguzi wa Wenyeviti namwuachia Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Uongozi aweze kulitolea maelezo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya saba ya Kanuni za Bunge toleo la 2007 pamoja na Spika na Naibu Spika, Bunge pia huongozwa na Wenyeviti watatu. Kanuni ya 11 inaelekeza kwamba Kamati ya Uongozi itapendekeza majina ya Wabunge sita kutoka mionganini mwa Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Bunge kwa kuzingatia jinsia na pande za Muungano, majina hayo huwasilishwa mbele ya Bunge ili yapigiwe kura.

Waheshimiwa Wabunge, Kamati ya Uongozi ilikutana jana Jumanne tarehe 12 Aprili, 2011 na kupendekeza majina yafuatayo:-

Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa George B. Simbachawene, Mheshimiwa Sylvester Massele, Mabumba halafu wakaona kwamba wasiendelee kubishana bila sababu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, kutokana na utamaduni uliojengeka katika Bunge letu, majina haya yanaletwa mbele yetu ili yathibitishwe. Naomba ieleweke pia kwamba Wenyeviti muda wao wa kuhudumia Bunge ni vikao kumi, miaka miwili na nusu, halafu tunachagua tena, lakini kwa nafasi ya Naibu Spika na Spika tunaendelea miaka mitano. Kwa hiyo, hayo ndiyo majina tuliyonayo.

Kwa hiyo, tutaomba ridhaa yenu.

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. RAYA IBRAHIM HAMIS:** Mwongozo wa Spika!

**SPIKA:** Mbonye hata sijamaliza hata kusema jamani? Mwongozo ni kwamba, mtu anatakiwa kumaliza kusema halafu ndipo mwongozo unaombwa.

Kwa hiyo, ninasema kwamba kwa utaratibu, haya majina Kamati ya Uongozi ilikutana na Makamu na Wenyeviti wakatafakari, wakapendekeza majina haya ambayo yana-*qualify* upande wa Muungano na jinsia na ni watatu.

Mheshimiwa Raya!

**MHE. RAYA IBRAHIM HAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 11(a), (b) na (c), Bunge letu tunaongozwa na Kanuni na Kanuni hii inatuambia kwamba, uchaguzi wa Wenyeviti wa Bunge utafanyika kwa kuzingatia jinsia na mapendekezo ya Muungano kwa kufuata utaratibu.

Kwamba (a) “Karatasi ya kura itakuwa na majina ya Wabunge sita ambao wamependekezwa na Kamati ya Uongozi kupigiwa kura kutoka mionganoni mwa Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge”.

Hivyo basi, kwa kuwa, Bunge letu linaongozwa na Kanuni, tunapendekeza kwamba kwa kuwa majina yanatakiwa kuwa sita na majina ambayo umeyataja ni matatu, tunaomba tuwekewe Wagombea sita ambao sisi ndiyo tutachagua watatu na watatu ambao hawatachaguliwa, na sivyo kama ambavyo mmetuwekea Wwagombea watatu kwa maana ya kuwa wanapiga bila kupingwa na sivyo taratibu na Kanuni zinavyosema.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, kwani fomu umeshaiona? Hujaiona! Kwa hiyo, umekwenda mbele...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, si umetaja majina?

**SPIKA:** Fomu ziko wapi? Kwa sababu kwa mujibu wa ...

**MBUNGE FULANI:** Umetaja majina matatu!

**SPIKA:** Tusibishane kwa mtindo huo. Katika kanuni zetu, hatubishani na Spika kwa mtindo huo. Kwa hiyo, tunaendelea. Sasa kwa maana ya kanuni yetu, tuna utaratibu pia. Kanuni ndivyo ilivyosema, lakini pia tuna utaratibu wa kwamba tunaweza kuamua kazi ya kukaa hapa Mezani, msidhani ni kubishana ila ni kazi nzito sana na Waheshimiwa walikuwa wamejadili na kufikiria kwamba tunafanyaje? Wakakubaliana kwamba jamani, sio kila mtu anaweza kukaa hapa, siyo rahisi hivyo. Ndiyo maana wao walifikia muafaka kwamba tunaomba tupendekeze kwa Bunge majina matatu tu. Mnaweza kupiga kura ya ndiyo au hapana kama mkitaka. Kwa hiyo, tuna maamuzi ya kufanya leo, lakini tutakapofika katika hatua inayohusika tutafanya uamuzi, kwa mfano, tumependezewa kama litakuwa jina moja kwa kuokoa muda, tunahitaji aje ajieleze kisha tupige kura ya ndiyo au hapana, lakini tutafanya maamuzi sisi wenyewe.

Halafu kukaa hapa, msidhani ni kazi rahisi kwamba mtu yejote anaweza kutoka huko akaja kukaa hapa. Sio rahisi hivyo! Kwa hiyo, ndiyo maana Kamati ya Uongozi

kwa kufikiria na kufikiria zaidi tena, siyo kwamba wameteuliwa kwamba wabakie hapo, wengine wote wanasema sisi hatuna ubavu, sasa tutaweka tu majina kwa sababu ya kuweka tu? (*Makofi*)

Kwa hiyo, tunaendelea na kazi inayofuata.

## T A A R I F A

**MHE. RAYA IBRAHIM HAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba mwongozo wako kama tunafuata Kanuni kama ilivyo, kwamba tunatakiwa tufuate Kanuni za Bunge ambazo zinatuongoza humu ndani, ama unatengua Kanuni inabidi utufahamishe kwamba Kanuni inatenguliwa ama tunafuata Kanuni kama ilivyoandikwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Shughuli za Bunge!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Kanuni inataka Wagombea wa nafasi hizi wawe na sifa moja tu. Awe Mwenyekiti wa Kamati au Makamu Mwenyekiti wa Kamati, hawa ndio wenye sifa ya kugombea. Lakini kwa ujumla wao wanaitwa Kamati ya Uongozi.

Mheshimiwa Spika, ulitumia busara jana ukawaita wote wenye sifa, maana sifa ya kugombea Uenyekiti ule siyo ya Wabunge wote. Uongozi umekutana nao, fomu zimetolewa na wito umetolewa, lakini wao wamekubaliana, yaani wale Wagombea wenye sifa kwamba Wagombea hawa watatu, hapa hoja anayoisema Mheshimiwa Mbunge hata ingetolewa leo yawezekana wale Wenyeviti na Makamu Wenyeviti hawatatokea wenye sifa wanaotaka kujaza fomu hizo, kwa sababu hili ni wazi kwa Wabunge wote.

Leo hapa tumeshuhudia kulikuwa na nafasi ya Mgombea wa SADC kwa Waheshimiwa akina mama, lakini timesikia hapa kwamba amegombea Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya peke yake. Wabunge akina mama hawapo? Kwa nini hawakugombea? Hili siyo jambo la kwanza. Mheshimiwa Stella M. Manyanya amegombea peke yake, lakini kwa nafasi ya Waheshimiwa Wabunge akina mama wote. Wabunge wanaostahili kugombea nafasi hizi wamekubaliana wenyeve kwamba Wagombee watu watatu na ndiyo majina matatu yamekuja, wale waliokuja wana sifa halali za kugombea.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, mimi binafsi ningewashauri na bahati mbaya sana Wenyeviti wote, Mmwakilishi wa Serikali alikuwepo, Kiongozi wa Upinzani Bungeni alikuwepo na Makamu wake walikuwepo kwa sababu nao ni Viongozi pamoja na Wenyeviti wengine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hii hoja mimi binafsi ningeshauri kwamba jambo hili lingeendelea tu.

**SPIKA:** Ni kweli hiyo Kanuni unayosema inasema Wagombea watatokana na Wenyeviti wa Kamati na Makamu wao. Sasa wote walikuwepo, wengine walifika wakasema sisi hatuna ubavu. Sasa mnataka tujaze tu majina wakati wenyewe wanasema hatuna ubavu? Ndivyo ilivyofikiwa. Wote walifika na walisema hatuna ubavu, wakateua majina wakasema sisi hatuwezi.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, tusiwe tunabishana *for sake of* kubishana. Nimesema wanaotakiwa kuchaguliwa ni Wenyeviti na Makamu wao na walikuwepo na wao ndiyo waliteua wenzao. Sasa ninyi mnataka tuwatoe wapi wengine? Anayetaka kujadili hapa aseme anawatoa wapi hao wengine.

**MHE. EZEKIA DIBOGO WENJE:** Mheshimiwa Spika, tunachosema hapa siyo *issue* ya Kamati ya Uongozi kwamba alikuwepo Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni. Tunachotafuta ni *the truth* kulingana na Kanuni za Bunge. Kwa hiyo, kama suala la makubaliano, ni kwamba hakuna makubaliano yanayofanyika kwenye *dark market* hapa, hapa vitu vyote vinafanyika kwenye *the light market*, hakuna *dark market* kwenye Bunge.

Kwa hiyo, haya masuala ya kutuambia kuna watu walikaa wakaelewana, hiyo walielewana kwenye *dark market* na kwenye Bunge hakuna *dark market*. Kwa hiyo, tunachosema ni kwamba ...

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, taarifa!

**SPIKA:** Ngoja amalizie kusema kwanza!

**MHE. EZEKIA DIBOGO WENJE:** Mheshimiwa Spika, tunachosema ni kwamba, tunahitaji kama Kanuni inasema kwamba Wagombea wanatakiwa wawe sita maana yake ni kwamba mnatakiwa mture fursa sisi Wabunge tunaopiga kura, yaani mture *room* ya kufanya *alternative choices*, ndiyo maana yake. Sasa mnapotuletea majina matatu tu hapa, hatukubaliani na hilo.

## T A A R I F A

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, Mbunge aliyemaliza kuongea, ameongea jambo kubwa sana. Anasema Kamati ya Uongozi ya Bunge ambayo wewe ni Mwenyekiti wake ni *dark market*. Hili ni jambo kubwa, hatuwezi kuliacha kwamba maamuzi yote tunayoyafanya ya Bunge, yote yanafanyika kwenye *dark market*. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Unapotosha.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Unaponiambia ni *dark market*, Mwenyekiti wa Kambi ya Upinzani yupo kwenye *dark market*, Wenyeviti wale watatu wako kwenye *dark market*, haiwezekani! (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, hebu endelea.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, tumekaa kwenye Kamati ya Uongozi na wao wakiwepo, tumekubaliana na hakuna aliyejitokeza, wamejitokeza watu watatu na watatu hao, pia demokrasi siyo lazima tushindane ni lazima tukubali huyu ana uwezo, huyu hana uwezo.

Mheshimiwa Spika, naomba tuendelee, tufanye uchaguzi. (*Makofî*)

**SPIKA:** Lakini kwanza kabisa...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, *narrow understanding* ya Mheshimiwa Serukamba...

**SPIKA:** Wote mkae chini, wote mkae chini.

**MBUNGE FULANI:** Kaa chini!

**MBUNGE FULANI:** Uwe na adabu, tuko Bungeni hatuko kwenye *club*...

**SPIKA:** Wote mkae chini na kila mtu anyamaze. Kwanza kabisa Mheshimiwa Mbunge, neno *dark market* naomba uliondoe. Kikao ninacho-chair mimi hakiwezi kuwa *dark market*, naomba uondoe kauli hiyo.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, ndiyo nasema kwamba...

**SPIKA:** Uondoe kauli. (*Kicheko*)

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, *narrow understanding* ya Mheshimiwa Mbunge aliyetoka kuongea.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, atoke nje huyo!

**MBUNGE FULANI:** Ondoa kauli wewe!

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, *order!* Tusikilizane.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, ninaposema *dark market* nilikuwa ninamaanisha kwamba ni maamuzi ambayo yanafanyika kinyume na kanuni zetu za Bunge zinavyotaka.

**MBUNGE FULANI:** Ondoa kauli.

**MBUNGE FULANI:** Akanywe kikombe cha babu huyo. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, nadhani umejizua kupita kiasi. Nafikiri ingekuwa wakati muafaka kutumia *Sergeant-At-Arms*. (*Makofi*)

## T A A R I F A

**MHE: HALIMA J. MDEE:** Taarifa.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika,...

**SPIKA:** Mtu anapopewa nafasi, mwacheni azungumze.

**MHE: HALIMA J. MDEE:** Amemaliza.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Amemaliza.

**SPIKA:** Eeh, kwa hiyo, tunatumia *Sergeant-At- Arms* anakwenda kuchukuliwa... Mheshimiwa Zitto.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba jana kwenye Kamati ya Uongozi tulikaa na kukubaliana kuhusiana na namna gani ambavyo uchaguzi huu utakwenda, lakini sio kweli kwamba kuna fomu ambazo zilitoka na watu wakajaza. Ilikuwa ni makubaliano mionganoni mwa Wenyeviti na ni kweli kabisa kwamba Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Naibu wake na Wenyeviti wengine amba wanatokea Kambi ya Upinzani walikuwa kwenye kikao hicho na ni dhahiri kwamba Kamati ya Uongozi wa Bunge siyo *dark market*, ni dhahiri kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pili, siyo sahihi kuchukua maneno ya Mheshimiwa Mbunge Wenje na kuyapa *narrow interpretation*... (*Makofi*)

Naomba nimalize. Siyo sahihi na wala siyo sahihi kwamba tunapofanya shughuli zetu za Bunge sasa tuanze kuchukua maamuzi ya kumwita *Sergeant-At-Arms* na kadhalika, lazima tuwe na ngozi ngumu, sisi ni wanasiasa tuweze kuepukana... (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Haiwezekani!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa maana hiyo naomba nimalizie kwamba utaratibu wa Wabunge walichokuwa wanaomba ni kwamba, Wabunge wawe na *choice*, waletewe majina zaidi ya nafasi zinazogombewa.

**WABUNGE:** *Out!*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Naomba nimalize, naomba nimalize.

**WABUNGE:** *Out!*

**SPIKA:** Tusikilizane, tusikilizane.

**MBUNGE FULANI:** Mnatuburuza!

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tulieni kwanza wenzetu wanaposema. Umemaliza?

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Ndio ninamalizia.

Mheshimiwa Spika, kama hakuna Mwenyekiti mwingine yejote au Makamu Mwenyekiti mwingine yejote ambaye ana nia ya kugombea, uchaguzi uendelee wala haina ugomvi. Jambo la msingi la kuzingatia ni kwamba Kanuni zetu zime-*provide* kwamba karatasi ya kura itakuwa na majina sita, kwa hiyo, katika hali ya kawaida ni kumwomba Mbunge mmoja au Waziri mwenye dhamana na masuala ya Bunge *a-move a motion* kusema rasmi kwamba hapakuwa na majina hayo sita, kuna majina matatu ili uchaguzi uweze kuendelea.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, hoja ya msingi ya Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis ni kwamba, tukienda kwenye uchaguzi bila kuzingatia kipengele cha Kanuni tutakuwa tunavunja Kanuni ambazo tumezitunga sisi wenyewe na ni lazima tuendeshwe na Kanuni zetu za Bunge. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tatizo lenu mnakuwa mmejipanga huko nini cha kusema hapa Bungeni hata bila kuangalia taratibu. Nimewambia Mheshimiwa Raya amewahi kabla hatujafika tulipofika. Nimewambia hivyo! Fomu ya majina matatu mmeipata wapi? Mnayo hapa? Ndiyo nimewambia mnawahi mno kabla ya kufikia *stage* tuliyofikia. Ningekuwa mimi nimewagawia fomu mkakuta hayo majina yapo matatu tu Mheshimiwa Raya angesimama na kusema mbona Kanuni inasema hivi?

Mimi nimetao taarifa tu, lakini sikuingia kwenye kifungu cha 11 kinachohusu kupiga kura. Nimetao taarifa kama walivyotoa taarifa wengine kwamba wamejiondoa, wengine wamafanya nini, lakini nikawaambia katika fomu mtakuja kuona. Ninyi wenyewe mnawahisha shughuli za Spika. Sasa tunaendelea. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunakwenda kwa utaratibu unaofuata. Sasa tunaanza uchaguzi.

**WABUNGE:** Mheshimiwa Spika, atoke nje, atoke nje, atoke nje!

**MBUNGE FULANI:** Mnatuburuza.

## T A A R I F A

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa gani?

**MBUNGE FULANI:** *Black market.*

**SPIKA:** Mheshimiwa Wenje hajafuta kauli kwamba sisi tunavyofanya siyo *black market*.

**WABUNGE:** Atoke nje! Atoke nje! Atoke nje!

**SPIKA:** Mheshimiwa Wenje, tunaomba ufute kauli. Ni utaratibu tu, huwezi kumtukana Spika na watu wake wote halafu ubakie wewe tu.

**MBUNGE FULANI:** Atoke nje, *out*.

**SPIKA:** Atafuta kauli, ni kawaida tu.

**WABUNGE FULANI:** *Out, out!*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, msikilizeni. Mheshimiwa Wenje nimekuPA nafasi!

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba ...

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muwe mnamsikiliza mwenzenu anaposema.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, *in real sense* sikusema kwamba Kamati yako ni *dark market*, ila nilisema kwamba *the process* iliyofanyika ndio ilikuwa *dark market*, sikusema kwamba Kamati yako ni *dark market*.

**MBUNGE FULANI:** *Hansard* si ipo!

**SPIKA:** Hapana, Mheshimiwa Mbunge sisi wote ni watu wazima, tulikaa kwenye *Board Room* ya Spika na Wenyeviti wote walikuwepo na Makamu wote walikuwepo, hiyo *dark market* ilikuwa wapi na *process* hiyo?

**WABUNGE:** Atoke nje! *Out!*

**MHE. KWABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Wenje apewe muda wa kuzungumza amalize.

**SPIKA:** Na ndicho hicho ...

**MBUNGE FULANI:** Atoke nje huyo!

**MHE. KWABWE Z. ZITTO:** Hawezi kutoka nje na hamna mamlaka ya kumtoa nje.

**WABUNGE:** Atoke nje! Atatoka huyo!

**MBUNGE FULANI:** Hatoki mtu.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Zitto, tunaku heshimu, atoke nje.

**MBUNGE FULANI:** Afute usemi, kama hafuti atoke nje.

**MBUNGE FULANI:** Hili ni Bunge siyo *Club*.

**MBUNGE FULANI:** Hatoki mtu hapa, la sivyo tunatoka wote.

**MBUNGE FULANI:** Tutatoka wote.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae chini.

**MBUNGE FULANI:** Hatoki mtu, msitake kutuburuza! Wanatuburuza bwana!

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane. Naomba mkae kimya tusikilizane.

**MBUNGE FULANI:** Mnatuburuza bwana!

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wote, tusikilizane. Naomba wote mkae kimya tusikilizane.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Naomba wote mkae chini, hakuna cha mwongozo hapa.

**MBUNGE FULANI:** Tufunge mlango tupigane.

**MBUNGE FULANI:** Vijana hao!

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, haiwasaidii kitu chochote na wananchi wanaowaoneni hapa wanaona kama mnafanya mchezo usiokuwa na biashara yoyote ya maana. (*Makofî*)

**MBUNGE FULANI:** Hao CCM hao!

**MBUNGE FULANI:** CHADEMA hamna adabu!

**SPIKA:** Spendi kusikia mtu anazungumza hapa, sasa wote mtaambiwa kutoka na mtasimamisha Bunge kwa ajili ya upuuzi.

**MBUNGE FULANI:** Msitumie wingi wenu kutuburuza.

**SPIKA:** Naomba mnyamaze. Waheshimiwa Wabunge, tunafanya mambo ya kijinga, Mheshimiwa Wenje maneno aliyotumia sio maneno ya mtu ambaye anawajibika. *Dark process, whether process or what*, siyo sahihi. Waheshimiwa tuheshimiane. Akisema anaondoa maneno haya itamgharimu shilingi ngapi?

Mheshimiwa Wenje itakugharimu shilingi ngapi? Kiongozi wa Upinzani itakugharimu shilingi ngapi ukisema nina-withdraw maneno hayo? Itakugharimu shilingi ngapi?

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, naomba ni-withdraw maneno ya *dark market* niseme *white market*. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mnajua hili Bunge watu wote wanawaona. Nchi nzima inawaona mlivyokuwa, watu mmechaguliwa kwa heshima zenu, kwanini mnafanya fujo isiyokuwa na akili jamani? Aah!

Tunaendelea na hatua inayofuata. Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi ...

**MBUNGE FULANI:** Taarifa!

**SPIKA:** Hakuna taarifa saa hizi, tunaendelea na uchaguzi. Mheshimiwa Waziri wa Nchi tunaomba utoe hoja ya ku-suspend kifungu cha 11 ili kusudi haya majina matatu yakubalike.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kama ulivyotoa taarifa hapa Bungeni kwamba tunaingia kwenye uchaguzi, naomba Bunge lako Tukufu likubali kutengua kifungu cha 11 (1) (a), (b) na (c) kwa kuzingatia kwamba majina yanayokuja ni matatu na siyo sita kama yalivyoolezwa kwenye kifungu cha Kanuni, na Bunge lako Tukufu naomba likubali kutengua kanuni hii ili uchaguzi huu uweze kufanyika. Naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)  
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Hoja ya Kutengua Kifungu cha 11 (1) (a), (b) na (c )*  
*cha Kanuni za Bunge ilipitishwa na Bunge*)

## **UCHAGUZI WA WABUNGE WA BUNGE LA AFRIKA**

**ND. JOHN N. JOEL – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu huo tutaanza na uchaguzi wa *Pan African Parliament* ambao kimsingi ndiyo una Wagombea ambao wanatakiwa wapigiwe kura halafu kwa hizi nyingine tutazileta ili kusudi muweze kufanya maamuzi baadaye.

Tutaanza na uchaguzi wa Bunge la Afrika, na kama nilivyotoa taarifa tuna makundi manne. Kundi A ni wanawake nafasi moja, Kundi B ni nafasi moja, kutoka Wabunge wa Zanzibar, Kundi C ni Bara nafasi mbili na kundi D ni Mbunge kutoka upande wa Upinzani nafasi moja.

Mheshimiwa Spika, sasa nitawataja Wagombea majina ikiwezekana uwaruhusu watoke ili warudi kwa utaratibu ule ambao tutakuwa tumekubaliana.

Wagombea wa Kundi A ni Mheshimiwa Dr. Mary M. Mwanjelwa pamoja na Mheshimiwa Bernadetha K. Mushashu.

**SPIKA:** Waheshimiwa walijotajwa tunaomba watoke. Mheshimiwa Bernadetha hajatoka. Sasa Mheshimiwa Mwanjelwa bakia na Mheshimiwa Bernadetha uende nje. Tumeshauriana hapa, tunafikiria wale Waheshimiwa wote wanaogombea hiki Kiti watoke nje kwa sababu inawezekana mkauliza maswali akajua majibu kutohana na mwenzake alivyoulizwa. Kwa hiyo, ninaomba uwataje wote ambao wanapaswa kutoka nje.

**MBUNGE FULANI:** Kifaransa au Kiswahili?

**ND. JOHN N. JOEL – KATIBU MEZANI:** Pamoja na niliowataja mwanzo, Wagombea wengine ni Mheshimiwa Kidawa Hamad Saleh.

**SPIKA:** Waheshimiwa mmatoka nje, hata Mheshimiwa Mwanjelwa toka nje.

**ND. JOHN N. JOEL – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Hamad Yussuf Masauni, Mheshimiwa Stephen J. Masele, Mheshimiwa Deogratias Ntukamazina, Mheshimiwa Dr. Hamisi A. Kingwangala, Mheshimiwa Luhaga J. Mpina, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Moses J. Machali na Mheshimiwa Magale J. Shibuda. Hawa ndio Wagombea wa Bunge la Afrika.

**SPIKA:** Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tunaanza na kundi la kwanza, Kundi A. Katika kundi hili anatakiwa Mbunge mmoja. Kwa hiyo, tunamwita Mheshimiwa Dr. Mary.

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika.

**MHE.ANNA M. ABDALLAH:** Mwongozo wa Spika. Tungependa kujua waulizwe maswali mangapi pengine tungeamua kabla hawajaingia.

**SPIKA:** Eeh, kwa kawaida tunauliza maswali matatu na muda wa kujieleza ni dakika tatu. Kujieleza ni dakika tatu na maswali ni matatu kama yapo. Tunakubaliana na hilo Waheshimiwa Wabunge?

**WABUNGE:** Ndiyo!

**SPIKA:** Kama kuna mtu anataka Mwongozo aseme sasa hivi. Tusiingize katikati Miongozo, Taarifa, nini, itakuwa ni vurugu tupu, anayetaka kupata maelezo apate sasa hivi.

**MBUNGE FULANI:** Lugha!

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mheshimiwa...

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Zainab Kawawa.

**SPIKA:** Zainab Kawawa yuko wapi? (*Kicheko*)

**MBUNGE FULANI:** Simama.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Nimesimama, ahsanteni. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua watatumia lugha gani kwa sababu hii ni *International Organisation?*

**SPIKA:** Eeh, Msimamizi wa Uchaguzi!

**ND. JOHN N. JOEL – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Spika, nilizitaja lugha ambazo zinakubalika katika Bunge la Afrika. Kwa mujibu wa ile Sheria na Itifaki, lugha ambazo zinakubaliwa kule ni Kingereza, Kiswahili, Kifaransa, Kiarabu, Kireno na Kispanyola. Nilizitaja.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika!

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Jamani, hebu kaeni chini. Mbona mna haraka? Mpeni mtu heshima kwanza. Eeh, endelea.

**ND. JOHN N. JOEL – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Spika, ni busara Bunge lako kuamua ni lugha gani ambayo mtapendelea kuitumia.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika!

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mwongozo!

**SPIKA:** Nilimwona Makongoro, alisimama. Ameondoka! Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa taarifa yako ya kuniruhusu kwa Mwongozo. Chaguzi zetu zinaendeshwa kwa Kanuni na Kanuni zetu zimetoa taratibu za kila chaguzi. Anachokisema Msimamizi wa Uchaguzi anapotosha na wala hafuati Kanuni. (*Makofi*)

Kuhusiana na uchaguzi wa Wabunge wa kutuwakilisha Bunge la Afrika, iko kwenye ukurasa wa 112, nyongeza ya tano, *election procedures* zimeelezwa kwenye Part IV na kipengele cha tisa kimeeleza *cartegologically* lugha wanayotakiwa kutumia ni Kingereza. Sasa naomba aliweke hili sawa asitoe tafsiri anazotaka kuzitoa yeye, tufanye uchaguzi tumalize au tutengue kama ambavyo tumezoea kutenguatengua pale tunapobanwa. (*Kicheko/Makofi*)

**SPIKA:** Msimamizi wa Uchaguzi.

**MR. JOHN N. JOEL – TABLE OFFICER:** Mheshimiwa Spika, naomba nisome kipengele hicho, ni Nyongeza ya Tano, Part II ni Section ya tatu ‘qualifications of candidate’ naomba niisome kwa kingereza;

*“No person shall be qualified to be a candidate for election to the PAN African Parliament unless he or she is a Member of Parliament of the United Republic of Tanzania, and is fluent in any of the languages approved for use in the proceedings of the Pan African Parliament”. (Applause)*

## TAARIFA

**SPIKA:** Taratibu kwa nini mna haraka sana. Hapa tulikuwa tunaongea na Halima Mdee, Halima Mdee unasemaje?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, sheria haisomwi kwa vipande vipande. Sheria inasomwa kwa ujumla wake. Part IV ya huo mchakato wa Uchaguzi wa Bunge la Afrika, imeelezea *Election procedures*.

**SPIKA:** Soma bwana wewe kwa nini useme tu.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** *Part IV, Fasili ya 9 inasema hivi: “Before the voting exercise takes place on election day, each candidate shall be given an opportunity to appear before the voters assembled in an ordinary sitting of the National Assembly and address them in English....”.* (Applause)

Kama mtu hajui Kiingereza leo ndio tutampatia hapa. (*Makofi/Kicheko*)

## TAARIFA

**SPIKA:** Nani mwingine alikuwa anatoa taarifa?

**MHE. JANUARY Y. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kazi ya Ubunge nilikuwa nafanya kazi Ofisi ya Rais, Ikulu na kabla ya hapo nilikuwa nafanya kazi Wizara ya Mambo ya Nje. Katika kazi kubwa tuliyofanya kama nchi ni kuhakikisha kwamba Kiswahili kinakuwa lugha rasmi.

**MBUNGE FULANI:** Ahaa!!! Acha wewe?

**MHE. JANUARY F. MAKAMBA:** Kiswahili inakuwa lugha rasmi ya Umoja wa Afrika. Tulitumia pesa zetu kama nchi Kiswahili kiingie kama Lugha Rasmi ya Umoja wa Afrika. Kiswahili kinatumika kwenye Bunge la Afrika. Sasa mimi nawashangaa wenzangu hapa kwamba Kiswahili ni fahari ya Mtanzania na tumehakikisha kwamba inatumika kwenye Umoja wa Afrika kwa kushinda Upinzani mkubwa uliokuwepo. Sasa nashangaa hapa kuna Upinzani kwa Wabunge tunaowapeleka kwenye Bunge la Afrika kwamba lazima wajue Kiingereza kana kwamba Kiswahili sio lugha. Kwa hiyo pamoja na kanuni nadhani ebu tuwe na fahari ya nchi yetu na tujiheshimu kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilitaka kutoa tu hiyo taarifa kama wenzetu hawajui kwamba Kiswahili kinatumika kwenye Bunge la Afrika, basi leo wajue.

**SPIKA:** Kwanza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kutokana na uzoefu wa Bunge hili katika kuwahoji wanaokwenda kutuwakilisha kwenye Mabunge haya kama Bunge la Afrika tuliwahoji kwa Kiingereza na walijieleza kwa Kiingereza. (*Makofi*)

Pili, kama Toleo la Kanuni namba 2 la mwaka 2007 bado inatumika aliyojasema Mheshimiwa Mbunge wa Kambi ya Upinzani ni sahihi kabisa. Lakini pia kwamba

Kiswahili ni lugha ya Taifa na tunaipa heshima huko duniani ni kweli, lakini katika *representations* hizi kuna lugha ya ndani kwenye Bunge la Afrika na *informal* kule nje, kwa hiyo watu wetu lazima wajue lugha ya Kiingereza na kwa kufanya hivyo wala hatudharau kabisa lugha ya Kiswahili ambayo tunajifanya sisi wenyewe. (*Makofî*)

Kama Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje, naomba tu niseme kwa hili ni vizuri twende na utamaduni wetu, tulifanya hivyo wakati uliopita, kama kuna kufanya jambo lingine tulifanye, lakini kwa sasa hivi ubishi uishe twendeni tuwahoji kwa lugha ya Kiingereza kama tulivyofanya miaka minne iliyopita.

**MBUNGE FULANI:** Tungeacha kuchangia!!!!

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge *Part II, qualification of a candidate* ni kwamba huyo tunayemchagua sisi angalau awe *fluent* katika lugha mojawapo. Kifungu anachosema Mdee ni *procedure* ya kumchagua, kwa hiyo tutatumia Lugha ya Kiingereza. Ndiyo hivyo.

**MBUNGE FULANI:** Hao wote wanajua.

**SPIKA:** Haya tunaanza, kwani nyie mnafikiri hawajui Kiingereza, wanajua. (*Makofî/Kicheko*)

Kwa hiyo, tunaanza na *the first candidate out of the two*.

**SPEAKER:** Dr. Mary Machuche Mwanjelwa, *you are here before the National Assembly and you are required to explain yourself at the time which is not more than three minutes and if there is any question we shall ask you three questions if there are any. So you can start three minutes.*

**MHE DR. MARY M. MWANJELWA:** *Thanks Madam Chair, your right-hand Prime Minister, Leader of the Opposition, Ministers and Honourable Members of this Parliament; my name is Doctor Mary Mwanjelwa, I here by humbly requesting you to vote for me so as to represent this Parliament and this country as a whole to the Pan African Parliament.*

*I have been involved in so many international relations and community development as well as human rights and community development as I said. As you all know my colleagues this position requires to do lots of research, consultation as well as networking and I believe that I am fit for this position. (Applause)*

*Please, I plead with you my dear colleagues to have a trust on me and I can met, I will represent you fully to the benefit of this country as well as to the benefit of this Parliament of the Republic of Tanzania. Thank you very much. (Applause)*

**SPEAKER:** *We have three questions to be asked to you. Honourable Tundu Lissu.*

**HON. TUNDU A. M. LISSU:** *Madam Speaker, I would like to ask the candidate the following very brief question:-*

*Honourable Candidate, I have read your brief biographical sketch in which you refer yourself as a Doctor. Now, I would like to know, whether this Doctorate is a Doctorate of Medicine, is a Ph.D or it is an Honorary Doctorate and if it is a Ph.D I would like to know which University conferred to you this high distinction? Thank you.*

**SPEAKER:** *Dr. Mary Mwanjelwa can you explain this?*

**HON. DR. MARY M. MWANJELWA:** *Thank your Honourable Tundu Lissu for your valid and valuable question.*

*The Doctorate I have is an Honorary Doctorate. Thank you.*

**HON. KABWE Z. ZITTO:** *Honourable Speaker, I would like to pose a question to the candidate. For the previous eight to ten weeks, there has been an invasion of an African country by western powers, that is Libya and the African Union has been trying to resolve the crisis; our country has been silent on that. When you become a Member of Pan African Parliament will you bring a motion to condemn the bombardment of the African country by western powers? (Applause)*

**SPEAKER:** *Honourable Mary Mwanjelwa.*

**HON. DR. MARY M. MWANJELWA:** *Thank you Honourable Kabwe Zitto for your valid and valuable question.*

*As you know Pan African Parliament it's a board that has got fully legislative power and according to your question Pan African Parliament condemns all the violence happening in Libya because it believes in a very peaceful dialogue. And me if at all and I expect and believe that you are going to vote for me today, I will make sure that Tanzania as a country having a representative in that Parliament to make sure that will be having a very peaceful dialogue towards this Libya situation. Thank you. (Applause)*

**SPEAKER:** *We have only one question remaining, the third question. So it is enough.*

**AN HONOURABLE:** *No!*

**SPEAKER:** *Hon. Dr. Mary M. Mwanjelwa, now you can ask for votes.*

**HON. DR. MARY M. MWANJELWA:** *Madam Speaker, thank you for giving me this opportunity again. Your right-hand Prime Minister, Ministers, Leader of the Opposition, My fellow colleagues, Member of this esteemed Parliament, I kindly request you to have a very fruitfully trust on me that I will never let you down. I will be a very*

*competent representative to the Pan African Parliament to represent this Republic Parliament so that I can really and truly represent this country accordingly. And after having said this, I humbly request all of you to vote for me. Thank you very much.*

**SPEAKER:** *Thank you, ohoo! One of the conditions you are not supposed to clap or to do anything, you see. So let us call another candidate Honourable Benardetha Kasabago Mushashu.*

*Honourable Benardetha Kasabago Mushashu, you are given three minutes to explain yourself and then after that you will be given three questions if any.*

**HON. BENARDETHA K. MUSHASHU:** *Thank you Honourable Madam Speaker, Honourable Prime Minister, Honourable Leader of Opposition, Honourable Members of Parliament; my name is Hon. Benardetha K. Mushashu. I am a Member of Parliament Special Seats. Professionally, I am a Teacher I taught for many years and then headed Secondary Schools for more than ten years. I have been in the Parliament since the year 2005, so this is my second term in Parliament. I used the first term to learn what Parliamentary activities are all about. So I feel that I am ripe to be able to represent you. (Applause)*

*Honourable Members of Parliament, I humbly stand before you to request you to vote for me, so that I can represent you on this Pan African Parliament. I have decided to contest for this position because I feel that I am adequately qualified to represent you in this capacity.*

*Honourable Speaker, I am saying so because educationally I hold a Masters Degree and secondly, the experience accrued both in the Parliament and outside over years necessitates me to stand here confidently and say, Yes I can represent you. (Applause)*

*Madam Speaker, I have attended a lot of trainings at national, regional, continental level and internationally and my C.V. has been issued to you earlier on, I am sure it is on your table. I was among those who attended the CWP in Accra Ghana and we passed the fifty fifty resolution. I was involved in the fine tuning of the SADC gender Protocol in Johannesburg. I also was invited to Kenya Parliament when they were passing the Sexual Offences Bill, I was also invited to Sweden Parliament, and I went to the United Kingdom Parliament. So this gave me another chance to study what Parliaments are all about.*

*Lastly, I also attended this same Pan African Parliament, I was invited, I stayed there for seven days and I also attended the Inaugural Ceremony which was officiated by His Excellency the President of the United Republic of Tanzania the then Chairman of AU. So, I feel that I am well qualified to represent you. Kindly vote for Honourable Benardetha K. Mushashu. So that, I will become your representative on this Pan African Parliament.*

*Honourable Members of Parliaments, please vote for me.*

**SPEAKER:** Rev. Msigwa

**REV. PETER S. MSIGWA:** *Thank you very much Madam Speaker.*

*Honourable Benardetha, could you please tell me the main objective of the Pan African Parliament?*

**HON. BENARDETHA K. MUSHASHU:** *The main objective of Pan African Parliament is to make sure that we do certain things to make sure that, we promote integration to enable us reach an ultimate integration of Africa, we get one Government and the United States of Africa.*

*But there are objectives such as promoting peace and security in the country, promoting regional economic communities and staff like that. But the ultimate aim is to make sure that we have one government and the United States of Africa.*

**SPEAKER:** *The second questions Honourable Leticia Nyerere.*

**HON. LETICIA M. NYERERE:** *Thank you very much Madam Speaker for giving me an opportunity to ask the candidate some questions as follows.*

**SPEAKER:** *Any question, but one question.*

**HON. LETICIA M. NYERERE:** *Okay! That's fine.*

*Honourable Mushashu you have told us about your profession, your qualifications and everything about your academic skills. Could you please tell me something about what you think about accountability and credibility?*

**HON. BENARDETHA K. MUSHASHU:** *Okay. Thank you very much for a very good question. What I feel like and it is also another objective of the Pan African Parliament that our governments should adhere to human rights, democracy, accountability and the rule of law. So, I feel that all government should adhere to that.*

**SPEAKER:** *Thank you. Honourable Serukamba.*

**HON. PETER J. SERUKAMBA:** *Thank you Madam Speaker, I have one question to Madam Mushashu.*

*I would like to know, I know as you told earlier on that, all the functions and the role of Pan African Parliament, what are the challenges you think are facing this Parliament?*

**HON. BENARDETHA K. MUSHASHU:** *Thank you. Honourable Members of Parliament, when Pan African Parliament was started it was aimed to be a Legislative Body. Up to now it is just a Consultative Body; it is not yet a Legislative Body. So that is one of the challenges because most of the recommendations they are making are not binding.*

**SPEAKER:** *Honourable Mushashu you have answered the three questions and you can now ask for votes.*

**HON. BENARDETHA K. MUSHASHU** *Thank you Madam Speaker. Honourable Members of Parliament, please vote for me because I assure you if you vote for me I will try my level best to offer you the best. (Applause)*

**SPEAKER:** *Thank you very much. So we have agreed that after we interview the group, then we vote, so that we go to another group. If we interview the whole list we may forget the other names. So, we are going to give the ballot papers now, so that we vote for these two and then we continue with the other group. Can you have some ballot papers please?*

Mnataka Kiingereza si hicho hapo. (*Makofi/Kicheko*)

(*Hapa karatasi za kupigia kura ziligawanywa  
kwa Waheshimiwa Wabunge*)

**SPIKA:** Piga kengele kusudi walioko nje warudi ili wahesabiwe. Naomba tuwe na utulivu, heshima zetu ni za lazima jamani. Msimamizi wa uchaguzi fanya haraka.

(*Hapa masanduku ya kupigia kura yalioneshwa  
kwa Waheshimiwa Wabunge*)

(*Hapa kura zilipigwa na kukusanywa*)

**SPIKA:** Msimamizi wa uchaguzi kwa hatua inayofuata.

**NDG. JOHN JOEL- KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Spika, kundi linalofuata ni kundi la Wabunge wa Zanzibar, tunaanza kumhoji Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe. *Honourable Kidawa Hamid Salehe you are given three minutes to explain about yourself and why you are decided to stand for this seat before this August Assembly and you will have three questions to answer, if there are any.*

**HON. KIDAWA HAMID SALEHE:** *Honourable Speaker, Madam Anne Makinda, the right Honourable Prime Minister Mizengo Pinda, my colleagues Honourable Members of Parliament; my name is Kidawa Salehe, a Member of*

*Parliament Special Seat coming from North Region of Unguja. My profession; I am an Economist, I am a Holder of a Master Degree in Economics and also Diploma in Fiscal studies. I am standing before you today this morning for only one purpose to request for your vote to enable me be a member of Pan-African House. I have gained enough experience and knowledge which enable me be a good representative of this Parliament to Pan-African House. Please Honourable Members of Parliament vote for me, I am begging you, thank you very much.*

**SPIKA:** *First question Hon. January Makamba.*

**MHE. JANUARY Y. MAKAMBA:** *Thank you Madam Speaker. I want to pose one question to the candidate. In 2004 African Heads of States adopted Swahili as one of the official languages of the African Union; and in his formal addresses, President Jakaya Kikwete has used Kiswahili to address the AU summit and even President Chissano once used Kiswahili. I want to ask you, will you follow their example in using Kiswahili as you deliberate in the Pan-African Parliament? Thank you.*

**MHE. KIDAWA HAMID SALEHE:** *Thank you very much for a good question. The answer is yes because Kiswahili is my mother tongue as well as my national language. So I will be very proud to use Kiswahili not only in PAP but in every institution allowed to use Kiswahili.*

**SPIKA:** *Second question, Honourable Wenje.*

**MHE. EZEKIA K. WENJE:** *Thank you Madam Speaker, I just want to know from Honourable candidate; I believe from the time you decided to contest you had a packing order and I want to know from your packing order what will be your priorities when shall we give you this opportunity to represent us in Pan-African Parliament?*

**MHE. KIDAWA HAMID SALEHE:** *I don't think that I got well the question but regarding to my priorities what I am going to do in the Parliament depending upon the objective of the Parliament; as Member of Parliament I will go through all the objective and policies of Parliament. So together with other as Members of Parliament we are going to follow what we have decided in the protocol as well as proceedings of the Parliament. (Applause)*

**SPIKA:** *Honourable Mtinda.*

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** *Thank you Honourable Speaker. Honourable Kidawa, as a Tanzanian woman; what specific issues are you going to present in the PAP concerning women in Tanzania?*

**MHE. KIDAWA HAMID SALEHE:** *Thank you Honourable Christowaja. As a woman, I believe that gender issue is of utmost important. But peace, tranquillity and stability will be one among the very most important because I know the importance of living in peaceful country. Thank you very much. (Applause)*

**SPEAKER:** *Thank you very much. The three questions has been answered, now you are given chance to ask for vote.*

**MHE. KIDAWA HAMID SALEHE:** *Thank you very much Honourable Speaker. My colleagues Honourable Members of Parliament, please do vote for me. Vote for me because I am capable and able to work for you and represent you in the House, please I am begging you. (Applause)*

**SPEAKER:** *Thank you very much, we wish you all the best and now I call Honourable Hamad Masauni. Honourable Masauni you are given three minutes to explain yourself why you have decided to stand for this position before this August Assembly and then you will be asked three questions if there any.*

**MHE. HAMAD YUSSUF MASAUNI:** *Thank you Madam Speaker. Honourable Madam Speaker, Honourable Prime Minister, Honourable Leader of the Opposition and Honourable Members of Parliament; my name is Engineer Hamad Masauni, I am Member of Parliament of Kikwajuni Constituency in Zanzibar.*

*Honourable Speaker and Honourable Members of Parliament, with great honour, I stand before you seeking for your votes to serve my country, to represent my country through Pan-African Parliament representation.*

*Honourable Speaker and Honourable fellow Members of Parliament, given this opportunity I will vigorously effectively and efficiently represent my country in this position. I strongly believe that, we will share our vision and commitments toward United Africa through encouraging African countries to integrate under the framework of the establishment of the African Union. I am confident that if I am elected today I will also use this opportunity to bring back home experiences and expertise that required to actually support the merging social, economic, divine of this country.*

*Honourable Speaker, Honourable Leader for Opposition and fellow Members of Parliament from parties present here today with great honour again please vote for me. As you believe, I am able, capable and I am also determined to serve you and to serve my country in particular and to serve my continent as a whole. Thank you for your attention. (Applause)*

**SPEAKER:** *Thank you and you have three questions, first question from Honourable Zitto Kabwe.*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** *Madam Speaker, I have one question to the candidate. Africa is under attack, imperialist powers are now trying to top up an African Heads of States and African Union is ignored. What is your view on this?*

**HON. HAMAD YUSSUF MASAUNI:** *Thank you Madam Speaker. As you all may know, one of the objectives of this organ is actually to promote peace, security and*

*stability for our Continent. So, if I am elected, I will push this agenda as you may know also that the objective of the African Union is to support our African Brothers from other countries who are in conflicts, to actually use peaceful means to solve their problems. (Applause)*

*Madam Speaker, so being one of the Members of Parliament representing the countries, I share the same mission that my country has in terms of ensuring that there is peace and stability in this Continent and therefore improving our economy and livelihood and reducing poverty of the people of African Continent. (Applause)*

**HON. ESTHER A. BULAYA:** *Thank you Madam Speaker for giving me a chance to ask a simple question. Honourable candidate, can you tell us when was the Pan African Parliament Established?*

**HON. HAMAD YUSSUF MASAUNI:** *Honourable Speaker, the Pan African Parliament was established in March, 2004 under the Article 17 of Constitutive Act. The idea of establishing this organ is to have an informed decision from the vision of our African Leaders. The idea is actually to involve African people, to get them involved in decision making and discussion on the matters, challenges and problems that are facing our Continent. (Applause)*

**HON. ZAINAB R. KAWAWA:** *Thank you Madam Speaker. I'm impressed with Honourable Masauni, honestly. Could you tell us what is your level of education, please? (Applause/Laughter)*

**HON. HAMAD YUSSUF MASAUNI:** *Honourable Madam Speaker, first of all, thanks to Honourable Zainab Kawawa for her trust on me. I believe this trust is also among all Members of Parliament who are present here today. Just a brief about my education: by profession I'm an Engineer, I have earned a Bachelor Degree in Engineering (Electrical and Electronic Engineering). But, also I have a Masters Degree in Economics and Environmental Technology. (Applause)*

*Honourable Speaker, also I have attended plenty of International programmes, so I have got a lot of certificates; it's difficult to mention all of them here. Thank you. (Applause)*

**SPEAKER:** *You have already answered the three questions, now you are given time to ask for votes. You can ask for votes if you want to. (Laughter)*

**HON. HAMAD YUSSUF MASAUNI:** *Honourable Madam Speaker, thank you. Honourable Prime Minister, Honourable Leader of Opposition, Honourable Members of Parliament from CCM, Members of Parliament from CHADEMA, from CUF, from NCCR-Mageuzi, from UDP, from TLP, please I need your votes. I need your votes to serve Africa, Africa needs me, I need Africa. Thank you so much. (Applause)*

**SPEAKER:** *Thank you very much. Now you can take your seat. As we have done before, we shall also vote this group before we continue to other groups. (Applause)*

*(Voting in Progress)*

**SPEAKER:** *Before we continue to the next stage, can we have the Minister of State to move a motion, so that we can extend this exercise until when we finish. Inabidi tufanye hivyo kwa sababu hatuwezi kupiga kura tukaondoka. Tufanye zoezi mpaka tutakapomaliza beyond saa 7.00.*

## **HOJA YA KUTENGUA KANUNI**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naomba Bunge lako Tukufu likubali kutengua Kanuni ya 28 hadi hapo kazi hii iliyo mbele yetu iweze kukamilika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:**  
Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Tunaendelea na uchaguzi huu, sasa tunaingia Kundi IC.

**NDG. JOHN JOEL – MSIMAMIZI WA UCHAGUZI:** Kundi la Tatu ambalo ni Kundi C, Wabunge wa Tanzania Bara na wagombea wako wanne: Mheshimiwa Stephen J. Masele, Mheshimiwa Deogratius Ntukamazima, Mheshimiwa Dkt. Hamis A. Kigwangalla pamoja na Mheshimiwa Luhaga J. Mpina.

**SPEAKER:** *Let's call in Honourable Stephen Masele. Tunapigia wawili. Honourable Stephen J. Masele, you are given three minutes to explain yourself before this August Assembly and you will be requested to answer three questions if there will be any.*

**HON. STEPHEN J. MASELE:** *Thanks Honourable Madam Speaker, Honourable Prime Minister, Honourable Leader of Opposition, Honourable Members of Parliament, my name is Stephen Julius Masele, I'm a Member of Parliament from Shinyanga. I'm a graduate from the University of Dar es Salaam in Political Science and International Relations.*

Madam Speaker, it's a huge privilege for me to be a Member of this House. I believe the best House produce the best representation in the Pan African Parliament. I have three reasons why I decided to contest for this position: (1) As we all know now

Africa is facing a lot of Political Crises, Pan African Parliament is an area of experience to me and I will like to add my knowledge on Pan African with regard to the conflict resolution in Africa. I'm sad and concerned with what is happening now with AU in regard of the issue of Libya. I would expect that the AU could make a strong statement against the NATO and the USA and allies on Libya. I'm saying this, I am not depositing Honourable Bernard Membe, but you never know.

Madam Speaker, secondly, I believe Pan African needs to learn the best from other Continental Parliaments. I believe we need to make Pan African Parliament very strong, to have more strong voice and to counterattack the move of NATO. We all believe now, the UN has less function and now main decision on International politics are being made by the US and NATO. We need Pan African to counterattack the move of NATO and to say nowhere we are supposed to say no! (Applause)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuonyesha ukweli na kuondosha upotoshaji, sasa nizungumzie kwa nini tumeona tu-*hamonize* Sheria hii ya Ushahidi na ya Jeshi la Polisi kuhusu tafsiri ya Afisa wa Polisi waanzie cheo cha *Constable* na kwenda juu. Afisa wa Polisi ni mweledi wa Jeshi la Polisi, ni mwajiriwa wa Jeshi la Polisi, wakati mwingine wanatoa ushahidi Mahakamani ambao ni wa kitaalam na taaluma yao yaani *professionalism* kama Afisa wa Jeshi la Polisi kwa sababu wanakuwa wameajiriwa. Tafsiri hiyo ni kielelezo kwamba wanapokuwa wanatafsiriwa kwamba wao ndiyo *Police Officer* katika eneo la ushahidi basi wanakuwa wanaaminiwa kwamba ni weledi na ndiyo wenye taaluma ya Jeshi la Polisi. Kwa hiyo, huo ndiyo msingi wake kwa nini sheria hizo mbili tunazioanisha kutoa tafsiri ya Afisa wa Polisi na ile nyingine ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, tunaitafsiri kwa maana ya kufanya kazi za Polisi zikiwa ni ukamataji na utendaji kwenye eneo la doria pamoja na misako.

Mheshimiwa Spika, Sheria hizi zimelenga kuboresha zaidi hasa watendaji kwenye Jeshi la Polisi, Sheria ambazo kwa kweli bila kuboreshwa au kurekebishwa zilikuwa zinaleta matatizo lakini tusifike mahali tukafika hapa tukaanza kutoa maelezo ya jumla katika kushambulia taasisi hii muhimu ya Polisi kwamba Sheria hizi Jeshi la Polisi wanakula rushwa hawa, maelezo hayo siyo sahihi, tukiacha maelezo kama hayo, tukawa tunayatoa bila kuyatolea maelezo Wabunge wengine, wanaweza siku moja Mbunge mwingine naye akasimama akasema, natoa mfano, Mawakili wa nchi hii wanakula rushwa, hatutafika, kama kuna Wakili anakula rushwa, anafahamika tena hata kwa jina, kwa hiyo, tusitoe maelezo ya jumla kwamba Taasisi inakula rushwa.

**SPIKA:** Na wewe u-*declare interest* zako sasa.

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, mimi siyo Wakili, lakini nimewahi kufanya kazi kwenye Jeshi la Polisi. Kwa hiyo, nina weledi na taaluma ya Jeshi la Polisi. Ndiyo sababu natumia nafasi hii kujaribu kutoa mchango wangu kueleza nini hasa tafsiri ya Afisa wa Polisi.

Mheshimiwa Spika, Sheria hizi ambazo zimezungumzwa hapa kwamba tusipozipitisha leo kwa sababu hazikuletwa hapa kama ile Sheria ya Hifadhi za Taifa, hizi ni Sheria zetu za Watanzania, kunapokuwa na haja ya kufanyiwa marekebisho, Sheria hizi ziletwe na tunaziitisha hata zile ambazo hazijaletwa leo kama zina matatizo zije kwa wingi ili Wabunge tuweze kuzifanyia marekebisho. Inapofika wakati tunahoji kwa nini imeletwa, kwenye *Schedule* hazikuwepo, Mheshimiwa Spika, tutazuia ufanisi kwenye Sheria mbalimbali wakati ni Sheria ambazo ni za Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, nalisema hili kwa sababu gani? Kama tutaendelea kubishana humu ndani kwa sababu tu Sheria fulani haikuletwa kama dharura, Sheria fulani hatukuiona kwenye *Schedule*, Sheria fulani mbona hapa tunaambiwa imekuwaje, wakati sheria hizi tunapoletewa hapa tunapata fursa ya kuzisoma, ni Sheria ambazo zina malengo mazuri kwa ajili tu ya ufanisi katika maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nashauri pia ile Sheria ya Hifadhi ya Taifa japo haikuonekana kwenye ile *Schedule* lakini ni Sheria ambayo kwa kweli inahitaji marekebisho na kama alivyosema Mwanasheria Mkuu wa Serikali, mimi naunga mkono moja kwa moja kwamba iwe mionganoni mwa Sheria ambazo tunahitaji kuzifanyia marekebisho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niache nafasi kwa mwenzangu, maana muda wangu bado upo ili na wao waweze kutoa mchango wao. Naunga mkono Muswada huu. (*Makofi*)

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuchangia. Nianze kwa kuishukuru Serikali kwa kuona umuhimu wa kuleta Muswada huu wa Kurekebisha Sheria kwa sababu inaonekana Sheria nyingi zitakazorekeblishwa zitakuwa kwa ajili ya tija kwa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuomba basi zile Sheria ambazo zitarekeblishwa kule kwenye maeneo vijijini wanakoishi wananchi, huwa hawafahamu hizi Sheria. Sheria inatoka, ikashawekwa kwenye *Government Gazettee* inapelekwa kwenye maofisi yaliyoko Mawilayani na mara nyingi zinabaki pale Wilayani, mwananchi wa kawaida anakuwa hajui. Mfano mdogo, unapanda basi mtu anavuta sigara mbele yako bila ya kujua kwamba imeshapitishwa Sheria kwamba huwezi kuvuta sigara mbele ya mtu mwengine. Kwa hiyo, naomba hizi Sheria uwekwe utaratibu wa kuhakikisha wananchi wote wanapata marekebiso ya hizi Sheria.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16, Kifungu cha 132 ambacho kinasema, watoto wale ambao watakuwa chini ya miaka 18 wasifungwe ile miaka 30 na badala yake irekebishwe. Nashukuru kwa marekebiso haya, kwa sababu mimi mwenyewe nilishuhudia watoto wadogo ambao wamefungwa kifungo cha miaka 30. Niombe basi pamoja na marekebiso ya Sheria hii, hawa watoto wawekwe kwenye Magereza ya Watoto wadogo na kule kwenye Magereza, wapate elimu kulingana na umri wao. Kama ni watoto wa umri wa *primary school* basi wapate elimu, kama ni watoto wa *secondary school* basi wapate elimu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na Sheria hii, Kifungu cha 7, Serikali inataka irekebishwe ili kuongeza makosa ya *pyramid schemes*. Sheria hii ya *pyramid schemes*, mara nyingi inawakumba akina mama wanaoingia kwenye mkumbo kwa sababu ya kutafuta kipato kidogo cha kulisha familia zao. Tulishuhudia *scheme* ya *women empowerment*, tukashuhudia *Dollar Jet* na baadaye tulishuhudia *DECI* ambayo watu wengi walipata hasara. Kwa hiyo, Sheria hii ni muhimu iende na *Bank of Tanzania Act* na iwe na *definition* au tafsiri kamili, ijulikane *pyramid scheme* ni nini.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu inaweza ikagusa mambo ya jamii moja kwa moja kwa sababu viro vikundi vyta akina mama, labda unakuta wapo sita na kila mwezi wanachangiana laki moja moja. Kama hii nayo itatafsiriwa kama ni *pyramid scheme* maana yake ni kwamba mpango huo unaweza ukaisha kwenye jamii na baadaye jamii itaendelea kuteseka. Kwa hiyo, naomba pawepo na *definition* kamili ya hii *pyramid scheme* na ikiwezekana pia pawe na *limitation*.

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20, Kifungu cha 38, ambacho kinasema Afisa wa Polisi anatakiwa ampe mkuu wake taarifa mara baada ya kufanya upekuzi. Hapa naomba tu nitoe tahadhari kwa sababu mara nyingi Polisi wanaenda kumpekua mwananchi au mtu ambaye wanafikiri ni mtuhumiwa, lakini anapita na ile hati ya kukamata mwenyewe, bila ya kupita kwenye Serikali ya Kijiji, bila ya kupita kwenye Kitongoji, anaenda moja kwa moja kumkamata mtu yule na kumpekua. Mimi naona kama hapa sio sawa, ni vizuri kwa vile Serikali yetu kule vijijini tumeiweka wenyewe basi ni vema huyu Askari amjulische Mwenyekiti wa Kitongoji kwamba leo nimekuja hapa katika Kitongoji, namhitaji bwana Juma au bwana Godfrey, nataka kwenda kupekua nyumba yake. Nadhani hiyo itakuwa haileti manung'uniko kwa mwananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Kifungu cha 383 (1), (2) na (3) ambayo inaipa mamlaka Mahakama kuamua kufuta rufaa na baadaye kuirudisha. Pia hapa naomba pawepo na tahadhari kwamba kuwepo na ukomo wa huo muda ambao rufaa inaweza kufutwa na ni muda gani inaweza kurudishwa. Kwa sababu, kama tusipoweka ukomo maana yake ni kwamba mwaka huu inaweza ikafutwa, ikakaa baada ya miaka mitano mtu huyu akasema nimekuja rufaa yangu ilifutwa na sasa nataka niendelee na kesi yangu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja, ahsante sana. (*Makofî*)

**SPIKA:** Sasa namwita Mtoa Hoja.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia na kujibu baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezichangia.

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja ya Sheria hii ya Muswada wa Marekebisho ya Sheria

Mbalimbali. Wa kwanza aliyeanza kuchangia ni Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Wa pili ni Mheshimiwa Tundu Antiphasi Mughwai Lissu, ambaye ametoa pia maoni ya Kambi ya Upinzani. Wa tatu aliyechangia Muswada huu ni Mheshimiwa Mchungaji Peter Simon Msigwa, wa nne alikuwa ni Mheshimiwa Assumpter Nshunju Mshama, wa tano alikuwa ni Mheshimiwa Alphaxard Kangi Ndege Lugola, wa sita alikuwa ni Mheshimiwa Betty Eliezer Machangu; hawa ndio waliochangia kwa mdomo, kama nimewanukuu sawasawa na kama nimemsahau mtu basi nitamtaja baadaye, lakini hiyo ndio kumbukumbu yangu kwa waliochangia kwa kusema.

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa kuniandikia wapo sita, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, wa Viti Maalum, Mheshimiwa Zahra Ali Hamad ambaye anawakilisha Baraza la Wawakilishi, Mheshimiwa Martha Umbulla, wa Viti Maalum, Mheshimiwa Selemani Jafo, Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau na Mheshimiwa Amina Amour na wa saba ni Mheshimiwa Naomi Mwakyoma Kaihula, ambaye amewasilisha mchango wake wa maandishi hivi punde.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba Sheria na Utawala, kwa maoni waliyotoa pamoja na angalizo walilolitoa kwenye sehemu ya ushahidi kwa mtu ambaye hayupo Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, sasa nije kwa Mheshimiwa Tundu Antiphasi Mughwai Lissu; ninamshukuru sana kwa elimu aliyoitoa, ametoa maelezo mazuri na maelezo hayo yanaweza pia kuboreshwa.

Mheshimiwa Spika, jina la Muswada ambao upo mbele yako ni Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali. Kama ilivyo, kuna jambo ambalo Wabunge wenzangu wameniambia ambalo lipo kwenye lile Jedwali la Marekebisho ya Sheria kuhusiana na Sheria ya Wanyamapori. Hoja ni kwamba utaratibu wa kuingiza Sheria nyingine ambazo hazikuwemo kwenye Muswada uliosomwa kwa mara ya kwanza unakiuka Kanuni. Mimi naomba tusaidiane tu, hakuna haja ya kufanya ubishi kama itaonekana ndivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida Jedwali ambalo nililiwasilisha kwenye Kamati Dar-es-Salaam, halikuwasilishwa kwa mujibu wa Kanuni ya 86(10) kwa sababu Muswada ulikuwa haujafikia hatua hii ya pili. Lengo la Jedwali na kama nilivyoeleza kwenye Kamati, mimi nilifikiri tumeelewana pale, lilikuwa ni kuisadia Kamati na Wadau, wajue Sheria zinazokuja ambazo tulikuwa tunafikiri kwamba ni vizuri zifanyiwe marekebisco.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali una jina hilo, ni tofauti na unapofanya marekebisco ya Sheria nyingine. Kwa hiyo, nafikiri kwa mujibu wa Kifungu cha Kanuni ya 84(3), nimesema kwamba kwa sababu hapa ni Bunge na sisi ndio tunatunga Sheria, ni vizuri tuelewane kwenye Kanuni na kama tunafikiri kwamba Kanuni hizi hazituruhusu, basi tutakubaliana kwamba ile sehemu iondoke.

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 84, ndiyo ambayo ilituwezesha sisi kufanya haya tuliyofanya kwa sababu, ukiangalia kwenye fasili ya 3 ya Kanuni ya 84, inasema:-

*“Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 99 ya Katiba, Kamati iliyopelekewa Muswada itakuwa na uwezo wa kufanya marekebisho katika Muswada wa Sheria kwa kumshauri Waziri au Mbunge anayehusika na Muswada huo kufanya mabadiliko, vilevile Serikali itakuwa na uwezo wa kuishauri Kamati ya Kudumu ya Bunge kuhusu kufanya marekebisho au mabadiliko juu ya Muswada binafsi”.*

Kanuni ya 84(4) inasema:-

*“Kabla ya Muswada wa Sheria uliofanyiwa mabadiliko haujawasilishwa Bungeni kwa ajili ya Kusomwa kwa Mara ya Pili, utapelekwa kwenye Kamati inayohusika kwa madhumuni ya kuzingatia mabadiliko hayo”.*

Mheshimiwa Spika, tulichofanya pale ni kuwa wazi kwamba tulikuwa tunatakiwa kufanya marekebisho katika sheria nyingine pamoja na zile ambazo tumeziondoa. Zile ambazo tumeziondoa hatukuziondoa kwa sababu ya kuhofia kwamba hazikufuata Kanuni, tumeziondoa kwa sababu ya ushauri uliotolewa kwenye Kamati kuhusiana na mantiki ya Sheria hizo na hapa ni lazima niseme...

## TAARIFA

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu, Taarifa.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, amenukuu Kanuni ya 84 (3) juu ya marekebisho ya Muswada na amesema kwa maneno yake kwamba vilevile Serikali itakuwa na uwezo wa kuishauri Kamati ya Kudumu ya Bunge, kuhusu kufanya marekebisho au mabadiliko juu ya Muswada Binafsi.

Mheshimiwa Spika, Muswada uliokuwa kwenye Kamati ya Katiba na Sheria haukuwa Muswada Binafsi. Mwanasheria Mkuu wa Serikali hakuwa na uwezo kwa mujibu wa Kanuni hizi, kuleta Jedwali la Marekebisho kwenye Kamati katika *stage* hiyo ya mjadala kwenye Kamati. Kanuni zinasema angefanya hivyo kama Muswada ungekuwa ni wa binafsi. Ahsante.

**SPIKA:** Kwa nini usingeisoma kidogo ile Kanuni iliyosema?

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

*“Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 99 ya Katiba, Kamati iliyopelekewa Muswada itakuwa na uwezo wa kufanya marekebisho katika Muswada wa Sheria kwa kumshauri Waziri au Mbunge anayehusika na Muswada huo kufanya mabadiliko. Vilevile Serikali itakuwa na uwezo wa kuishauri Kamati ya Kudumu ya Bunge kuhusu kufanya marekebisho au mabadiliko juu ya Muswada binafsi”.*

**SPIKA:** Endelea kueleza *argument* yako sasa.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, *argument* yangu ni kwamba kwa mujibu wa Kanuni, namna pekee Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuleta Jedwali la Marekebisho Bungeni ni baada ya Muswada Kusomwa Mara ya Pili chini ya Kanuni ya 86(10) (b), ambayo aliifanya jana. Katika hatua ya Muswada Kusomwa Mara ya Pili, hauwezi ukaleta kitu ambacho hakikuwepo kabisa katika Muswada. Haiwezekani kuleta Sheria ambayo haikutangazwa katika Gazeti la Serikali kwamba hii inatakiwa ifanyiwe marekebisho, inachomekwa tu kwenye *debating floor*, huo sio utaratibu wa Kanuni za Bunge hili. Naomba Kanuni za Kudumu za Bunge hili ziheshimiwe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, maelezo yako ni sahihi kwamba Muswada tunapousoma Mara ya Kwanza unakuwa *public*, kwa hiyo, haujaingia kwenye hatua ya kurudi Bungeni na hata kwenye tovuti yetu unakuwepo. Sasa huu Muswada ukishasomwa Mara ya Kwanza utakaporudi wakati huo, hata *public hearing* kama mnavyofanya sasa hivi inaweza kufanyika.

Sasa kama maelezo haya ni kweli kwamba wakati Muswada wa *Miscellaneous Amendments* Unasomwa Mara ya Kwanza, baadhi ya Sheria zilizoletwa humu hazikuwemo, sio sahihi. Hivyo ndivyo alivyosema. Kama zililetwa nje ya *First Reading* tuliyokuwanayo hapa sisi, ikaletwa kwenye Kamati, hiyo sio sahihi. (*Makofi*)

Lakini pia jana Mheshimiwa Tundu Lissu alikuwa anahoji Muswada mwingine ule wa *Miscellaneous* uliomalizika kuhusu maeneo ya EPZ akasema tumesoma kwa hatua zote. Tunapozungumzia hatua zote ni *First Reading* kwa sababu zamani tulikuwa tunaweza kuitisha hatua zote hapahaha lakini tuka-introduce suala la *public hearing*, kwa hiyo, haiwezekani Ukasomwa Mara ya Kwanza hapa, ukafanya *public hearing* hapohapo, ukaingia Kusomwa Mara ya Pili hapohapo na Mara ya Tatu, hiyo ndiyo tunayoikataa. Lakini Ukitisomwa Mara ya Kwanza Bunge hili, hapa katikati unategemea kutakuwepo na *public hearings*, Kamati itafanya utafiti wake, wananchi wataweza kusema, tukifika hapa Mkutano unaofuata au mwingine wowote baadaye ndio Tunasoma Mara ya Pili ile ya Kusomwa Mara ya Tatu ni kama *endorsement* tu basi.

Kwa hiyo, pale jana kwa Muswada ule wa Maeneo ya EPZ ulifuata utaratibu lakini hili unalolisema sasa kama ndivyo ilivyokuwa, sio utaratibu. (*Makofi*)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni, wewe ndio Jaji Mkuu hapa na sitabisha isipokuwa tutakapofika kwenye eneo hilo, pengine tunaweza kushauriana.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo Mheshimiwa Tundu Lissu, alilizungumzia kwa kirefu ni hili ambalo lipo kwenye Sheria ya Ushahidi na baadhi ya wachangiaji wengine wamelizungumzia pamoja na Mwenyekiti wa Kamati, alipotuambia kwamba tuangalie sana kuhusu ule ushahidi ambao unachukuliwa kwa njia ya mtandao.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusiana na suala la *definition* ya *Police Officer*, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Kangi, kwa maelezo yake. Marekebisho tunayofanya kwenye Sheria hii yanahu Sheria ya Ushahidi na ndivyo Kifungu hicho kinavyoanza, *for purposes of this Act*. Kwa hiyo, maana ya Polisi tunayotoa tafsiri yake ni yule Polisi anayetajwa na anafanya shughuli ambazo zimeainishwa katika Sheria ya Ushahidi, ni shughuli gani hiyo?

Mheshimiwa Spika, katika Sheria ya Ushahidi, Kifungu cha 27, Polisi anafanya kazi moja, kuchukua maelezo ya ungamo. Kwa mfano, mtu anapokabiliwa na kesi ya mauaji anakwenda kuchukuliwa maelezo, sio kila Polisi anamchukua maelezo. Huyo Polisi anayechukua maelezo hayo ni lazima awe mwenye cheo cha Koplo na zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa katika utekelezaji, imeonekana kwamba ma-Koplo sio wengi katika maeneo mbalimbali na matokeo yake maelezo hayo yanachelewa kuchukuliwa. Kwa hiyo, sasa tunasema kwamba neno Polisi na hii kazi ni kazi ya utaalamu na Polisi wa sasa sio Polisi wa miaka ya 50, 60 na 70, tunao Polisi ambao wana taaluma na wamesoma vizuri kama watu wengine, sasa tunataka badala ya kuanzia Koplo, Konstebo na yeze aweze kuchukua maelezo hayo na tafsiri ya Polisi kwa mujibu wa Sheria ya *Evidence Act* ifanane na Polisi anavyotafsiriwa katika Sheria ya Polisi na Polisi Wasaidizi, ambayo ndio Sheria inayo-govern administration ya Polisi. Kwa hiyo, hicho ndicho tunachofanya.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia ile Sheria ya Polisi, Kifungu cha 4, kimeweka mlolongo wa vyeo. Makonstebo ni watu gani, *NCOs* ni watu gani na *Gazetted Officers* ni watu gani. Kwa hiyo, nia ya mabadiliko haya kwa mujibu wa Sheria ya Ushahidi ni kuruhusu Polisi Konstebo kuweza kuchukua maelezo chini ya Kifungu cha 27, hayo ndiyo tunayoyafanya.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Sheria ya Ushahidi pia Mheshimiwa Tundu alisema kwa maelezo marefu, nafikiri alikazia zaidi kuliko ilivyokuwa inatakiwa. Anacho sema Mheshimiwa Tundu ni kwamba unapokuwa umekaa kwenye kiti, unaamua jambo, Hakimu au Jaji, jinsi shahidi anavyoonekana inaweza kukusaidia pia kujua *integrity* ya ushahidi wake, yaani kwa maana ya ile *demeanour*, anavyoonekana, anavyopepesa macho, anavyokwepa maswali lakini Waheshimiwa Wabunge, hebu angalieni kwenye *screen* ya Bunge, niangalieni mimi pale, niangalieni nilivyo hata nikipepesa macho mtaona. Kwa hiyo, ni lazima tukubali kwamba sasa hivi dunia

imebadilika. Mtu yuko Washington, wewe upo Dar es Salaam na tumeanza kufanya kwa mfano kwenye *negotiations* sio lazima uende New York, unaweza kukaa Dar es Salaam pale, mkazungumza, mkaelewana. Juzi katika kesi moja tumechukua ushahidi kutoka Italia na hatukuona tatizo lolote.

Mheshimiwa Spika, lakini pia hili lazima niliseme kama mtaalam na kama *head* wa Chama cha Mawakili wa Tanganyika, ninatakiwa kuzungumza kwa heshima kwa Mheshimiwa Lissu, *credibility* ya shahidi halitegemei kumuona tu, inategemea pia na vitu vingine. Katika Juzu ya Maamuzi ya Mahakama ya Afrika Mashariki, Juzu ya 18 ambayo ilitolewa mwaka 1951, ukurasa wa 233, kuna uamuzi huo ambao umetu-guide Majaji. Lakini kama ukishindwa kupata hapo, kuna kesi ambazo Mahakama zetu zimeamua, Majaji wetu wa Mahakama ya Rufani wameamua kuhusu jambo hili la *demeanour*, sio lazima utegemee *demeanour* peke yake. Kuna vitu vingine vyaya kufanya. Kuna kesi ya JACKSON MWAKATOKA, mwaka 1990, Ripoti ya Sheria Tanzania ya mwaka 1990, ukisoma ukurasa wa 17, utaona uamuzi wa Mahakama ya Rufani ambao unazungumzia kuhusu suala hili. Lakini pia kuna kesi ya zamani ambayo ndiyo msingi wa kesi hizi, kesi ya Uganda ambayo inaitwa TUWANOI v. UGANDA ya 1967, ukurasa wa 91 wa yale ma-book ya *East Africa*. Kwa hiyo, hili suala la *demeanour* haliwezi kukufanya ukaacha kutumia teknolojia.

Mheshimiwa Spika, nitoe taarifa kwamba tutaleta Sheria ya Matumizi ya TEKNOHAMA ili ku-*rationalize* kutumia mambo haya katika Sheria zetu, ushahidi na mambo haya ya uchunguzi wa makosa ya jinai. Kwa hiyo, namwomba ndugu yangu hapa asiogope mambo haya, mambo haya yanakuja na hatuwezi kuyakwepa na kwa sababu tuna Waheshimiwa Majaji, Mahakimu na wenyewe wamefundishwa mambo haya, wamejifunza namna ya kutoa haki, nina hakika watafanya kazi hiyo vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wazo ambalo Mheshimiwa Tundu amelizungumzia, kwa sababu nafikiri alitoa elimu lakini elimu ile nafikiri inahitaji kuangaliwa upya. Nafahamu kazi ya Wakili ni kushawishi na naomba wakati wanashawishi wasiwe Mawakali. Unashawishi watu wakubaliane na wewe na hapa ukiwa Bungeni, Bunge ndilo linalotunga sheria na katika kushawishi lazima ulielekeze Bunge kama ulivyofanya kwenye Kanuni kwamba hili jambo halikuwepo na limekuwa sio sawasawa kulileta. Kwenye hili la kufananisha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kwamba Polisi alivyotafsiriwa pale ni sawasawa na ile ya *Evidence Act*, ndugu yangu kwa kweli sio sahihi. Tafsiri ya *Criminal Procedure Act*, yaani Sheria ya Makosa ya Jinai inawahusisha Sungusungu na Mgambo, hatuwezi kuwapa hao nafasi ya kuchukua maelezo ya washtakiwa kwa sababu kazi hii hawajasomea. (*Makofi*)

Sasa kama mimi nilivyokubali kwamba hilo la kwanza tukubaliane kwamba tuliondoe na hili nafikiri hoja hiyo na wewe pia uiondoe.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Hii kengele iliyogongwa sio ya kwako.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, sawa. Mheshimiwa Tundu, aliongea vitu vingi lakini nafikiri wakati wa kupitia Vifungu, nafikiri vingine nitavigusia.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Kifungu cha 6 hichohicho, Mheshimiwa Mchungaji Peter Simon Msigwa ametoa angalizo kwamba mantiki ya marekebisho ya Kifungu cha 6 haielewi. Kifungu cha 6, labda kuna *confusion*, tulifanya marekebisho ya Sheria kwenye eneo hili la mtoto wa miaka 12 - 18 anayebaka adhabu yake ni hii hapa. Ilivyo sasa ni kwamba yule anayejaribu kubaka ambaye ana umri wa miaka 12 - miaka 18 kosa lake ni kubwa zaidi kuliko huyu anayebaka, kosa lake kifungo cha maisha au kifungo kisichozidi miaka 30. Kwa hiyo, tunasema kwamba tunaoanisha kusudi adhabu hiyo ya mtoto isiwe hivyo, ndivyo tunachofanya hapa.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna mawazo mengine ya kutowapeleka hawa watoto kwenye shule za manunda, hilo sasa ni suala la sera na mimi nalichukua lakini kwa ajili ya kubadilisha sheria, tunachofanya hapa ni kupunguza adhabu ya mtoto huyu isiwe kifungu cha maisha au miaka 30 isipokuwa hizi zinazotajwa hapa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna jambo limezungumzwa kuhusiana na adhabu ya viboko, wengine wanasema adhabu hii hairuhusiwi kwamba inakiuka Sheria ya Mtoto na inakiuka mikataba ambayo Tanzania imeingia na yalitolewa madai kwamba tunasaini mikataba kusudi tupate fedha, nafikiri pia tuangalie maneno tunayotumia, unajua hili ni Bunge ambalo kila mtu anakusikia na wengine nje wanaskia, sio vizuri kusema mambo mengine haya ambayo yanaweza kutuharibia sifa kama nchi. Adhabu ya viboko inatawaliwa na sheria, yako masharti ambayo lazima uyafuate na kuna maneno ambayo tunatumia, Kiswahili kinaweza kuyakosa, kiboko kwa mtu mkubwa kwa Kiingereza tunasema *whipping*, kwa mtoto *canning* na hata ile fimbo inayotumika ni *regulated*, ina ukubwa fulani na ina urefu kiasi fulani na pia huwezi kuitoa hiyo adhabu mpaka kwanza mtabibu aruhusu kwamba huyu mtoto anastahili kupigwa viboko lakini vilevile hata Waheshimiwa Majaji au Mahakimu wanaweza kutoa adhabu mbadala, kuna *description* hapa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nachosema ni kwamba adhabu ya kiboko ilivyo kwenye Sheria zetu siyo adhabu ya kutweza, kinachozuia ni kutoa adhabu ya kutezwa na naomba kuchukua nafasi hii kuwaasa Walimu, sio suala la kwenda kuchuma fimbo na unaanza kuitumia kuwachapa watoto, hiyo itakuwa ni adhabu ya kutweza lakini kama fimbo ile imekuwa *prescribed* kwenye Sheria, ni lazima ufuate hayo masharti. Ni vizuri kuachana na adhabu ya viboko lakini ukifanya hivyo uwe na kitu mbadala kwa sasa Sheria yetu inaona kwamba ni vizuri tuendelee na adhabu hiyo ya viboko lakini sio adhabu ya kutezwa. Naona niliseme hilo kwa sauti kubwa kusudi lieleweke.

Mheshimiwa Spika, kwenye Kifungu cha 10, tumefanya mabadiliko kwenye Kifungu cha 287A, Mheshimiwa Tundu Lissu alisema kwamba mabadiliko hayo siyo ya maana na akaja na hoja kwamba kuna *issue* ya *mens rea* yaani *mens rea* ni ile *common*

*intention*, unataka kufanya nini, umefikiria kitu ukasema lazima ufanye kosa fulani au ufanye kitu fulani lakini la pili ni *actus reus* yaani lile tendo la kufanya tendo ovu.

Mheshimiwa Tundu ni Mwanasheria na nafikiri anafahamu kabisa kwamba kuna *distinction* kati ya kosa la *armed robbery* na *robbery with violence*, *there is a big difference, there is a distinction, mens rea* ni sawasawa lakini *actus reus* ni tofauti na kuna kesi nyingi nafikiri sina haja ya kukusomea, utakuwa unazijua mwenyewe na kama unaweza kufuatilia kesi zangu nilizokuwa naamua ukuta tafsiri hiyo ya kosa la *armed robbery* na *robbery with violence*. Tunachofanya hapa, tunafanya *distinction* kwenye Sheria na sio zaidi ya hapo, nafikiri tutaelewana tu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelizingumzia ni Sheria ya Uchawi. Kwanza kuna hili la *pyramid schemes, pyramid schemes* tunachofanya sio kigeni isipokuwa tunaleta kitu ambacho kitazuia hayo na ninyi ambao mnafanya hizo shughuli muache tamaa, kwa sababu *banking* ina sheria yake lazima ufuate utaratibu.

Mheshimiwa Spika, kuna vitu vingine hivyo mkifanya, kuna nchi zimefanya haya mambo mpaka zikaanguka yaani mkiwa na *DECI* kubwa kama ile, inaweza kutuletea matatizo nchini. Kwa hiyo, lazima kuwe na *regulation*. Kuna tatizo la watu kutumia simu kuiba fedha kwenye M-Pesa au Tigo au nini, *you have to capture that*, sheria lazima iwe mbele, ndicho tunachofanya hapa.

Mheshimiwa Spika, kwenye Sheria ya Uchawi, watu wanashangaa kwamba kwenye karne hii bado Serikali inaanmini uchawi. Serikali inaanmini uchawi kwa sababu na ninyi mnaamini uchawi na tukipekua mifuko ya watu wengine hapa tutakuta mahirizi. Wengine wanasema kwamba ukisimama hapa mpaka ukae vizuri. Sasa jamii yenye inaanmini hivyo. (*Kicheko/Makofit*)

Mheshimiwa Spika, sasa tunachofanya ni nini? Leo asubuhi nilikuwa naangalia taarifa ya habari kutoka Musoma, wanasema kwamba kuna mtu amekufa, wamemkamata mama mmoja amekubali kwamba ye ye ndiye amefanya hiyo shughuli na wampe pesa amfufue. Yule mama alipokwenda kwenye ile nyumba, nikasikia, mimi sijui, eti yule bwana katoa tu kichwa hivi, machozi yakatoka, karudi tena kulala. Sasa mambo hayo ni mambo ya imani. Mimi ni Mkatoliki wala sioni aibu kusema hivyo lakini mambo hayo yapo.

Mheshimiwa Mongella alichaguliwa kufanya utafiti wa uchawi, akatembea nchi nzima, akatoa ripoti uchawi upo. Kuna Profesa mmoja, sijui kama ni wewe, amefanya utafiti wa uchawi, uchawi upo. Wale tunaosoma Biblia wanasema upo lakini wanasema usiogope na hata kwenye Mithali pale wanaimba, nani ataniweza Mungu ndiye mlezi wangu.

Mheshimiwa Spika, sasa tunachofanya hapa ni nini? Baada ya Sheria hii kupigiwa kelele sana ili ifanyiwe marekebisho, katika Kifungu cha 8, kilitoa nafasi kwa huyo mtu anayetuhumiwa kwenda kujitetea yaani kufanya uchunguzi (*enquiry*) naye ajitetee kwa

sababu kuna watu wengine hapa, ile Kamati ya Ufundu ya Timu ya Bunge labda wakipata nafasi waje watuelimishe na wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa huyu mtu ndiye tunasema kwamba amekubuhu na *DC* amefanya uchunguzi imegundulika kwamba ni kweli anafanya hivyo tunamhamisha aende mahali pengine, anaweza kwenda kwa wachawi wenzake, anawajua. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, tunasema sasa hiyo Sheria imepewa nafasi hiyo ya kumpa nafasi kuthibitisha kwamba yeze siyo mchawi. Nafikiri tuwe *realistic*. Unajua kuna mambo mengine ambayo ukikaa hapa na viti vyekundu hivi unafikiri upo Ulaya, lakini *be realistic*, nyie wenyewe mnajua Waheshimiwa, kwa hiyo, tunachofanya hapa ni kwamba tunapandisha adhabu kwamba huyu ambaye anakataa, zamaani alikuwa anapigwa faini ya shilingi 150 na wanalipa au kifungo kisichopungua miezi miwili. Sasa haya matatizo yanakuwa makubwa, nyie Wabunge mnatoka kwenye Majimbo, mnajua kuliko mimi ambayo yanawasibu watu huko, ndicho tunachofanya hapa lakini ninyi ndio watungaji wa Sheria na Sheria ili iwe na maana lazima ichukue maslahi ya watu walio wengi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limezungumziwa, ni Kifungu cha 22, ile adhabu ambayo ilikuwa inatolewa zamaani ilikuwa inataja kiwango, lakini tumeona kwamba katika utekelezaji, inabidi kila wakati ukitaka kubadilisha viwango inabidi uje hapa Bungeni na tunafikiri kwamba Mahakama ipo kwenye nafasi nzuri zaidi ya kuangalia kwa sababu hata Jaji anaweza kutoa amri Wakili asilipwe fedha na mtu anayemtetea kama akiona kwamba Wakili huyu hakufanya bidii yoyote kwenye kazi hiyo. Jaji anaweza kusema usimlipa huyu pesa, inawezekana. Mimi nilishafanya hivyo mara mbili, kama unaona mtu hakufanya kazi yoyote. Kwa hiyo, Mahakama iko kwenye nafasi nzuri zaidi kuliko kutunga sheria na ukaweka kwamba ikiwa hivi basi aliipe kiasi hiki. Tunashauri adhabu hiyo ambayo tunapendekeza ndiyo iwe adhabu ambayo inastahili, mambo mengine yanahu su vifungu maalum nya utumishi.

Mheshimiwa Spika, kwa hili la *Extradition*, Kifungu cha 43, ni kwamba yapo makosa ambayo unaweza kumkamata mtuhumiwa bila kuwa na hati ya kukamata, yapo! Sasa ni kwamba huyu ni mkosaji mtoro, kama yule Mtanzania mmoja ambaye alifanya makosa kule Uganda akakimbilia mahali fulani na ukamuona, *by the time* unakwenda kuchukua hiyo hati ya kumkamatia, anakuwa ameshajificha. Ndiyo tunasema kwamba huyo mtu akamatwe na kwa utaratibu wa kawaida, atapelekwa Mahakamani au arudishwe alikotoka, ndiyo maana tunesema hivyo.

Mheshimiwa Spika, hili la mwisho la Sheria ya Wanyamaporu ambayo tumeifanyia marekebisho, marekebisho ni madogo sana lakini kwa kuheshimu uamuzi wako, naiondoa Sheria hiyo kwenye Jedwali na kwenye Shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili*)

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2011 (The Written Laws (Miscellaneous Amendment Bill, 2011)**

Kifungu cha 1

**MHE. TUNDU M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 77(1), inayohusu akidi ya vikao, inataka nusu ya Wabunge wawepo wakati wa kufanya maamuzi. Sasa sijui kama tuna akidi iliyotimia.

**MWENYEKITI:** Akidi inatosha, tunaendelea!

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 2

Kifungu cha 3

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 4

**MWENYEKITI:** Katika muda wa kupitia Kifungu kwa Kifungu, Kanuni yetu ya marekebisho inamruhusu Mheshimiwa Mbunge kuleta kwenye *floor* marekebisho au Serikali yenye Muswada ikaleta marekebisho au Kamati iliyoshughulikia Muswada ikeleta marekebisho. Kama marekebisho yale yameletwa na Mbunge binafsi na Kamati, katika *stage* hii tunasikiliza marekebisho ya ile Kamati au yule Mbunge kama anavyofanya Mheshimiwa Tundu Lissu. Kama tutajadiliana kuhusu marekebisho haya halafu tunapiga kura, kama kura yetu itakubaliana na marekebisho ya Mheshimiwa Mbunge, basi Kifungu kile kinaondoka na Serikali pengine haleti marekebisho katika Kifungu kile. Kama tutakapojadiliana tutakataa marekebisho ya Mheshimiwa Mbunge au Kamati, basi marekebisho ya yule Mbunge au Kamati yanawekwa pembeni, tunaendelea na marekebisho ya Serikali kama yapo au kama Kifungu kilivyokuwa. Kwa hiyo, huu ndiyo utaratibu, Mheshimiwa Tundu Lissu!

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika Kifungu cha 4 cha Muswada, napendekeza ile tafsiri ya neno *Police Officer* inayopendekezwa katika Kifungu cha 4(a) ifutwe badala yake iwekwe tafsiri ifuatayo:-

*“Police Officer” includes any member of the Police Force and any member of the People Militia when exercising Police functions in accordance with the law for the time being in force”.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nielezee maana ya pendeleko langu. Hii tafsiri nayoipendekeza ya neno “*Police Officer*” ndiyo tafsiri iliyopo katika Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20. Sheria inayoruhusu Polisi kuchukua maelezo ya shahidi, kukusanya ushahidi na kufanya upelelezi siyo Sheria ya Ushahidi bali ni Sehemu ya Pili ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai. Sasa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai inatafsiri “*Police Officer*” kwa mapana hayo, itakuwa vizuri iwapo hii ndiyo itakuwa *standard definition* ya hilo neno “*Police Officer*” katika Sheria zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 4(b), napendekeza kufutwa kabisa kwa *paragraph (b)* katika Muswada inayotaka marekebisho katika tafsiri ya neno “*oral evidence*”, ifutwe kabisa na maana yake ni kama nilivyosema katika hoja yangu jana ushahidi wa TEKNOHAMA una matatizo yake ambayo hayajatafutiwa majibu. Moja, kama nilivyosema Mahakama inapochukua ushahidi, ni lazima yaani *shall*, inatakiwa kuandika *demeanour* ya shahidi, kuandika hiyo *body language* ya shahidi, *it is a mandatory requirement* kwenye Sheria ya sasa hivi ya Mwenendo wa Jinai. Sasa kwenye TEKNOHAMA hakuna uwezekano wa Mahakama kuweza kujua huyo shahidi ana *behave* namna gani, hawezi kuonekana mwili mzima katika *screen*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ushahidi wa Teknohana una tatizo lingine ambalo nililisema jana kwamba kuna mashahidi ambao wanakataa kutoa ushahidi, wanakataa kuapishwa na Kifungu cha 137 au 199, nafikiri nilisema jana, kinalekeza kwamba shahidi kuwa *refractory*, huyo anayekataa kuapishwa au anayekataa kutoa ushahidi anadhibitiwa na Mahakama yaani Mahakama inaanuru aende ndani mpaka atakapokubali kutoa ushahidi. Sasa tukiruhusu ushahidi utolewe kwa Teknohana, shahidi yuko Marekani au Italy na kadhalika anapokataa kuapishwa itakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba mapendekezo yangu yakubaliwe.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kwa upande wa Serikali!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ushahidi ambako ndiko tunataka *definition* hii iende, katika Kifungu cha 27 inasema pale ambapo mtu anatoa maelezo ya ungamo anasema:-

(1) a confession voluntarily made to a Police Officer by a person accused of an offence may be proved as against that person.

(2) the onus of proving that any confession made by an accused person was voluntarily made by him shall lay on the prosecution.

(3) a confession shall be held involuntary made if the court believes that it was induced by any threat, promise or other prejudice carried out by the Police Officer to whom it was made or by any member of the Police Force or by any other person in authority.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukienda kwenye tafsiri ya neno “*Police Officer*” kwenye Sheria hii ya Ushahidi inasema:-

“for the purposes of this Act, Police Officer means any member of the Police Force of or above the rank of a Corporal”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunasema tafsiri hiyo ni finyu inayowazua watu wenyewe utaalamu wa kazi ya Polisi, ndiyo tunasema kwamba aanzie *Constable* kama inavyotafsiriwa kwenye Sheria ya Polisi na Polisi Wasaidizi. Sasa hili linalopendekezwa na Mheshimiwa Tundu Lissu linawaingiza Sungusungu na Wanamgambo na wenyewe wachukue maelezo hayo, haiwezekani! Kwa sababu gani? Nawaheshimu sana Sungusungu wanapotekeleza kazi zao kwa mujibu wa Sheria lakini wanapovunja Sheria zile siko nao. Kwa hiyo, nasema hatuwezi kuweka rehani haki za watuhumiwa, ndiyo maana tunasema kwamba hii iende kwa wale ambao ni *Professional Police*, watu wanaofanya kazi ya Kipolisi. Tafsiri hii haihusiani na ile tafsiri iliyoko kwenye *Criminal Procedure Act* na namwomba Mheshimiwa Tundu Lissu kwamba mantiki hapa ni Sheria ya Ushahidi, Kifungu cha 27, ni nani achukue maelezo ya mtuhumiwa? *Definitely*, kama unayoyasema ni kweli hawezi kuwa Sungusungu wala Mgambo, ni lazima awe a *Professional Police*, Polisi mwenye utaalamu. Napendekeza mabadiliko yaliyofanywa kwenye Sheria hiyo yabaki kama yalivyo.

**MWENYEKITI:** Kuna (b) ambayo imefuta ya kwenu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwenye hili la Teknohama, narudia tena na nimetaja mifano ya kesi za Majaji walionitangulia. Kitu kikubwa katika mambo haya wala siyo *demeanour*, *demeanour is a fraction* na usifikirie wala usiwe na mawazo ya kwamba kesi zote hizo ni za *criminal*, ziko kesi za biashara ambapo unatakiwa ufanye *decision* leo ili kusudi kesho mtu aweke mali yake kwenye *stock exchange*, kuna uamuzi ninatakiwa nifanye sasa hivi ili New York wakifungua soko lao saa tatu leo yaani kama sasa hivi basi uamuzi huo uwe umefanywa, huwezi kungoja mpaka mtu aje hapa mzungumze naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapa tutofautishe kwani kuna mambo ambayo yanatakiwa yaamuliwe kama umeme na Sheria ilivyo sasa inatukwaza, nafikiri wote tunafahamu na Wakili Msomi Mheshimiwa Mbunge anafahamu kwamba dunia hii siyo ya jinai (*criminal*) pekee yake, hii dunia pia ni ya biashara na biashara haingoji kesho. Lakini hata kama ni kesi ya jinai ambayo iko Mahakamani, naweza kuisema nayo ni kesi dhidi ya Professor Mahalu, tumechukua ushahidi kwa yule Muitaliano ambaye alikuwa anakataa kuja na hatukupata tatizo, tatizo lililokuwepo ni la kisheria kwamba yule aliyechukua ushahidi hakuwa anatakiwa kuchukua ushahidi nje ya Dar es Salaam. Sasa swali linakuja kwenye mtandao pale unaponiona nipo Bungeni au niko Kiagata? Hilo ndilo lilikuwa swali lakini mwenyewe sasa kabla ya swali hilo halijajibiwa akasema amejitoa na ndiyo ustaarabu, usibishane mpaka mwisho, akajitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sababu ya kufanya mabadiliko hayo ya kutumia Teknohama ni kukubali ukweli kwamba sasa hivi mambo yamebadilika na utaratibu wa

kusema *safeguards*, *safeguards* zipo na *safeguard* mojawapo ni Jaji mwenyewe. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge ambaye pia ni Wakili maarufu, nafikiri Sheria hii itawasaidia zaidi wafanyabiashara na watu ambao wanafanya makosa ya jinai kwani kuna makosa ambayo ni ya kibiashara pia, yes! Kama unaiba kwenye *stock exchange* unapatikana uko Tanzania, umehamisha fedha na yenyewe inakusaidia hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nasimamia kwamba haya marekebisho yanayopendekezwa na Serikali yana tija kubwa sana kwenye kukua kwa uchumi hasa baada ya ninyi jana kupitisha yale marekebisho ya EPZ. Kwa hiyo, namwomba mwenzangu kama mimi nilivyokubali kuondoa ile ya *Wildlife* basi na yeche tuendelee mbele.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja hii ni ya Tundu Lissu kwa hiyo tunakupa dakika tatu.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza sana hoja ya Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Hoja kuhusiana na pendekezo la kwangu la kufanya tafsiri ya neno *Police Officer*, kama ni kweli kwamba mapendekezo ya Muswada huu kuhusiana na neno *Police Officer* ilikuwa na lengo la Kifungu cha 27 cha Sheria ya Ushahidi basi Muswada ungesema hivyo katika madhumuni na sababu zake lakini sababu na madhumuni ya Muswada hayasemi hivyo kuhusiana na *Police Officer* ila inasema Kifungu cha 3 kinarekebishwa kwa kufuta tafsiri ya neno *Police Officer* na kutoa tafsiri mpya ili kuondoa mkinzano uliokuwepo kati ya Sheria hii na Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi. Kwa hiyo, hii *amendment hailetwi for purposes of section 27* ya Sheria ya Ushahidi bali inaletwa ili kuondoa *conflict* kati yake na Sheria ya Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema kwamba inaleta *conflict* nyingine na Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ambayo ina-govern kuchukua maelezo ya mashahidi na hii Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai inasema *Police Officer* ni *member* yeyote wa Jeshi la Polisi na ni pamoja na Mgambo anapotimiza wajibu wake kama Polisi kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge hili. Sasa ni wazi kwamba tusi-create ukinzano mwingine kati ya tafsiri mpya na tafsiri ambayo iko kwenye Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na Kifungu cha (b), ni kweli maamuzi ya migogoro ya kibiashara yanahitaji kufanya haraka lakini waliosema “harakaharaka haina baraka” hawakukosea vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Unaendelea na mapendekezo yako ya *amendment* au tupige kura?

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yapigiwe kura ili ijulikane kwamba yamepigiwa kura na yamekataliwa na Bunge.

**MWENYEKITI:** Haya! Waheshimiwa Wabunge, naomba mnisikilize sasa, tunazungumzia mapendekezo katika Kifungu cha 4 cha Muswada wetu kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Tundu Lissu.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja ili amuliwa na Kukataliwa)*

*(Hoja ya Mheshimiwa Tundu A.M. Lissu ilikataliwa na Bunge)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya  
Bunge zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 5

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima  
bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 6

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana. Kuhusiana na Kifungu cha 6 cha Muswada napendekeza kwamba hicho kifungu cha 6(4) kifutwe na badala yake kiwekwe kifungu kifuatacho, kifungu kidogo cha 4; “Where the offence of attempted rape is committed by a person who is of the age of between twelve and eighteen years, that person shall;

- (a) If a first time offender, be sentenced to a term of three months in a reformatory centre;
- (b) If a second time offender, be sentenced to a term of six months in a reformatory centre; and
- (c) If a third time offender or habitual offender be sentenced to twelve months in a reformatory centre.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu yana lengo la kuweka ulinganifu (*consistence*) kati ya Kanuni ya Adhabu kama ilivyo na Sheria ya Haki za Mtoto. Kama nilivyosema katika hoja yangu jana, Sheria ya Haki za Mtoto iliyopitishwa na Bunge hili mwaka 2009 Kifungu cha 119(1) kinakataza watoto kupewa adhabu ya kifungo jela. Sasa mapendekezo ya Muswada ni kwamba watoto wawe wanafungwa jela, tukifanya hivyo tutakuwa tunakanusha kile ambacho Bunge hili tukufu lilikifanya miaka miwili iliyopita, hilo ni la kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kwamba kifungu cha 6(4) kama kinavyopendekezwa katika Muswada hakiweki ufanuzi huyo mtoto wa chini ya miaka

kumi na nane ni miaka kumi na nane mpaka wapi, ni mpaka mwezi mmoja, mpaka mwaka mmoja au mpaka lini? Hakuna ufanuzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hapa ni la kisheria. Kanuni ya Adhabu imeweka wazi kwamba mtoto wa chini ya miaka kumi na mbili hawezi akafanya tendo la ngono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pendelezo langu linazingatia hiyo kanuni ya *criminal responsibility* katika makosa ya ngono. Kwa hiyo, ikikubaliwa Sheria itasema wazi kuwa mtoto anayezungumziwa ni mtoto wa kuanzia miaka kumi na mbili mpaka kumi na nane ambaye anaheسابika kwamba ana *criminal responsibility*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba mapendelezo haya yakubaliwe na Bunge lako Tukufu. Asante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Asante, upande wa mtoha hoja ya Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri kwamba adhabu ambazo anapendekeza Mheshimiwa Mbunge zinatweza watoto.

**MWENYEKITI:** Kutweza ndiyo kufanyaje?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutweza ni kama zina *torture*, ni *cruel*.

**MWENYEKITI:** Aah za ukatili zaidi!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, za ukatili zaidi. Yaani sikujua kama Mheshimiwa anaweza kuwa mkatili kiasi hiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunachopendekeza ni kwa ajili ya kumsaidia mtoto *a-reform* badala ya kuanza na kifungo. Sasa Mheshimiwa Mbunge hapa amesema *if is a first time offender, be sentenced to a term of three months in a reformatory centre. Issue* hapa sio kufunga, *issue* ni kumpa huyu mtoto Mtanzania mwenzetu anayeanza kukua nafasi ya kujisahihisha. Sasa tunasema; kifungu cha 4 tunachoongeza kinasema kama huyu mtu ni mkosaji wa kwanza, basi apewe adhabu ya viboko vitano badala ya kumfunga kwa sababu ukishamaliza kumpatia viboko vitano jioni yuko nyumbani, kesho yuko shule, ndiyo maana iliyopo hapa. Halafu haya mambo ya kukimbilia kwenye *reformatory centre* yanafanya watoto wanakuwa sugu, ndiyo maana hiyo tu. Kwa hivyo ni ukatili wa ajabu kwa kuanza na kosa hilo la kifungo kwenye *reformatory centre*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya pili tunasema kama huyu mtu anarudia tena kosa hilo la kutaka kubaka basi aende jela *six months* kama ameshaanza kuwa nunda lazima aende jela miezi sita, kama anarudia rudia (*habitual*) basi aende jela miezi 12, lakini mwanzo tunafikiri viboko vinatosha na adhabu hii ni ulinganisho, hatutengenezi adhabu mpya. Tulifanya mabadiliko ya sheria kwenye eneo hili hili kuhusiana na makosa ya kubaka na umesema mwenyewe kwamba sheria hii haitoi tafsiri miaka 18 kuteremka chini inaishia wapi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Tundu Lissu, nilishakuita kwamba ni Wakili mahiri na bado siwezi kuondoa hizo fikra zangu kwamba wewe ni Wakili mahiri. Kwenye Sheria ya *Penal Code* hiyo kwamba inaishia wapi unaipata kwenye *penal code* tunaanza na msingi wa *criminal responsibility* ambayo jana pia uliisema *criminal responsibility*. Tunaanza kusema hivi mtoto wa miaka miwili, mitatu, mitano, saba, nane, tisa hawezi kuwa *criminally responsible* mpaka miaka 10, sasa ikaja *concept* ya pili ambayo pia ni ya kisheria kwamba umetumia neno lile ambalo nisingependa kulitumia, mtoto wa miaka 12 mwanaume hana uwezo wa kujamiihana, sitaki kutumia ngono kwa sababu nadhani ngono siyo neno sahihi, hana uwezo huo sasa mimi nilifanya hesabu nilifaalu masomo 13 kwenda *form five* kama unafanya hesabu *sub set* hapa ni ipi? Kama unaanzia miaka 18 sasa utaishia wapi, utaishia 10 au utaishia 12? Utaishia 12 afadhali.

Kwa hiyo, unaposema kwamba hujui miaka 18 inaishia wapi ulikuwa unakosea au samahani Mheshimiwa Mwenyekiti. Kwa hiyo, nasema kwamba miaka 18 hiyo tunazungumzia hawa watoto kati ya miaka 12 na 18 ambao katika Sheria nyingine ile ambayo tulifanya marekebisho yale tulivoleta mwaka juzi, wao wakipatikana na kosa la kubaka adhabu ni hizi, lakini Sheria ilivyo sasa huyu akipatikana na kosa la kujaribu kubaka, siyo kubaka, kujaribu *pants down* bado hajafika mahali pake unampa adhabu kubwa zaidi kuliko yule ambaye anabaka. Sasa hii haina mantiki, hilo nafikiri ungekuwa umeshalionia tusingekuwa tunarumbana hivyo kwamba yule anayebaka kosa lake ni dogo, huyu anayejaribu kosa lake kubwa *how?* Haina maana, sijui kama unanielewa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa mwalimu kama hunielewi basi nitarudisha cheti changu cha ufundishaji, lakini tunachosema ni hicho kwamba mtoto wa miaka 12 hadi 18 kwa Sheria tuliyofanya marekebisho akipatikana na makosa adhabu zake sasa ni hizi. Sasa huyu ambaye anajaribu tu yaani kujaribu tu *pants down* adhabu kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Mheshimiwa Tundu Lissu atakuwa ameshanielewa kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba kifungu hicho kibaki kama tulivyokifanyia marekebisho kwenye jedwali la marekebisho ya sheria yetu. Asante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tundu Lissu dakika tatu.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kuamini kwamba Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaamini kweli kwamba kumweka mtoto katika kituo cha mafunzo (*reformatory centre*) ni kumtweza zaidi kuliko kumfunga jela. Kama ingekuwa hivyo basi tukubaliane kwamba Bunge hili lilikosea sana lilipokataza watoto kufungwa jela chini ya Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009. Bunge limekataza watoto kufungwa jela kwa sababu kifungo cha jela ni kitendo cha ... magereza yetu siyo pikiniki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana napendekeza kwamba badala ya kuwafunga jela ambayo imekatazwa na Sheria tulioitunga humu humu ndani, watoto hawa wapelekwe kwenye vituo vya mafunzo (*reformortory centres*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na viboko Mikataba ya Kimataifa (*the convention on the rights of the child*) tumesaini inakataza *cruel* na hizo adhabu ambazo Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali anasema zinatweza. Hatuwezi tukala mkate wetu na bado tukadai kuwa tunao, hatuwezi tukasema kwamba tunakubaliana na Sheria za Kimataifa zinazohusu Haki za Watoto halafu tukaendelea kuwachapa watoto viboko kwa kutumia sheria iliyotungwa mwaka 1938 wakati wa ukoloni wakati Mikataba ya Kimataifa ya Haki za Binadamu ilikuwa bado haipo (*we cant eat our cake and still have it*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Wabunge wenzangu tunapofanya uamuzi huu naomba msimuangalie Tundu Lissu, angalieni Sheria mliyotunga miaka miwili iliyopita. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Haya kengele imegonga. Eeh, Mwanasheria Mkuu naona unataka kusema.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Tundu Lissu anafanya *reference* kwenye Sheria ya Watoto, lakini naomba nisome kifungu anachokitaja; ni kweli inasema “a child shall not be sentenced in imprisonment. That is the general rule” lakini inaendelea kusema; “where a child is convicted of any offence punishable with imprisonment the court may in additional or alternative to any other order which may be made under this Act;

- (a) Discharge the child without making any order;
- (b) Order the child to be repatriated at the expense of government to his home or district of origin if it is within Tanzania; and
- (c) Order the child to be handled over to the care of a fit person or institution named in the order, if the person or institution is willing to undertake such person.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo isije ikajengwa hoja kwamba hapa tunachofanya ni kuwafunga watoto, mamlaka haya yanaachwa kwenye mahakama kwa mujibu wa sheria hii. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa kama nilivyosema utaratibu wetu, hoja ya mtoa hoja Mheshimiwa Tundu Lissu anasema tuondoe vifungu hivi vilivyoko kwenye Muswada tubadilishe na vifungu alivyoleta yeye.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima  
pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 7  
Kifungu cha 8  
Kifungu cha 9  
Kifungu cha 10  
Kifungu cha 10B

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 11

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Kifungu cha 12

(*Vifungu viliyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 13

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tundu Lissu, marekebisho.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante. Kuhusiana na Kifungu cha 13 cha Muswada, ni mapendekezo yangu kwamba badala ya kurekebisha kifungu cha 7(8) cha Sheria ya Uchawi kama inavyopendekezwa katika Muswada, Bunge lako Tukufu litumie fursa hii kuifuta Sheria ya Uchawi kutoka katika vitabu vyetu vya Sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasema maneno yafuatayo; “*Repeal of The Witchcraft Act Cap. 18, the Principal Act is repealed.*”

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nielezee; Sheria ya Uchawi ilitungwa mwaka 1934 wakati wa Ukoloni na Sheria ya Uchawi ilikuwa inaruhusu ma-DC wa kikoloni kuondoa watu waliokuwa wanadhaniwa kuwa wachawi katika maeneo yao walikozaliwa, wanakoishi na kuwapeleka maeneo mengine ambako hawajazaliwa na Sheria hii tumekuwa nayo mpaka leo tunapozungumzia kuibadilisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka 20 iliyopita Tume iliyoteuliwa na Rais, Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, kuangalia kama nchi hii ifuate demokrasia ya vyama vingi iliangalia vilevile mfumo mzima wa kisheria unaotakiwa ili kwenda sambamba na mfumo wa demokrasia wa vyama vingi, na katika mapendekezo ya Tume ya Nyalali, tume hiyo ilipendekeza sheria nyingi (sheria zilizotajwa zilikuwa 42) kwamba zifutwe kabisa kwa sababu zinaenda kinyume na haki za binadamu, ilikuwepo pia Sheria ya Uchawi. Sasa haikufutwa na badala yake leo inapendekezwa itiliwe nguvu zaidi kwa

kutoa adhabu kali zaidi kwa wale wanaodhaniwa ni wachawi lakini hawataki kuondoka kwenye maeneo yao, hawataki kuondoka kwenye nyumba zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haiwezekani nchi hii ni nchi ya kidemokrasia, inaamini na inalinda haki za binadamu. Kama tunaamini na kulinda haki za binadamu huu ni wakati muafaka wa kuondokana na Sheria ambayo ilishatamkwa na Tume ya Rais kwamba haifai ili twende na mfumo wa kisasa zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inayoamini uchawi katika karne ya 21, karne ya TEKNOHAMA kwa kweli tutadhihakiwa kwenye Mikutano ya Kimataifa. Kwa hiyo, ili kuokoa Taifa hili na dhihaka ya Kimataifa kwamba nyie bado mnaamini uchawi kwenye karne ya 21, huu ni wakati wa kuifuta hii Sheria ya Uchawi. (*Kicheko/Makofi*)

**MWENYEKITI:** Inaonekana kama wewe mchawi mchawi hivi. (*Kicheko*)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja anayoitoa Mheshimiwa Tundu Lissu ingekuja kama hoja ya kufuta sheria rasmi ili kusudi tuichangie. Sisi tulichosema hapa ni kubadilisha adhabu. Lakini pia nadhani sio sawa sawa kushawishi, najua wewe ni mwanasiasa, mimi *I am a professional lawyer*, siangalii jimbo, naangalia kitabu cha sheria. (*Makofi*)

Baada ya Tume ya Rais kuleta mapendekezo hayo unayoyasema Bunge hili ni Bunge la Kumi, lakini Wabunge wenzenu wazima na akili zao walifanya marekebisho ili kuondoa kasoro ambazo Tume ilikuwa imesema kwamba kasoro moja Mheshimiwa Mwenyekiti utaniwia radhi, kasoro moja ilikuwa ni kwamba sheria ilikuwa haitoi nafasi kwa mtu anayetuhumiwa kutoa utetezi. Ndio maana kifungu cha 8 kikabadilishwa na Sheria namba 12 ya mwaka 1998 nilikuwepo hapa kama Msaidizi wa Waziri na sheria ikabadilishwa. Kwa hiyo, kusema kwamba hii ni sheria ya kikoloni kwa sauti kubwa namna hiyo, si sahihi. (*Makofi*)

Sheria hii ilifanyiwa marekebisho na Sheria namba 12 ya mwaka 1998 ambayo pia ilikifanyia marekebisho kifungu cha 8 kinachompa Mkuu wa Wilaya kama msimamizi wa Wilaya kushughulikia masuala haya ya kijamii yanayowasumbua watu. Nafikiri itakuwa si sahihi kusema kwamba kuamini kuwa uchawi upo ni kitendo cha ajabu. Lakini nakuomba *u-define* uchawi ni nini? Kwa sababu nafikiri hapo ndio *philosophy* ya uchawi ni nini? Labda Mheshimiwa Mchungaji Msigwa nafikiri amebobea kwenye eneo hilo, uchawi ni nini? Sheria yenye ina-*define instrument* za kichawi na ukiangalia zipo. (*Makofi*)

Nilikwenda kufundisha Malawi kwenye Mahakama ya Biashara nikaambiwa kwamba kuna mzee mmoja anafundisha watu kuruka usiku. Nikaenda pale nikakuta kuna wanafunzi. Kwa hiyo, nafikiri itakuwa ni Waingereza wenye sheria hii waliifuta mwaka gani, mwaka 1700 na kitu. Lakini *halloween* unakumbuka Amerika kuna kitu kinaitwa *halloween* mwezi wa Novemba, unajua ni sikukuu ya wachawi. Kwa hiyo, si kweli kusema kwamba hiki kitu tutaonekana ni watu wa ajabu. Kuna watu wanafanya vitendo na Mheshimiwa Mwenyekiti na Mheshimiwa Mbunge ameniletea *note* hapa na

mwenyewe anasema kwamba uchawi bwana watu wanaweza kuingia hapa Bungeni huwezi kuwaona, huwezi kumjua, *it is not scientific*. Nakubali sijui, lakini najua kwamba hawa watu hizo ndizo *elements* za uchawi. Tunachofanya hapa ni kubadilisha adhabu tu. Lakini Mheshimiwa hoja iliyopo mbele yetu ilioletwa na Mheshimiwa Tundu Lissu ni kwamba sheria hii ifutwe, hiyo sio hoja yetu sisi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, kwa maana hiyo Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Tundu Lissu unasemaje, dakika tatu.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante na wala sitatumia dakika tatu zote hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali angesaidia sana hili Bunge kama angetusomea hicho kifungu anachodai kinatoa haki kwa mtu anayetuhumiwa kwa uchawi, ingetusaidia sana. Kwa sababu hicho kifungu kinachotoa haki ya mtu kujitetea hakipo kwenye Sheria ya Uchawi na ndiyo ilikuwa sababu ya Tume ya Rais, Tume ya Marehemu Jaji Mkuu Francis Nyalali kusema kwamba sheria hii ifutwe kwa sababu ni sheria ya kukandamizana, hajabdalishwa kutoa haki kwa mtuhumiwa wa uchawi kujitetea. (*Makofi*)

Sasa kama Wamarekani bado wana *harrowing* na mimi nimekaa Marekani miaka kadhaa iliyopita sijui. Ninachofahamu ni kwamba Sheria ya Tanzania ya Uchawi haitoi *due process* ilikwishakuwa denounced by *Presidential Commission of Enquiry* kwamba ni *unconstitutional* inatufanya tunaonekana wa ajabu na hii ni karne ya 21 for god sake. Asante.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado sijafuta kauli yangu kwamba huyu ni Wakili mahiri. Kifungu cha 8(1) cha Sheria ya Uchawi kinasema kama ifutavyo, nitasema kwa Kiingereza na nitatafsiri kwa Kiswahili baadae.

“If it is reported to the District Commissioner that a person is suspected of practising witchcraft and the District Commissioner after due inquiry is satisfied that the person so suspected causes or is likely to cause fear, annoyance or injury in mind, person or property to any other person by means of pretended witchcraft or is practising witchcraft for gain or reward, he may for reasons to be recorded, order the person so suspected to reside in any specified locality within his district until such order is varied or revoked. And further or in the alternative may order such person to report to the District Commissioner or to a local authority at such intervals not being less than seven days as he shall direct, until such order is varied or revoked.”

Kwa Kiswahili kama kunatolewa taarifa kwa Mkuu wa Wilaya kwamba kuna mtu anatuhumiwa kufanya mambo ya kichawi na Kamishna, huyo Mkuu wa Wilaya akaamini baada ya kufanya uchunguzi na akaridhika kwamba huyo mtu anafanya vitendo vinavyoleta hofu maana yake uchawi ni mambo ya hofu. Unaamka unakuta paka mlangoni kwako utatoka? Hofu au maudhi unalala kitandani unaamka uko chini kazi ya

Wanyaturu hao, ehee au inaharibu akili. Haya ni kwamba hii ndio *due process* ambayo tunazungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo haya ni vizuri yashughulikiwa kwa njia hii. Lakini kifungu cha pili naomba unisikilize Mheshimiwa Lissu kwanza kwa sababu mimi unajua mwenyewe; “*Any order made under this section shall with the reasons thereof be forthwith reported the District Commissioner to the Regional Commissioner*, yaani huyu Mkuu wa Wilaya baada ya kutoa amri yake anatakiwa amjulische Mkuu wa Mkoa. Katika hiyo taarifa aliyompelekea Mkuu wa Mkoa lazima kuwe na taarifa yake ya uchunguzi. Mkuu wa Mkoa anapewa mamlaka ya kuzuia kwa muda au kubadilisha ile amri ya Mkuu wa Wilaya au Rais wa Jamhuri hii nae anaweza kutengua hizo amri zinazotolewa. (*Makofi*)

Sasa Mheshimiwa Wakili anaposema hakuna *due process*, mimi nimesoma sheria nyingi kwa sababu nilivyosema ulikuja Marekani wakati mimi nimeshaondoka sioni mantiki yako ya kusema kwamba hiki hamna *due process* hapa. *There is a due process here. Inquiry* nisamehe kama nasema kwa sauti kwa sababu mimi ni Wakili, *inquiry* ndugu yangu, *inquiry* hii ndio *due process*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, nawaoamba Watanzania, hii Sheria ya Uchawi iko kihalali kwenye sheria zetu na kwamba uko utaratibu ambao unatoa haki kwa mtu anayetuhumiwa kuonyesha kwamba yeze sio mchawi. Lakini akishindwa kuonyesha hivyo basi Mkuu wa Wilaya ana mamlaka chini ya sheria kwa kufuata utaratibu ulioanishwa ni kifungu cha 8(1) ambacho marekebisho hayo yalitokana na sheria hiyo namba 12 ya mwaka 1998.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni rai yangu kwamba kifungu hiki kama kilivyoandikwa na Serikali kibakie kama kilivyo. Ahsante Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Zaidi ya hapo Waheshimiwa Wabunge kama alivyosema Mwanasheria hapa hatutungi Sheria ya Uchawi, tunafanya marekebisho katika kifungu cha sheria hiyo.

Kwa hiyo, kusema tutakifuta kwa mujibu wa *amendment* hizi *miscellaneous*, tutakuwa hatujafuata utaratibu unaostahili. Kwa hiyo, wanaofikiria kwamba hoja aliyoileta Mheshimiwa Wakili Tundu Lissu iingie kwenye vitabu vyetu hivi waseme ndiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mbunge lakini pia ni Wakili. Wanaofikiria kwamba tuingize kifungu alicholeta yeze katika mabadiliko haya waseme ndio na wanaofikiria kwamba hakuna haja ya kuingiza mabadiliko aliyoileta Mheshimiwa Tundu Lissu waseme sio.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

*Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

(Hoja ya kukifanya mabadiliko kifungu cha 13 ilikataliwa na Bunge)

**MWENYEKITI:** Pendekezo hili nalo limefutwa. Tunaendelea.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima  
bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 14  
Kifungu cha 15  
Kifungu cha 16  
Kifungu cha 17  
Kifungu kipycha 18

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko  
yoyote)

Kifungu cha 19

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Muswada unapendekeza katika Kifungu cha 19 kufanya marekebisho katika kifungu cha 222 cha Sheria ya Mwenendo wa Jinai kwa kufuta neno *acquit* na badala yake kuweka neno *discharged*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutafanya marekebisho kama inavyopendekezwa katika Muswada basi hakuna uwezekano tena wa Mahakama kuachilia mtuhumiwa huru kwa kumfutia hatia hata kama upande wa mashtaka hautaenda Mahakamani kwa sababu yoyote ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya kukubali mapendekezo haya yatakuwa ni kufunga milango kwa ukatili mkubwa dhidi ya haki za watu wetu. Itakuwa ni sawasawa kisheria kama Muswada huu utapitishwa kama inavyopendekezwa itakuwa ni sawa sawa kisheria kwa Mahakama inamwachilia huru kwa kumfutia kesi kwa kum-*discharged* mtuhumiwa akifika kwenye *gate* la Mahakama anakamatwa anarudishwa tena anashtakiwa, anakaa Magereza pengine miezi sita au 10 au miaka mitatu anaachiliwa anarudishwa tena *it will never end*, itakuwa ni kufunga mlango kwa *serious abuses of human rights*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Bunge hili linapoamua juu ya kufanya hivyo mfikirie *consequences* za kufunga milango namna hii ya kisheria. Kwa hiyo, katika Kifungu cha 19 napendekeza hicho kifungu kiondolewe kabisa ili sheria kama ilivyo leo, sheria yetu kama ilivyo leo kifungu cha 222 kinasema “Mlalamikaji asipokwenda Mahamani wakati anafahamu tarehe ya kesi anafahamu kesi itafanyikia wapi, hana sababu yoyote ya maana ya kutokwenda Mahakamani, Mahakama itamfutia hatia

mshtakiwa na akifutiwa hatia maana yake ni kwamba hataweza kushtakiwa kwa kosa hilo hilo kwa tendo hilo hilo. (*Makofi*)

Kifungu hicho kilitungwa na Bunge ili kulinda haki za watuhumiwa, sheria zetu zinaamini *presumption of innocence*, mtu asije akakaa Magereza awe anatuhumiwa makosa ya jinai wakati wale waliomshtaki hawaonekani Mahakamani. Kwa hiyo, ili kulinda haki za wananchi wetu naomba Bunge lako Tukufu lisifanye marekebisho kama inavyopendekezwa. Naomba Waheshimiwa Wabunge wa upande wa pili, msimuangalie Tundu Lissu, angalieni maelfu ya Watanzania walioko Magerezani. Nashukuru. (*Makofi*)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo fulani hapa nchini watu wanaweza kujigeuza fisi yaani ikawa mbojo, Singida kule kuna kitu kinaitwa mbojo.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani naomba mwongozo wa kiti chako. Hii ni mara ya pili Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali badala ya kujibu hoja anasema watu wa Singida, watu wa Singida. Watu wa Singida hawako kwenye mjadala hapa, samahani. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahaa!!! Sisi tunajua mnafahamiana kwa vilemba. Waarabu wa Pemba wanafahamiana kwa vilemba. (*Kicheko*)

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Hii ni *serious business*.

**MWENYEKITI:** Nikiambiwa mimi ningekasirika kweli maana sio mwarabu wa Pemba. (*Makofi/Kicheko*)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Nilikuwa sijafika huko nilikokuwa nakwenda, lakini nikuombe radhi kama nimekukosea. Kila mtu ana nyongo kasoro Yesu na Mtume Muhammad. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri hoja inayojengwa hapa ni kama vile Serikali inataka kufanya haya Mheshimiwa Lissu anayosema. Tunachofanya ni nini, naomba muangalie kwenye *schedule* ya Serikali *para G*, tunachofanya. Tunafuta neno *acquit* kwa sababu ukisema *acquit*, kama mtu kesi imekwenda Mahakamani halafu *accused person* amekuwa *acquitted*, ina maana kwamba mashtaka yake hayaendelei tena. Tunachofanya ni kwamba badala ya *ku-acquit awe-discharged* ili kwa sababu kama huyu atarudi akiwa na sababu basi uweze kurudisha lile kosa.

Sasa tunasema hivi kinachofuata kwenye tano tunatoa mamlaka kwa Mahakama kupima sababu zinazotolewa na huyo mtu. Ndio maana nilianza na ule mfano labda kwa sababu nimetaja Singida kwa bahati mbaya. Lakini mambo ambayo yanafanywa mtu asifike Mahakamani siku zote yanatofautiana. Wewe unakwenda Mahakamani ukafika mahali ukapata ajali Mahakama zinaanza kazi saa 3.00 au kwenye foleni umechelewa Mahakamani, sasa kesi inafutwa yaani huyu mshtakiwa anakuwa *acquitted*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachosema ni kwamba uende upate nafasi ya kurudi Mahakamani na ukafanye *application* wala sio *certificate* kama mapendekezo ya Mheshimiwa Tundu Lissu anaposema. Kwa sababu ukisema *certificate* ndio sasa unakaribisha tena kwamba wafanye Mawakili hapa hatutengenezei mtu fedha tunataka huyu mtu mwenyewe arudi afanye hayo maombi kusudi hiyo kesi iweze kuendelea na hapa tunasema waendesha mashtaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, waendesha mashtaka ni Mawakili wa Serikali na watu wengine binafsi. Unaweza kuwa na sababu ya msingi kwa nini hukwenda Mahakamani tunaiachia Mahakama ipime hizo sababu. Tunasema *where the court dismiss the charge and discharge the accused person under section 222 or 226 the complainant may tunaweka muda within 30 days from the date of the dismissal, file an application for reinstatement of the charge.* (*Makofi*)

Kwa hiyo, tumeweka muda kwamba ikipita miezi 30 hawezi kufanya na Mamlaka ya kuamua kama kuna sababu za msingi tunaiachia Mahakama. Kwa hiyo, sio sahihi kusema kwamba tunanyang'anya Mamlaka Mahakama ya kuamua kuhusu suala hili. Tunachosema huyu mtu anayelalamika inaweza kuwa ni wewe una kesi Mahakamani ulipigwa mahala ukashtaki, anakutetea Wakili wa Serikali hakufika Mahakamani kesi inafutwa utaumiza Watanzania wasio kuwa na makosa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, tunampa huyu mtu ambaye huyu Wakili hakufika Mahakamani aweze kumwambia Wakili twende akatoa sababu na kama Wakili anakataa nakwenda kwa mtu mwingine. Haya ndiyo mamlaka tunayatoa na Serikali imefikiria kwa sababu kuna matatizo. Hapa hatumwangalii Wakili wa Serikali tunamuuliza kwa nini hukufika. Tunaangalia yule ambaye analalamika ambaye kesi yake inaendeshwa na Wakili wa Serikali kusudi Wakili wa Serikali akienda aseme kwa nini hakufika Mahakamani na mwenye mamlaka ya kusema tunakubali si Wakili wa Serikali ni Mahakama wenyewe. Kwa hiyo, zile *power* za Mahakama bado zipo. Huyu ndiyo atakayeamua na si Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri kwenye kifungu cha sita pale kipyaa nasoma kwa kiingereza; "*the court may (inaweza Mahakama) upon being satisfied that the complainant absence was due to reasons to which the complainants had no control or could not within the circumstances to have control grant an application for reinstatement of the charge and proceedings if any.*"

Nongwa nini? Hapa hatusemi kwamba ni *open ended, this is not an open cheque.* Anatakiwa kuitosheleza, kuiridhisha Mahakama kwamba mimi nilichelewa kwa sababu a, b, c na inafanyika hivyo kwenye kesi hizi za madai. Tunachosema sasa ni kwamba ifanyike pia kwenye *criminal cases.* Kwa hiyo, haya ndiyo marekebisho ambayo sisi tunapendekeza na tunadhani kwamba yanatija. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye haya ambayo Mheshimiwa Tundu Lissu anapendekeza tunasema *where no certificate is filed under the provision of subsection four, the court shall acquit.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkoo hiyo ni Ibara nyingine. Yeye alikuwa anataka tufute.

**MWANASHERIA MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napendekeza kwamba yabaki kama yanavyoonekana kwenye marekebisho tulioleta.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tundu Lissu dakika tatu.

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante. Kifungu cha 222 cha Sheria ya Mwenendo wa Jinai kama kilivyo sasa hivi Mahakama haina *automatic powers* za kufuta hatia kwa sababu kifungu hicho kinasema kwamba Mahakama inaweza ikaahirisha kesi badala ya kumfutia mtuhumiwa hatia Mahakama inaweza kama inaridhika kwa sababu maalum kwamba huyu ambaye hakuja Mahakamani ana sababu za msingi basi Mahakama inaweza ikaahirisha kesi ikaipangia siku nyingine ya kusikilizwa.

Kwa hiyo, *does not follow automatically* kwamba Mwendesha Mashtaka asipokuja hata kama ana sababu za msingi basi kesi yake inafutwa, sio hivyo. Sheria kama ilivyo *ina-safeguard* za kutosha kwa pande zote inalinda haki za mtuhumiwa ambaye kesi yake inachukua muda mrefu kwa sababu waendesha mashtaka hawafiki Mahakamani na vilevile kama kuna sababu za msingi Mahakama bado inaweza ikaahirisha kesi badala ya kufuta hatia ya mtuhumiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimemsikia Mwanasheria Mkoo wa Serikali akisema kwamba hata tukibadilisha hilo neno *discharge* bado wanatakiwa wapelekewe maombi Mahakamani, ndivyo inavyopendekezwa. Sasa tatizo la mapendekezo haya yanayoletwa na Serikali ni kwamba watapewa *application* mara ya kwanza, hawaendi Mahakamani, Mahakama inam-*discharge* huyu mtuhumiwa, wanapeleka maombi mengine ndani ya siku 30 inarudishwa. Huu mchezo hautaisha na bahati mbaya labda nitangaze maslahi sijui. (*Makofi*)

Mimi nafanya sana kazi ya msaada ya kisheria kwa wananchi amba hawana lolote, hawana uwezo wa kifedha wa kulipa Mawakili na hawa ndiyo amba wanafungwa siku zote, hawa ndiyo wanaowekwa ndani, wanakaa magereza kwa miaka. Asante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo mapendekezo ya Mheshimiwa Tundu Lissu yamewekwa pemberi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima  
bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 20

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 20 cha Muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 226 cha Sheria ya

Mwenendo wa Jinai kwa kufuta maneno *acquit* (kufuta hatia) na badala yake kuingiza maneno *discharge*. Kama nilivyosema kuhusiana na mapendekezo ya kifungu cha 19.

## T A A R I F A

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sioni mapendekezo haya anayosema kwa sababu mapendekezo yaliyokuwepo hapa ni *amendment of section 225 halafu (c) ana-renumber clause 1- 42 as clause 20 – 41*, halafu kwenye (e) anasema *in Part XII by deleting the whole of that part*. Hayo marekebisho anayosema mimi sina. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Huna *page two* ya mabadiliko yake? Kuna *page two* ya mapendekezo ya Mheshimiwa Tundu Lissu. *Page two* ina (c) kubwa na (d) *Part IV* ndiyo tuko kwenye *Part IV* sasa hivi; (a) aliomba tu-*delete* kifungu chenu cha 19, tupo *Part V* sasa. Kwa hiyo, tumemaliza hiyo lakini sasa tupo kwenye (b) ndiyo alikuwa anaendelea kusema. Mheshimiwa Tundu Lissu endelea.

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kumsaidia Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika D(a) tunesema kwamba *by deleting clause 19 and 20 as renumbered*. Sasa tume-deal na *clause 19*, kifungu cha 20 tumekuwa hatujaishughulikia. Nafikiri ndiyo shida ya hiyo.

**MWENYEKITI:** Kuna Kifungu cha 19 kipyä ambayo kilikuwa cha 20 zamani, halafu kuna kifungu cha 20 kipyä ambacho kilikuwa kifungu cha 21. Kwa hiyo, wewe unazungumzia kifungu cha 20 cha zamani. Tumelewana.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisaidie tu, kwenye Muswada nafikiri kifungu cha 22 ambacho *kina-amend section 245* ambayo kuna marekebisho kwa upande wa Serikali kwenye (h), tunafuta maneno *the high court or 2000/= shillings in the case of appearing the third line of paragraph (a)*. Sasa baada ya hapo haya marekebisho ambayo Mheshimiwa Tundu Lissu anayafanya yanayuhusiana na kifungu cha 225 wala si kifungu cha 226. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Halafu pia Mheshimiwa Tundu Lissu ulipokuwa unafanya *amendments* ulipokea *amendments* za Serikali?

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea hii *schedule of amendment* jana na sehemu (g) ya *schedule of amendment* niliyopata inasema *by deleting clause 19 as renumbered and substituting for it the following 20 the Principle Act is amended in section 226* na ninachosema ni hicho ambacho kimependekezwa katika

*schedule of amendment* kiondolewe. Kifungu (g) 20 na mapendekezo yangu ndivyo yanavyosema sema *by deleting clauses 19 and 20 as renumbered*. Kwa hiyo, ni kile kile.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkoo wa Serikali umemuelewa?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemuelewa lakini ukisoma kwenye tumbo la maeneo yake ana-refer kwenye section 225, *the Principle Act is amended in section 225*, yeye anasema 226.

**MWENYEKITI:** Serikali inasema 225 Mheshimiwa Lissu anasema 226. Sasa *which is which?*

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda sijui tuta-resolve namna gani hii. Kwenye *schedule of amendments* ya kwangu kuna para (a), para (a) inasema *delete clause 19 and 20*. Sasa tumeshazungumzia clause 19 na tulikuwa tunaenda kwenye clause 20 ndiyo inayohusu section 226 and then kuna paragraph (b) ndiyo inahusu *introduction of new section of 225*, hatujafika huko bado. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Kwenye amendment hakuna 225 haipo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatukupendekeza marekebisho yoyote kwenye kifungu hicho.

**MWENYEKITI:** Haipo kwenye 225?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Taarifa Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Ngoja kwanza tu-sort out problem tuliyonayo. 225 katika amendment zote haipo. Wewe ulikuwa una-refer ipi? Labda utueleze. 225 is not there so you can explain to us how did you get it? Unafungua kitabu, sisi tunataka kujua umeitoa wapi? (*Makofî*)

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nisome nilikoitoa. Utanifanya nisome Kanuni lakini niseme nimeleta hii *schedule of amendment* inayohusiana na hicho kifungu 225 kwa mujibu wa Kanuni labda itachukua muda kuitafuta inayosema kwamba mjadala wa Muswada utamudu kuboresha misingi ya Muswada.

Kwa hiyo, *in my mind* nilikuwa nafikiri kwamba kufanya mabadiliko katika kifungu cha 225 (4) ni sehemu ya kuboresha Muswada. Sasa inawezekana nimekosea and I am not God. (*Makofî*)

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANA:** Muongozo wako Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Muongozo kuhusu nini? Sisi tunajadiliana na hoja ya Mheshimiwa Tundu Lissu sasa muongozo inakuwaje? (*Makofî*)

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipaye ufanuzi kwa sababu mara nyingi tukiwa tunajadili Miswada yetu inakuwa na nafasi katika Kamati ili kupunguza muda wa kujadiliana hapa Bungeni. Napenda nifahamu kama Mheshimiwa Tundu Lissu alishawahi angalau kwenda kwenye majadiliano ili kusaidia Bunge kupunguza muda wa kujadiliana humu ndani na muda haututoshi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ni kweli lakini ni haki pia ndiyo maana kuna kifungu cha kuweza kunaniihi. Anachokisema sasa hivi Mheshimiwa Tundu Lissu kwamba yeze alileta mabadiliko mapya katika Muswada huu. Sasa hukutueleza, kwanza tueleze halafu tutafikia hatua zake.

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimeleta hoja mbili katika *para (a)*. Hoja ya kwanza inahusu Kifungu cha 19 ambacho kimeshafanyiwa maamuzi. Kilichobaki nu kifungu cha 20, sasa kifungu hiki ambacho hakijafanyiwa maamuzi inahusu mapendekezo ya kubadili kifungu cha 226 cha Sheria ya Mwenendo wa Jinai. Hicho hakijafanyiwa maamuzi bado. Kwa hiyo, nilikuwa nataka tuifanyie hii maamuzi halafu sasa hii mpya ambayo nimeleta ndiyo ifuate. Twende kufuatana na utaratibu ambao umekuja kwenye *schedule of amendments*. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Sisi tumeshafuta ile ya kwako ya mwanzo tumekataa. Kwa hiyo, tulikuwa tunaingia (b) yake. Sasa zilikuwa *related* au ziko tofauti? Kwa sababu wewe una-*introduce a new subject* ya 225 na wenzio wamefanya *amendment 226*. Sasa hapo wewe una-*amendment* ya Serikali kwa mtindo upi.

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kukusaidia kusudi tuondokane na huu mkanganyiko. Naomba nifute *paragraph (b)* ya *schedule of amendment* ili sasa tuzungumzie kifungu cha 20 ambacho hakijafanyiwa maamuzi.

**MWENYEKITI:** Sisi tumefanya kifungu cha 20.

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujafanya kifungu cha 20 tumefanya kifungu cha 20.

**MWENYEKITI:** Ndiyo tunaingia sasa, ndiyo *argument unayofanya* wewe sasa unasema tuondoe ipi?

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema tuonde (b) ile 20 iko (a) ukisoma by *deleting clauses 19 and 20 as renumbered*.

**MWENYEKITI:** Eleza halafu sisi tutajua nini cha kufanya.

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa sawa. Kwa hiyo, naomba niiondoe hiyo ambayo inaleta rabsha ya *paragraph (b)* iondoke kabisa twende na kibaki kifungu cha 20 cha Muswada kinachohusu kifungu cha 226 na kama nilivyo sema.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sahamahi sio ustaarabu *ku-interfere* wakati Mheshimiwa Mbunge anazungumza. Mimi nafikiri mapendekezo ya Mheshimiwa Tundu Lissu yamekwisha. Kwa sababu kwenye D pale amefuta ile (b) halafu kwenye C ana-renumber vifungu vyote hivyo halafu pendeleko ni ile ya (e) ambayo hatujaifikia.

**MWENYEKITI:** Mimi nilitaka aeleze kwanza halafu tumuelewe vizuri. Mheshimiwa Lissu naomba uendelee.

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 20 cha Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 226 cha Sheria ya Mwenendo wa Jinai kwa kufuta maneno ya *acquit* na kuyabadilisha maneno *discharge*. Hio ndiyo ambayo ninaomba iwe *deleted*.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia *schedule of amendment* iliyowasilishwa Bungeni ambayo mimi ninayo. Kwenye ukurasa wa pili pale hakuna *anything to do with* 226 na ile 225 ndiyo tumeikataa, sisi hatukuleta marekebisho hapo. *I think is also fair* na naona umeanza hiyo kazi kuwa mkweli kwamba hujafanya mapendekezo yoyote kwenye hii *schedule* 226 hukufanya humu.

**MWENYEKITI:** Kwa sababu uki-delete humu kama alivyopendekeza kwamba tu-delete Part V(b) umeondoa chote kinabakia (c) ambayo nayo umesema *just the renumbering*. Kwa hiyo, unakuta kwamba haya maneno tukishaondoa wewe huna kitu. *There is nothing here*. Kwa sababu tuki-delete hiyo Part V (b) hiyo na (d) ndogo ambaye is not applicable katika mapendekezo haya wewe huna kingine.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Kifungu kipyta cha 21

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Kifungu kipyta cha 22

Kifungu kipyta cha 23

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu kipyta cha 24

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Kifungu kipyä cha 25  
Kifungu kipyä cha 26  
Kifungu kipyä cha 27  
Kifungu kipyä cha 28  
Kifungu kipyä cha 29

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima  
bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu kipyä cha 30

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima  
pamoja na marekebisho yake*)

**NDG. NENELWA MWIHAMBI - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kilichokuwa kifungu kipyä cha 31 kinafutwa, na badala yake kile kifungu cha 33 ndiyo kinakuwa kifungu cha 31.

Kifungu kipyä cha 31

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima  
bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu kipyä cha 32

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima  
pamoja na marekebisho yake*)

Kifungu kipyä cha 33  
Kifungu kipyä cha 34  
Kifungu kipyä cha 35

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima  
bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu kipyä cha 36  
Kifungu kipyä cha 37

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na  
mabadiliko yake*)

Kifungu kipyä cha 38

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima  
bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. NENELWA MWIHAMBI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya 11 ambayo ilikuwa na vifungu vinya 39 na 40, inafutwa na badala yake Sehemu ya 12 ndiyo inakuwa Sehemu ya 11 na ina kifungu cha 39.

Kifungu kipyta cha 39

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na  
marekebisho yake)*

Kifungu kipyta cha 40

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima  
bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. NENELWA MWIHAMBI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Sehemu Mpya inayoongezwa ya 12 ambayo ina kifungu cha 41.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Attorney General*, ile tuliamiwa kwamba mliingiza haikuwepo kwenye *original*.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kile, kile sehemu inafutwa, ile *amendment of the Wildlife Conservation Act*, tumeiondoa. Asante, nashukuru! (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, hicho kifungu, *part* hiyo imeondolewa kwa sababu zilizotolewa kwanza.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na mapendekezo ya Mheshimiwa Tundu Lissu, lakini nafikiri na yenyeewe sasa yanakuwa yamekwisha.

**MWENYEKITI:** Eeh, yameondolewa kwa sababu *part* imeondolewa.

*(Bunge lilirudia)*

**(Muswada wa Sheria kwa ajili ya kufanya marekebisho katika Sheria Mbalimbali**  
**(A Bill for an Act to Amend Certain Written Laws)**

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kuwa Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Marekebisho ya Sheria

Mbalimbali wa mwaka 2011 (*The Written Laws Miscellaneous Amendments Act, 2011*) kifungu kwa kifungu na imeukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika. Hivyo basi, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa mwaka 2011 (*The Written Laws Miscellaneous Amendments Act, 2011*) kama ulivyorekebishwa au kubadilishwa katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:**  
Mheshimiwa Spika, naafiki. (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Muswada wa sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa Muswada huu umepita hatua zote. Kama mnavyoona hii hatua ya tatu tunafanya tu ku-*confirm* kwamba tumepitia, tumemaliza. Lakini hatua kubwa ni ile Kusomwa Mara ya Kwanza, halafu unatakiwa usipitiwe katika Bunge lile lile yaani kikao kile kile, inabidi uje baadae. Kwa hiyo, huu Muswada umepita hatua zake zote. Napenda kuwapongeza walioandaa na Kamati iliyoshughulikia Muswada huu na nampongeza Mheshimiwa Tundu Lissu kwa kufanya kazi ya ziada. Ndivyo tunavyotakiwa kubadilika na kufanya kazi kama inavyostahili, isipokuwa, wanakubaliana na maamuzi ya Kamati, halafu mmoja wa Wajumbe wa Kamati anakuwa siyo mmojawapo. (*Makofi*)

Sasa hili nimeliona ni tatizo. Inaonekana ni tatizo kwa sababu kama atakuwa ni *member* wa *committee* inayohusika, wakati huo Kamati imekubaliana kwamba tunaleta hapa kwa makubaliano ya *two third*, halafu *one member* wa Kamati hiyo anakuja tena anakuwa *just the other way round*. Nadhani hili itabidi tuliangalie vizuri kwa taratibu zetu wenywewe. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, asubuhi tulikuwa na uchaguzi, sasa nitaongeza muda mpaka atangaze yale matokeo yote. Msimamizi wa Uchaguzi!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, samahani, nina tangazo kidogo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Kuhusiana na hili?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, hapana, nina tangazo tu la dharura.

**SPIKA:** *Okay*, dharura!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, nimeletewa *message* hapa ili Wajumbe tu wajue wasije wakaona hawakuonekana kwenye televisheni. Wananiambia kwamba, naomba kunukuu: “Jioni tumepata tatizo la mtambo wa kurusha matangazo ya Bunge toka Dodoma. Kuna kifaa kimeharibika, lakini tunayo *spare* yake, tunaipeleka usiku huu Dar es Salaam. Itafungwa asubuhi, matangazo ya asubuhi yaweze kurushwa kesho. Tunaomba radhi sana kwa Mheshimiwa Spika na Bunge kwa tatizo hilo ambalo hatukulitarajia.” Hili ni tangazo kutoka *TBC*.

**SPIKA:** Haya, leo hatutaonekana. Matangazo ya uchaguzi. Sasa mnashangilia nini Waheshimiwa?

**MBUNGE FULANI:** Ni hasara ya Tundu Lissu! (*Kicheko*)

**SPIKA:** Haya, naomba tusikilize matokeo ya uchaguzi.

**NDG. JOHN JOEL – MSIMAMIZI WA UCHAGUZI:** Mheshimiwa Spika, asubuhi tumefanya uchaguzi katika maeneo manne. Naomba nitoe matokeo ya kura zilizopigwa asubuhi kwa makundi yote manne kama ifuatavyo:-

Kundi A lilikuwa ni la Wabunge Wanawake. Kura zilizopigwa zilikuwa 275, kura zilizoharibika zilikuwa ni kura tatu na matokeo ni kuwa Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa alipata kura 129, Mheshimiwa Bernadeta Mushashu alipata kura 143. Kwa hiyo, kwa Kundi A aliyechaguliwa kuliwakilisha Bunge la Tanzania katika Bunge la Afrika ni Mheshimiwa Bernadeta Mushashu. (*Makofi*)

Kundi B lilikuwa ni la Wabunge wa Zanzibar. Kura zilizopigwa zilikuwa ni 277, kura zilizoharibika zilikuwa tano na matokeo yake yalikuwa kama ifuatavyo, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh amepata kura 55, Mheshimiwa Mhandisi Hamad Yussuf Masauni amepata kura 217. Hivyo, Bunge limemchagua Mheshimiwa Mhandisi Hamad Yussuf Masauni kuliwakilisha Bunge la Tanzania katika Bunge la Afrika. (*Makofi*)

Kundi C lilikuwa ni la Wabunge wa Tanzania Bara kuwapata Wabunge wawili. Kura zilizopigwa zilikuwa 278, kura zilizoharibika ni 14 na matokeo ni kama ifuatavyo, Mheshimiwa Deogratius Ntukamazina amepata kura 78, Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangalla amepata kura 114, Mheshimiwa Luhaga Mpina amepata kura 151, Mheshimiwa Stephen Masele, amepata kura 185. Hivyo, Bunge limewachagua Mheshimiwa Stephen Masele pamoja na Mheshimiwa Luhaga Mpina kuwa Wabunge wa Bunge la Afrika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kundi la mwisho lilikuwa ni Wabunge wa Kambi ya Upinzani na matokeo yake ni kama ifuatavyo, kura zilizopigwa zilikuwa ni 267, kura zilizoharibika zilikuwa tatu. Matokeo yake ni kama ifuatavyo; Mheshimiwa Moses Machali amepata kura 38, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa amepata kura 226, kwa maana hiyo,

Bunge limemchagua Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa kuwa mwakilishi wa Bunge letu kwa upande wa Kambi ya Upinzani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wawakilishi wote kwa pamoja wanaowakilisha Bunge ni watano, Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, Mheshimiwa Hamad Yussuf Masauni, Mheshimiwa Stephen Masele, Mheshimiwa Luhaga Mpina na Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa chaguzi zile nyingine, Wabunge walipita bila kupingwa. Kwa Bunge la *SADC* ni Mheshimiwa Stella Manyanya na kwa uwakilishi katika Baraza la Uongozi wa *APRM* ni Mheshimiwa Martha Umbulla. (*Makofi*)

**SPIKA:** Taarifa hiyo imesainiwa na wale wote tuliowaomba wawe mawakala wenu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, napenda nichukue nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa wote hawa kwa kuchaguliwa kwao katika ngazi hii. Wakati huo huo nadhani tulishatangaziwa kwamba wale watakoakuwa wanamsaidia Spika katika kuendesha shughuli hii walitajwa asubuhi kuwa ni Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa George Simbachawene hawapo kwa sasa wanaendelea na *public hearing* na Mheshimiwa Sylvester Mabumba. Kwa hiyo, kwa ujumla upande wa Spika, sasa hivi tuna timu yote, tunaweza kufanya kazi kwa urahisi zaidi kuliko siku zilizopita. Kwa hiyo, naomba niwapongeze sana. (*Makofi*)

Bunge la Afrika nafikiri linatakiwa kukaa mwezi ujao, kwa hiyo, safari hii tutakuwa *represented*. Bahati mbaya ni kwamba Wabunge wote ni wapya, kwa hiyo tunawasihi wakafanye kazi ya ziada kabisa kuweza kuchukua nafasi mbalimbali katika Bunge hili kwa sababu Bunge la mwisho sisi tulichukua *Presidency* na Wabunge wengi hapa walichukua nafasi mbalimbali katika Kamati za huko. Kwa hiyo, naamini kabisa hawa waliochaguliwa ni watu makini kabisa, watakwenda kuchukua nafasi mbalimbali katika maeneo hayo. Kwa hiyo, mimi naomba niwapongeze. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, ili kumalizia suala la *SADC*, hapa msimamizi wa uchaguzi anatangaza kwamba kesho wanaopenda kugombea nafasi iliyobaki ya *SADC* ni wanaume kutoka Chama Tawala, wachukue fomu, zinapatikana na mwisho wa kurudisha fomu ni saa 10.00 jioni kesho, uchaguzi utafanyika tarehe 15. Kwa hiyo, wale wanaotaka kuchukua fomu wakachukue huko kwa Katibu kwa utaratibu unaohusika. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, leo kazi ilikuwa nzito, nilifikiria ingeweza kumalizika upesi, lakini hatukufanikiwa. Nawashukuru sana kwa kazi zote. Napenda kuahirisha kikao cha Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

(*Saa 1.42 usiku Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Alhamis,  
Tarehe 14 Aprili, 2011 saa tatu asubuhi*)

